

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA SABA**

**Kikao cha Tano - Tarehe 8 Novemba, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Kabla hatujaanza kikao, Waheshimiwa Wabunge, nina Mgeni wa Kimataifa wa kumtambulisha.

*I would like to recognise the presence in the Diplomatic Gallery of His Excellence is a Nigeria High Commission to Tanzania who is Abdulmumin Abubakar.*

Vile vile kabla hatujaanza, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu, anapokuwa hayupo Bungeni kuhudhuria vikao huwa Bunge linajulishwa. Sasa ninayo barua ya Mheshimiwa Waziri Mkuu anasema: “Nimekwenda Dar es Salaam kwa shughuli za kikazi. Nitakuwa huko kuanzia tarehe 8 Novemba, 2004 na kurejerea Dodoma tarehe 10 Novemba, 2004. Wakati sitakuwepo atakayekaimu shughuli za Serikali Bungeni ni Mheshimiwa Anna Margereth Abdallah, Waziri wa Afya.” *(Makofi)*

Na. 60

**Mapambano dhidi ya UKIMWI**

**MHE. ABU T. KIWANGA** aliuliza:-

(a) Pamoja na jitihada za Serikali za kupambana na UKIMWI, je, Serikali haioni kwamba si vyema kutumia fedha nyingi kwa watu ambao hwajaathirika kwa makongamano na matangazo yanayohamasisha ongezeko la ugonjwa huo; na vile vile ione sababu ya kurekebisha tangazo la “USIONE SOO” kwa kuyaondoa maneno “SEMA NAYE” na matamanisho ya ngono yanayodhihirishwa na watangazaji wale wawili wa kike na wakiume?

(b) Kwa kuwa hapo awali kondomu ilijulikana kama *Duress*, je, Serikali haioni kuwa ni vyema kuendelea kutumia jina la *Duress* badala ya kondomu au kutumia jina

lingine la kistaarabu ambalo litakuwa na mantiki ya kuzuia ngono zembe kuliko kutumia neno kondomu ambalo lina mantiki zaidi kwenye uhalifu wa kuchochea ngono?

(c) Tangu janga la UKIMWI liingie Tanzania hapo mwaka 1986; je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kupambana na janga hili na kuwahudumia waathirika kwa vitendo badala ya maneno matupu ya kusemea UKIMWI tu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM W. LUKUVI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tafiti zimeonyesha kuwa watu wenye virusi vya UKIMWI ni wachache sana wakilinganishwa na ambao hawajaathirika. Lengo la uhamasishaji ni kuwasalimisha ambao hawajaathirika na kupunguza wagonjwa wa baadaye wakati waliothirika wanasaidiwa kwa hali na mali. Kwa hiyo, ni busara kutumia fedha kwa makundi yote mawili kadri ya mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, tutalitazama tena kama nilivyoahidi wiki iliyopita tangazo la Usione Soo, Sema naye kwa lengo la kulifanyia marekebisho kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge walikuwa wamependekeza na ninayo taarifa nimejulishwa na waandalizi wa tangazo hili kwamba wamebuni tangazo jipya ambalo limeanza kurushwa kwenye *Radio One* kuanzia juzi Jumamosi, tarehe 6 Novemba, 2004.

Juzi wakati Mheshimiwa Rais alipokuwa Singida anafungua Hospitali ya Misheni, wote tumesikia yeye anapendekiza badala ya kusema Usione Soo, anasema Uone Soo. Nafikiri tutatumia maneno yake ya busara wakati tunafikiria kurekebisha tangazo hili.

(b) Mheshimiwa Spika, neno sahihi ni *Durex* ambalo ni jina la kibiashara linatotumiwa na watengenezaji wa kondomu. Yapo majina mengine, kwa mfano Salama na kadhalika. *Durex* zilikuwa kondomu za mwanzo hapa nchini na jina hilo likatumika sana kama tunavyotumia bukta kwa maana ya kaptura. Jina kama lilivyo halina ubaya, ila mtumiaji anaweza kulitumia vibaya.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inawahudumia wagonjwa wa UKIMWI kwa Mpango Maalum wa Matibabu kupitia Wizara ya Afya. Serikali imetoa shilingi bilioni 2.0 ili kuanzisha mpango huo wa tiba. Misaada mingine inategemewa kutoka Benki ya Dunia, Mpango wa Rais George Bush wa Marekani, Rais Mstaafu Bill Clinton, Mfuko wa Kimataifa wa kudhibiti UKIMWI, Tiba na Malaria na wadau wengine wa maendeleo.

Tiba itatolewa katika hospitali zilizoteuliwa zenye uwezo wa kumudu tiba hiyo na watakaopatiwa tiba ni wale ambao wamepimwa na kuonekana wanahitaji dawa za kurefusha maisha (*ARVs*).

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa watu binafsi, asasi mbalimbali pamoja na mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya kila wawezalo kuwasaidia waathirika na yatima. Jukumu hili ni letu sote na lisionekane kuwa ni la Serikali peke yake.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nilikuwa na swali moja la nyongeza. Taarifa iliyokuwepo ni kuwa Uganda hivi sasa imeweza kudhibiti kasi ya ugonjwa wa UKIMWI, kwa hiyo, kusema kuwa ni tunatumia kwa ajili ya kuzuia ongezeko kwa matangazo na tiba, iwapo Uganda imeweze kupunguza kasi kwa kushughulikia zaidi waathirika, je, Serikali ina mtazamo gani kwa mwelekeo wa mafanikio haya Uganda?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abu Kiwanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunazo taarifa kwamba wenzetu Uganda walianza mapema na wamejitahidi sana, lakini pia hata hapa kwetu tumejitahidi sana. Niliahidi wiki iliyopita kwamba, wiki hii *TACAIDS* na Wizara ya Afya watatangaza rasmi takwimu ya tathimini mpya ya Tanzania ya hali ya maambukizo ya UKIMWI. Mtakaposikia hizo taarifa mtaona kabisa kwamba hata hali ya Tanzania imepungua sivyo ambavyo takwimu zinaonyesha hivi sasa.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Napenda kuuliza swali dogo la nyongeza. Kutokana na takwimu za sasa ambazo bado *TACAIDS* na wengine hawatoa takwimu mpya. UKIMWI unaongezeka siku hadi siku na kutokana na jinsi ambavyo mapambano yanavyoendelea inaimanisha kwamba nguvu zetu kutokana na UKIMWI zinarudi nyuma na UKIMWI unaenda mbele, je, haiwezekani sasa hivi kufanya tathimini mpya na kuweza kuangalia upya je, mipango yetu tuliyoifanya katika Mitaa yetu, katika Majumba yetu na katika tabia zetu kwamba tubadilisha ili twende njia nyingine ili tuweze kupambana vizuri zaidi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Juma Mtupa Mikidadi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa maambukizo mengi yanasababishwa na tabia zetu. Kwa hiyo, naunga mkono wazo la Mheshimiwa Mbunge kwamba lazima tuendeleo kujizatiti na kuhakikisha kwamba wote kwa pamoja tunashirikiana katika kuhakikisha kubadilisha tabia zetu ambazo zinasaidia kwa kiasi fulani maambukizo dhidi ya UKIMWI. Lakini juu ya takwimu, narudia tena kwamba kwa takwimu, nataka Waheshimiwa Wabunge tsubiri kidogo tupate takwimu mpya ili tuweze kujipanga upya tuone je, tunaendelea namna gani.

## **Madhara ya Njaa - Mkoa wa Mtwara**

**MHE. ABDILLAH O. NAMKULALA (k.n.y. MHE. LYDIA T. BOMA)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa, ukame ulioikumba nchi yetu katika kipindi cha mwaka 2000/2004 ulisababisha uhaba wa chakula kwenye maeneo mengi ya nchi na kusababisha wananchi kwenye baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Mtwara kula ugali wa mihogo yenye sumu na kufanya baadhi yao kupata ulemavu:-

(a) Je, Serikali inalifahamu tatizo hilo?

(b) Je, ni hatua gani zilichukuliwa za kuokoa afya za wananchi hao walioathirika kutokana na kula mihogo hiyo yenye sumu?

(c) Je, ni wananchi wangapi na kutoka katika Wilaya ngapi waliathirika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Boma, lililoulizwa na Mheshimiwa Abdillah Namkulala, kwa niaba yake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu tatizo la wananchi kwenye baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Mtwara waliokula mihogo mchungu na kuathirika.

(b) Mheshimiwa Spika, hatua za haraka zilizochukuliwa na Serikali baada ya tatizo hili kujitokeza ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuwatambua waathirika katika Wilaya za Mtwara Vijijini na Newala ambako wananchi waliokula mihogo mchungu waliathirika.

(ii) Kuzipatia Kaya 192 zilizokuwa na waathirika msaada wa tani 23,874 za mahindi kwa ajili ya chakula.

(iii) Serikali kupitia Wizara ya Afya, ilifanya utafiti kuhusu ugonjwa wa kupooza uliowaathiri wananchi wa Mtwara Vijijini na Newala na kugundua kuwa ugonjwa huu ni wa kawaida na ulishawahi kutokea katika Wilaya ya Masasi mwaka 1988 na unajulikana huko kama Konzo. Kwa kuwa ugonjwa huu siyo ugonjwa wa ajabu kama ilivyodaiwa, Mkoa pamoja na Wizara ya Afya wamechukuwa hatua za kutosha kukabiliana nao.

(iv) Kutokana na hali ya upungufu wa mvua katika Mkoa wa Mtwara, katika msimu wa mwaka 2003/2004, Serikali ilipeleka jumla ya shilingi milioni 10 za ununuzi wa mbegu za Mtama kwa ajili Wilaya zote Mkoani Mtwara.

(c) Mheshimiwa Spika, jumla ya wananchi 228 katika Wilaya za Mtwara Vijijini na Newala waliathirika kwa kula muhogo mchungu wenye *cyanide* kwa muda mrefu waliathirika kwa muda mrefu kutokana na upungufu wa vyakula vingine ambavyo vilikuwa havipatikani kwa wakati huo katika Wilaya hizi.

**MHE. ABDILLAH O. NAMKULALA:**Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa waathirika hawa bado wapo hivi sasa; je, Serikali ina mpango gani wa kudumu wakuwasaidia kwa sababu hawana uwezo tena wakufanya shughuli yoyote viungo vya vimepooza?

(ii) Kwa kuwa Serikali haikuleta japo punje ya msaada wa chakula Mtwara Vijijini lakini wapinzani wamemshikilia bango kwamba *DC* amepokea na ameuzua, je, Serikali inatoa tamko gani kumkosha *DC* wangu anayefanya kazi nzuri? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Baada ya kutokea tatizo hili Serikali ilitoa msaada wa chakula kama nilivyosema kwa wale waathirika wachache waliokuwepo. Tatizo hili huwa linakuwepo kila mara, kilichotokea ni kwamba wananchi wakati ule kwa sababu ya tatizo la upungufu wa chakula walikula chakula chote cha akiba cha muhogo ule wa kawaida mpaka wakaenda kula muhogo mchungu kwa sababu walikuwa hawana chakula kingine mbadala.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kawaida wananchi wa eneo la Mtwara na Newala ndio chakula chao cha kudumu. Miaka yote ndio chakula chao cha kudumu kwa hiyo, mwaka huu baada ya kuwapelekea Mtama wamejitahidi kupanda mbegu ya Mtama na hali ya mazao ni nzuri.

Kwa hiyo, hatutarajii uathirika utokee mwaka huu kwa sababu hali ya chakula ni nzuri na uathirika wao hauwasababishii matatizo ya kutokushindwa kujitegemea.

(b) Serikali imeleta chakula cha aina mbili:-

(i) Wilaya ya Masasi ambayo walikuwa na matatizo ya ugonjwa huu lakini wanaita Konzo ambao wameuzoea tulipeleka tani 600 za chakula kwa ajili ya kuwasaidia kwa sababu wao pamoja na kuathirika lakini pia kulikuwa na hali ya ukame ambao ulikuwepo. Kwa hiyo, walihitaji chakula kingi zaidi lakini Wilaya hizi za Newala na Mtwara Vijijini.

Serikali ya Halmashauri ya Mtwara pamoja na Newala nao walipewa chakula siyo vyama vya upinzani, ni Serikali ndio iliyotoa chakula kwa ajili ya wananchi wale, lakini katika Kaya tu ambazo zilionekana zina matatizo zaidi. Kwa hiyo, Serikali ilitoa chakula lakini pia na mbegu za Mtama ambazo zilikuwa na thamani ya shilingi milioni 10.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa huu muhogo mchungu unaonekana kwamba unaathiri afya ya wanachi, je, Serikali imechukua hatua gani ya kuupiga marufuku usitumike kama chakula katika sehemu hizo ulipo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huu muhogo unaathiri kama haukuandaliwa inavyotakiwa. Wananchi wanajua jinsi ya kuuandaa ili hiyo sumu iondolewe. Kwa hiyo, hatutaupiga marufuku, tutaendelea tu kuwafundisha wananchi jinsi ya kuuandaa muhogo huu.

Na. 62

### **Daraja mbadala Morogoro Mjini**

**MHE. OSCAR T. MLOKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mto Morogoro umeigawa Manispaa ya Morogoro katika maeneo Makuu mawili; na kwa kuwa daraja lililopo *Shan Cinema* ambalo ndilo pekee linalounganisha Mji huu lilijengwa kabla ya Uhuru limechakaa kiasi cha kutohimili mizigo mizito:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga daraja mbadala kabla ya hilo lililopo halijavunjika kabisa?

(b) Kwa kuwa lipo daraja la miti kiasi cha mita 100 chini kidogo ya daraja hilo la *Shan Cinema* linalohudumia waenda kwa miguu pale ilipo *Community Centre* maarufu kwa jina la *DDC*; je, isingekuwa busara kwa Serikali kulijenga kwa kiwango cha kupitisha magari ili kupunguza msongamano ulioanza kujitokeza Mjini Morogoro?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Thobias Mloka, Mbunge wa Morogoro Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mto Morogoro unaugawa Mji wa Morogoro katika maeneo mawili muhimu. Maeneo hayo ni yale yenye huduma za Hospitali, Shule na Hoteli na huduma za mabasi, soko na Ofisi za Serikali kwa upande mmoja. Lakini upande mwingine ni huduma nyingine zinazoendelea. Pande hizi zinaunganishwa na Daraja lililoko *Shan Cinema* ambalo lilijengwa mwaka 1953. Madaraja mengine katika mto huu ni pamoja na Daraja lilipo kando ya mji wa Morogoro inapopita barabara ya *TANZAM*, Daraja la Nguzo ambalo lina uwezo wa kupitisha

magari tani 7 lakini yenye upana usiozidi mita mbili na Daraja la Kichangani ambalo ndilo linatumika kupitisha magari makubwa kuelekea kwenye Kituo cha Reli cha Morogoro.

Mheshimiwa Spika, Daraja la *Shan Cinema* lililojengwa miaka ya 1951 iliyopita lakini bado lina uwezo wa kupitisha magari yaliyo chini ya tani 15 ambao ni uzito au uwezo mkubwa kidogo. Hata hivyo Serikali inaona umuhimu wa kujenga daraja lingine ili kupunguza msongomano wa magari yanayopita kwenye daraja la *Shan Cinema*.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja mbadala katika eneo litakaloteuliwa, naishauri Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro pamoja na wakazi wake kulilinda daraja la *Shan Cinema* kwa kupitisha magari yasiyozidi uzito ulioruhusiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa daraja mbadala kupitia eneo la daraja la miguu (*foot bridge*) ili kuunganisha maeneo ya *DDC* na Shule ya Msingi ya Mwere, eneo hilo kwa bahati mbaya ni eneo ambalo halifai kujengwa daraja kwa kuwa halimo katika ramani ya mji au *Master Plan* ya mji wa Morogoro. Kwa hiyo, litajengwa mahali ambapo itaonekana inawiana vizuri na mpango wa Mji wa Morogoro.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa dalili za kukua kwa mji ni kuwepo na msongamano wa watu na magari; na kwa kuwa eneo hili la mji sasa lina msongamano mkubwa na ni tatizo sugu, je, Serikali haioni kuwa umefika wakati wa kufikiria miundombinu mbadala kukabiliana na tatizo kama hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oscar Mloka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua adha iliyopo katika Mkoa wa Morogoro hivi sasa na ndio maana juhudi unaona zinaendelea, kuna hatua moja imeshaanza, kubwa ni kuhamisha kituo kikubwa cha mabasi na kukijenga pale eneo la Msamvu badala ya lile eneo la zamani pale Mjini. Lakini kama nilivyosema inahitaji maamuzi ya msingi kutazama nini hasa tunaweza tukafanya si kwa mji wa Morogoro tu lakini hata miji mingine vile vile ambayo nayo inakabidhiwa na tatizo kama hilo. Kwa hiyo, tunalikubali na baadaye kazi tutayofanya ni kuwafanyia kazi kwa ujumla ili tuweze kuona ni miundo gani iweze kuimarishwa zaidi.

Na. 63

**Malipo Yanayotolewa kwa Mtu Aliyefariki akiwa Kazini**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa ndugu wenye ndugu zao waliofariki wakiwa kazini juu ya kiwango kidogo cha malipo ya fidia ya shilingi 83,000/= kwa mujibu sheria Na. 363 ya mwaka 1983; na kwa kuwa Serikali imejitoa katika shughuli za uzalishaji na kujihusisha na biashara na kwa kuwa, viwanda vingi vinafanya kazi kwa kujitegemea na kwa mikataba yao wenyewe:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta sheria hiyo haraka Bungeni ili iweze kufanyiwa marekebisho kulingana na hali halisi ya sasa?

(b) Je, malipo hayo yanalipwa na mwajiri pekee yake au Serikali inachangia na kama Serikali inachangia ni kwa asilimia ngapi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Tabora, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Kwa mujibu wa marekebisho ya sheria ya Fidia Na.17 ya mwaka 1983 (*Workmens' compensation Amendement (Act No. 17 of 1983)*), viwango vya awali vya fidia kwa mtumishi aliyekufa akiwa kazini ilikuwa ni shilingi 83,000/= au kiasi kisichozidi shilingi 180,000/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya mafupi sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Mchemba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kupitia Awamu ya Pili ya Mpango wa Maboresho ya Sheria za Kazi (*Phase II of Labour Law Reforms*) unaosimamiwa na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, imeanza kufanya maboresho kwenye Sheria ya Kazi. Mambo muhimu yanayoangaliwa katika mpango huu ni pamoja na kuangalia upya viwango vya fidia vilivyowekwa katika sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Wanaoumia wakiwa Kazini ili iendane na mazingira yaliyopo.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kuwa viwango vya fidia vimekuwa vikongezeka mwaka hadi mwaka kadri mazingira yanavyobadilika. Serikali kama mwajiri kupitia Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 na Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 imeweka kiwango cha fidia kati ya shilingi milioni moja na shilingi milioni kumi anachostahili kulipwa mtumishi wa umma anayekufa kutokana na madhara ya kazi. Utaratibu utakaotumika katika kufanya malipo haya ni kama ilivyoelezwa kwenye Kanuni Na. 110 hadi 112 za Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. Aidha, Serikali haihusiki na malipo ya fidia kwa watumishi wengine walio nje ya Utumishi wa Umma. Malipo ya fidia kwa watumishi hao hufanywa na waajiri husika.



Hata hivyo kama nilivyoeleza Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo ndiyo msimamizi wa utekelezaji wa Sheria ya Fidia, *Cap. 263* ya mwaka 1954 ikisomwa pamoja na marekebisho yake.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mara nyingi Serikali imekuwa ikiipa kitu kinachoitwa kifuta machozi; hivi kifuta machozi badala ya fidia halisi kinatokana na Sheria ipi katika Utumishi wa Serikali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Beatus Magayane, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuna wakati ambapo Serikali hulipa kifuta machozi kutokana na uwezo ambao upo na kutokana na tukio ambalo limetokea wakati ule. Lakini kwa madhumuni ya *Workmen's Compensation*, malipo yanatokea na sheria ambayo nimeitaja. Kwa hiyo, haya ya nafasi na tukio mahsusni ni *description* ya Serikali.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa katika Sheria ya Fidia ambayo Mheshimiwa Waziri ameitaja; na kwa kuwa mfanyakazi anapofariki anaacha mjane au na watoto ambao wanafuatilia kulipwa hiyo fidia na malipo hayo saa nyingine huwa yanachelewa kwa muda mrefu.

Je, Serikali haioni inavyochelewesha kuwalipa wajane au yatima hizo pesa isilipe na riba ili kuwapa fidia vizuri kwa watoto walioachwa? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Kwanza namshukuru kwa swali lake zuri. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inajitahidi katika kuongeza ufanisi wa utendaji wake ikiwa ni pamoja na kuharakisha malipo kwa wale wanaopata ajali kazini na kufariki. Sasa *issue* ya riba haiko kwenye sheria lakini pale ambapo Serikali itafanya kazi yake kwa uharaka na ikalipa kwa wakati unaotakiwa, basi hakutakuwa na haja ya riba.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwakumbusha waajiri wote kwamba ni haki ya wajane na watoto kupata fidia baada ya mfanyakazi kufariki kutokana na ajali kazini na kwa hivyo, haki yao ni pamoja na kuharakisha malipo yao.

Na. 64

**Tofauti ya Kipato Kati ya Watumishi wa Serikali ya Zamani na wa Sasa**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa watumishi waanzishaji wa Serikali ya nchi hii walio hai ni maskini na waliokufa wamekufa wakiwa maskini na kwa kuwa hivi sasa vijana wengi baada ya muda mfupi tu wa utumishi wao wanamiliki mali nyingi na kutajwa kuwa ni matajiri:-

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zinazosababisha watumishi waanzilishi waliotumikia nchi yao kutokuwa na mali?

(b) Je, ni sababu zipi za msingi zinazosababisha watumishi wa sasa kumiliki mali na kutajwa kuwa ni matajiri baada ya muda mtupi tu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sina hakika kwamba watumishi waanzilishi wa Serikali walio hai ni maskini na waliokufa wamekufa wakiwa maskini na wale wa sasa kuwa matajiri.

Mheshimiwa Spika, tangu tupate Uhuru hadi sasa sera za Serikali katika utawala wa kuendesha uchumi zimekuwa zikibadilika kukabiliana na changamoto za maendeleo ya wakati husika.

Mheshimiwa Spika, toka kipindi cha Uhuru hadi miaka ya themanini, mwelekeo wa kisera, kisheria na kimaadili haukuruhusu watumishi kuwa matajiri. Watumishi wamekuwa wanaishi maisha ya kawaida ya kila Mtanzania, isipokuwa kwa miaka ya hivi karibuni ambapo Serikali imechukua hatua za kuongeza viwango vya mapato na mishahara ya watumishi ukilinganisha na miaka iliyopita. Huenda ndiyo inaleta hisia kuwa watumishi wa sasa ni matajiri kuzidi watumishi wa miaka iliyopita.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea na utaratibu wa kuboresha mapato ya watumishi wake mara kwa mara kulingana na uwezo wake na hiyo inaonekana kama ni kujenga utajiri kwa watumishi wa hivi sasa ukilinganisha na wa miaka iliyopita.

Aidha, kuanzia miaka ya 1990 katika kuondoa umaskini kwa wananchi wote wakiwemo wale watumishi wa Serikali na katika kujenga uchumi madhubuti, sera za Serikali za uchumi zilibadilika kwa Serikali kujitoa katika uendesaji na umilikaji wa njia kuu za uchumi. Sera hii ilitoa fursa kwa wananchi na watumishi kwa ujumla kujishughulisha na uzalishaji mali na utoaji huduma na kupata mapato ya ziada vile vile watumishi wanaruhusuriwa kushiriki katika uwekezaji kwa njia ya kujinunulia hisa na hivyo kupata mapato kwa njia ya gawio.

Mheshimiwa Spika, ni katika mabadiliko hayo ambapo Serikali kupitia Waraka Na. 2 wa mwaka 1991 ilifanya siku ya Jumamosi kuwa siku ya mapumziko kwa kusudi la kuwawezesha watumishi kujishughulisha na uzalishaji mali na kujiongezea mapato.

Hivyo tofauti inayoonekana hapa ni ile itokanayo na sera zilizopo kuwawezesha na kuwashirikisha watumishi wa umma na wananchi kwa ujumla katika kuzalisha mali na kutoa huduma, hivyo kujiongeza mapato ili wajiondolee umaskini.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa inajitokeza baadhi nyakati, wafanyakazi kuwa na kazi aina moja. Lakini pia hujitokeza kati ya watu hao kuonyesha kwamba wanamiliki mali; huoni kwamba njia moja iliyosababisha hivyo ni kutokuwa waaminifu na kuonyesha ubadirifu ndani ya Serikali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa watumishi wanaofanya kazi ya aina moja wakawa na juhudi au bidii tofauti na kwa hiyo ikawa sababu ya wao kutokulingana katika mapato yao na mimi kwa kweli nawaomba watumishi wa Serikali wafanye kazi za Serikali kwa uaminifu kwa muda wa kazi na wakiweza waweze kuongeza juhudi ili wasiwe maskini na waweze kuheshimiwa. (*Makofi*)

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na mambo mengine, nadhani swali hapa ni *Retirement Benefits*, kwamba hivi karibuni mambo yameimarika zaidi wame-improve kwa upande huo wa maslahi na *Retirement Benefits* za watumishi kuliko wale walio-*retire* zamani. Kwa mfano, Katibu Mkuu wa zamani aliye-*retire* mwaka mmoja tu kabla ya mabadiliko haya anaendelea kupata shilingi 25,000/=. Sasa hao wengine labda wanapata laki moja na wanao-*retire* leo. Kwa hiyo, mahali pengine duniani wanavyoleta mabadiliko kama hayo, ugusa wote, je, Serikali si ingetazama hilo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jackson Makwetta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, watumishi walio kazini sasa hivi na wale waliostaafu Serikalini wote ni wananchi wa Tanzania, kwa hivyo Serikali ingependa wote wawe na maisha mazuri.

Lakini nyakati zinapita hata hivyo Serikali imekuwa ikijitahidi kila inapoweza kuwawezesha wale waliostaafu kuwa na hali nzuri kwa mfano wale waliochukua mapato yao mkupuo sasa wamerudishwa katika ule utaratibu wa kulipwa kila mwezi. Kwa hiyo, Serikali ina nia njema kwa wananchi wake wakiwemo watumishi wastaafu na watumishi walioko na itaendelea kufanya hivyo kwa kadri ya uwezo wake lakini tukumbuke kwamba Serikali ina majukumu mengine zaidi kulipa mishahara na mafao na ningeomba sana tija na ufanisi ndio njia pekee ya kuongeza mapato ndani ya uchumi wa nchi na kwa hivyo kuongeza mapato ya Serikali ya kuweza kulipa na mafao na maslahi mengine mazuri kwa watumishi waliopo na wale waliostaafu.

**Vidhibiti Mwendo**

**MHE. STEPHEN M. KAZI** aliuliza: -

Kwa kuwa, kumekuwa na nia kubwa ya kutaka kujua kama utaratibu wa kutumia vidhibiti mwendo katika magari Tanzania ni hatua sahihi ya kuzuia ajali barabarani zikiwemo pia na hatua nyingine; na kwa kuwa mojawapo ya sifa za magari ya kisasa ni mwendo wa kasi na mataifa yote ikiwemo Tanzania tunajenga barabara bora za lami kama kichocheo cha mwendo wa kazi na tuna magari yenye uwezo wa kwenda umbali wa kilometa 180 hadi 360 kwa saa kama inavyoonekana kwenye chombo cha kupimia mwendo.

(a) Je, kwenye hali hiyo, maagizo ya Serikali ya kufunga vidhibiti mwendo unaendana na mwelekeo wa dunia ya sasa?

(b) Ni mataifa yapi yanayotumia vidhibiti mwendo na wanavitumia kwenye magari yanayofanya shughuli zipi?

(c) Je, mpaka sasa Serikali imeshafanya utafiti ili kuona kama vidhibiti mwendo ndiyo njia bora ya kupunguza ajali ikilinganishwa na matatizao mengine kama madereva wasiokuwa na mafunzo, ukiukwaji wa sheria, hali ya magari na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa moja ya sifa za magari ya kisasa ni kuwa na mwendo wa kasi na mataifa mbalimbali ikiwemo Tanzania yanajenga barabara bora za lami. Hata hivyo barabara hizo hapa nchini haziboreshwi kwa ajili ya kuchochea mwendo kasi unaoweza kusababisha ajali kama inavyotokea hivi sasa. Miongoni mwa matatizo yanayochangia uongezekaji wa ajali za barabarani hapa Tanzania ni kwamba magari yanavyokwenda kasi yanapishana kwenye njia moja.

Katika nchi nyingi zenye ukomo ulio juu wa mwendo kasi, barabara zao ni pacha yaani *double carriage ways* ambapo magari yanavyokwenda upande tofauti hayakutani.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa barabara hapa nchini lengo lake hasa ni kupunguza ajali zinazoweza kusababishwa na ubovu wa barabara na sio kuchochea mwendo wa kasi. Serikali imeweka sheria ya kuwataka wamiliki wa magari ya abiria kufunga vidhibiti mwendo yaani *Speed Governors* ili kudhibiti mwendo wa kasi na hivyo kuepusha ajali zinazoweza kutokea kutokana na mwendo wa kasi. Kwa sababu hiyo vidhibiti mwendo katika magari ya abiria vinaendelea kuwa na umuhimu hasa kwa kadri tunavyoendela kuboresha barabara zetu nchini hadi hapo tutakapofika

hatua ya kuwa na barabara pacha. Hatua hii ya Serikali haipingani na mwelekeo wa dunia.

(b) Mheshimiwa Spika, zipo nchi mbalimbali zenye sheria ya vidhibiti mwendo katika magari ya abiria zikiwemo nchi za Afrika Kusini, Misri na Nigeria. Aidha, nchi nyingi za Ulaya zinayo sheria yenye kuweka ukomo wa kasi kwa magari ya abiria. Katika nchi hizo ukomo ni kasi ya kilometa 100 kwa saa. Sisi hapa nchini ukomo wetu ni kilometa 80 kwa sasa.

(c) Mheshimiwa Spika, mwendo wa kasi ni moja ya vyanzo vingi vya ajali hapa nchi na Serikali inapojitahidi kisheria kudhibiti mwendo wa kasi kwa kutaka mabasi ya abiria yafungwe *Speed Governors* inajua kuwa inadhibiti moja tu ya vyanzo vikubwa vya ajali. Ndiyo maana pamoja na kudhibiti mwendo kasi wa magari ya abiria, Serikali pia inatilia mkazo kuhusu kuimarisha elimu kwa madereva, elimu kwa watumiaji wengine wa barabara, kuimarisha ubora wa barabara, kusimamia ubora wa magari, kudhibiti ulevi wa madereva, kudhibiti ratiba za Mabasi na kadhalika.

Hivyo kwa kuwa vyanzo vya ajali ni vingi hakuna njia moja pekee inayoweza kupunguza ajali isipokuwa kwa kudhibiti njia zote zinazoweza kusababisha ajali ikiwa ni pamoja na kudhibiti mwendo wa kasi kwa magari ya abiria.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo bila shaka ametupatia ufafanuzi wa kutosha. Kwa kuwa hali hii ya ajali bado inaendelea na tunaiona wote na juhudi zinafanyika katika maeneo mbalimbali na Mwanza nawashukuru sana askari wa usalama barabarani kwa kusimamia na kukagua leseni za madereva hasa wale wanaoendesha gari za abiria kama mabasi, daladala na *taxi*.

(i) Sasa swali ni kwamba katika hizo hatua alizosema Mheshimiwa Waziri ni ipi hasa ambayo ni ya muhimu ambayo sisi sote tunapaswa tuifahamu ili tusaaidiane kusimamia?

(ii) Mheshimiwa Spika, ningependa tu kufahamu kwamba katika kipindi cha usalama barabarani huwa tunafanya mara moja kwa mwaka hapo ndio tunahamasisha jamii, tunawasaidia, tunawaeleza mambo mengi kuhusiana na usalama barabarani. Kwanini chini ya Wizara hii tusingimamie na tukafanya uhamasishaji wa aina hiyo mara tatu kwa mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza anauliza kwamba lipi hasa kubwa ambalo tufanye katika kupunguza ajali katika hatua zote ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Spika, hatua zote alizozitaja zote zina umuhimu wake zile za elimu kwa madereva, ina umuhimu wake mkubwa kabisa na ndio maana sasa hivi hatumpi

leseni dereva mpaka kwanza asome na afuzu, hatua za kuelimisha watumia njia wengine vile vile tunaendelea.

(a) Mheshimiwa Spika, hivi sasa tumeshaanzisha somo la usalama barabarani katika shule za msingi, tumeanza kwa majaribio katika mikoa mitatu Dar es Salaam, Pwani na Morogoro. Baadaye somo hili tutalisambaza kwa nchi nzima ili kizazi kipya hiki wakiwa bado watoto wadogo waelewe taratibu na sheria za barabarani ili wawe na uelewa mpana zaidi.

Vile vile ubora wa magari kwa sababu karibu asilimia 20 ya ajali inasababishwa na magari mabovu sasa hivi hatuna sheria ya kulazimisha kukagua magari (*Compersory Record Inspection*), sasa hivi ni hiari.

Mheshimiwa Spika, kupitia Wizara ya Ujenzi inaandaliwa sheria ambayo itafanya ukaguzi wa magari wa lazima na magari yale ambayo yatapata stika kwamba ni mazima ndio yataonekana barabarani, magari mabovu hayataonekana barabarani nafikiri wenzetu Wizara Ujenzi hii sheria wanaikamilisha itakuja ndani ya Bunge na ni hakika mtaititisha. Hatua zote hizi ni za muhimu lakini kubwa kabisa uzembe ni mwingi sana barabarani. Ningependa Watanzania wenzangu uzembe mwingi sana, kuna ukungu, dereva haoini anataka ku-*overtake*, kuna kona kali dereva anataka ku-*overtake*, taa mbovu dereva anatembea usiku kama ajali ya juzi kule Tabora lile lori taa zilikuwa mbovu, wakasema twende hivyo hivyo tu Mungu atasaidia, zikazimika wakaingia huko, kwa hiyo, toa wito kwa habari za uzembe.

(b) Kuhusu usalama barabarani tufanye mara tatu kwa mwaka, ni pendekezo zuri, tutalitazama lakini sasa hivi tumeunda Kamati za usalama barabarani za Wilaya na Mkoa ili shughuli hizi badala ya Kitaifa tunafanya sisi mara moja kwa mwaka wao kule Wilayani na Mikoani ziwe ni shughuli za siku kwa siku.

**MHE. KHALIFA SULEMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, asante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri katika maelezo yake amekubali kuwa msingi wa ajali nyingi katika nchi yetu na si nchi yetu na nchi nyingine ni mwendo mkali wa magari.

Kwa kuwa baadhi ya nchi sasa wanatumia njia mbili katika kupunguza hali hii kwanza ni kuweka *automatic cameras* ambazo zinanasa magari yanayokwenda mbio na njia ya pili ni ya kuwalipisha faini ya papo kwa papo ili kupunguza ujeuri wa madereva kuona mimi naweza kuepuka hii nikaenda mahakamani anaonaje wazo hili nalo wakaanza kulifikiria ili likaweza kusaidia kupunguza hali hii tuliyonayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ushauri anaotoa Mheshimiwa Mbunge ni ushauri mzuri tu, hili za faini ya papo kwa papo hata hapa Tanzania tunao lakini faini zetu ni ndogo sana ni shilingi 20,000/= . Kwa hiyo, madereva wanazilipa palepale anaendelea kufanya kosa lile na akikamatwa tena analipa tena 20,000/= anazo.

Kwa hiyo, kwa sababu tunaona faini hizi zinawapa motisha kuendelea kufanya makosa katika marekebisho ambayo yatakuja ya sheria ile ya *Traffic Act* liko pendekezo la kuongeza viwango vya adhabu ili dereva afikirie mara mbili kabla hajarudia lile kosa.

Kuhusu kuweka *cameras* barabarani ili kuwanasa wanaovunja sheria ni wazo zuri, tunalo hata Wizarani sasa hivi tunakusanya uwezo ili tukipata uwezo wa kifedha tuweze kuweka *cameras* kama wanavyofanya katika nchi nyingine.

Na. 66

### **Pasipoti Kwa Vijana Waliozamia Meli**

**MHE. ALI MACHANO MUSSA** aliuliza: -

Kwa kuwa, vijana wetu wa Kitanzania waliondoka nchini kwa kutumia njia isiyo nzuri ya kuzamia meli kutokana na hali mbaya kimaisha kwa wakati huo na kuwa baadhi yao hawakufa wako katika nchi mbalimbali za Bara la Ulaya; na kwa bahati nzuri huleta pato lao kwa wazazi na jamaa zao hapo nchini lakini wao wenyewe wanashindwa kufika kutokana na ukosefu wa pasipoti za Tanzania: -

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Watanzania hao kupata pasipoti ili waweze kurudi kihalali?

(b) Kwa kuwa kutenda kosa siyo kosa ila kurejea kosa ndio kosa, je, Serikali haioni kuna haja ya kuwasamehe vijana hao makosa yao yaliyopita?

(c) Je, Serikali inajua kuwa wapo baadhi ya Watanzania wenye asili ya mabara mengine ambao wana pasipoti zaidi ya moja?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Machano Mussa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa Sheria ya Uhamiaji Na. 7 ya mwaka 1995 kifungu cha 33(f) ni kosa la jinai kwa Mtanzania yeyote kuondoka nchini bila kufuata sheria ikiwa ni pamoja na kuzamia meli. Hivyo wale wote wanaofanya hivyo wanastahili kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Aidha, Balozi zetu za Nchi za Nje na Ofisi za Wawakilishi wetu wa nchi ambazo hatuna ofisi za Ubalozi hutoa pasipoti kwa Watanzania walio nje ili mradi wawe na uthibitisho wa uraia wao wa Tanzania. Hivyo Watanzania walioko nchi za nje bila pasipoti wanaweza kufika kwenye Ofisi za Balozi zetu au ofisi za wawakilishi ili wapate hati za kusafiria baada ya kuthibitisha uraia wao kwa mujibu wa sheria na hivyo waweze kurudi nchini kihalali.

(b) Mheshimiwa Spika, nchi yetu huongozwa kwa misingi ya sheria, kanuni na taratibu ambazo kila raia anapaswa kuzifuata. Usemi kwamba kutenda kosa sio kosa ila kurejea kosa ndilo kosa ni usemi wa hekima ya kimaisha tu, lakini sio wa kisheria. Kwa mujibu wa sheria, adhabu hutolewa mara moja baada ya kosa kuthibitishwa bila kusubiri lifanyike kosa la pili au la tatu. Hivyo wale wote waliozamia na wanaotazamia kuzamia hata kama kosa limefanyika kwa mara ya kwanza, wahusika wakibainika wanastahili kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria ya pasipoti na hati za kusafiria Na. 20 ya mwaka 2002 kifungu cha 19 (i), mtu yeyote haruhusiwi kumiliki pasipoti ya aina moja, zaidi ya moja pasipo kibali maalum. Vile vile sheria ya uraia Na. 6 ya mwaka 1995 kifungu cha 7 (1) hairuhusiwi mtu mwenye umri zaidi ya miaka 18 kuwa na uraia wa Tanzania na uraia wa nchi nyingine yaani *dual Nationality* na yeyote atakayefanya hivyo atakuwa amepoteza sifa ya kuwa raia wa Tanzania. Mtu wa aina hiyo akibainika atanyang'anywa uraia wa Tanzania.

Aidha, kwa sasa Serikali haina ushahidi wa kuthibitisha taarifa za kuwepo kwa baadhi ya Watanzania wenye asili ya Mabara mengine ambao wana pasipoti zaidi ya moja. Namwomba Mheshimiwa Mbunge au mwananchi yeyote mwenye ushahidi wa mtu mwenye pasipoti zaidi ya moja yaani ile ya Tanzania na ya nchi zingine, atupatie taarifa na Serikali itamshughulikia kwa mujibu wa sheria za nchi yetu.

**MHE. ALI MACHANO MUSSA:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri yenye kuelewewa, naomba niulize swali moja. Kwa kuwa hutokea usumbufu mkubwa kuipata pasipoti, je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na hatua hiyo ya kubadilisha utaratibu huu ambao unaletea usumbufu kwa Watanzania ambao husumbuka wakati wa kupata pasipoti ili kwenda nchi za nje na haswa wale wazawa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida haipaswi Mtanzania kusumbuka, Mtanzania hupata pasipoti katika hali ya kawaida. Jinsi utaratibu ulivyo kwamba Mtanzania pale alipo anapohitaji pasipoti, anajaza fomu kubwa kwa kila Mkoa wake, anakamilisha kila kitu, analipia malipo shilingi 20,000/= tu, wakishakamilisha zile fomu zinaletwa makao makuu pasipoti inaandikwa, inapelekwa katika Mkoa wake anaipata.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo ukifuatwa hakuna usumbufu isipokuwa baadhi ya raia wetu hawapendi kuulizwa maswali, sasa hakuna Serikali itakupa pasipoti bila kukuuliza maswali, akiambiwa sasa athibitishwe kama yeye ni raia athibitishwe uraia wake na nchi yote inavyompa raia wake lazima ihakikishe kwamba ni raia sasa anaona ni usumbufu akihojiwa kwamba pasipoti sasa unakwenda nchi gani kufanya nini na nini kwa sababu wengine wanataka pasipoti iwe kama *furniture* aiweke ndani ya nyumba tu. Akihojiwa kidogo hivyo anaona ni usumbufu.

Lakini mwisho Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wote kama kweli kuna mtu ambaye anasumbuliwa kupata pasipoti tulateeni taarifa ili tuweze kukwamua,



hatutaki Watanzania wenye safari za dhati kabisa, wenye sababu za dhati kabisa wasumbuke kupata pasipoti kwa sababu ni haki yao wanapoitafuta. (*Makofi*)

Na. 67

### **Serikali Kulipia Madeni ya Vyama vya Ushirika**

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA** aliuliza: -

Kwa kuwa kuanzia mwaka 1999/2000 hadi mwaka 2001/2002 Serikali ilivilipia madeni Vyama Vya Ushirika vya *KCU, KDCU, NCU, KNCU SHIRECU* na *BCU* kiasi cha shilingi bilioni 9,940 zilizodaiwa na wakulima na Benki mbalimbali kwa nia ya kuvinusuru kufilisiwa na viendeleo kukopesheka na kwa kuwa, Chama Kikuu cha Ushirika *MBICU* kilifilisiwa kwa kushindwa kulipa deni lililokuwa chini ya shilingi bilioni 3, hivyo mali zake zote zilizohamishika kama Hoteli, Maghala, Mashamba na kadhalika kwa kukosa wanunuzi.

Je, Serikali haiwezi ikalipia deni la *MBICU* ili mali zote ambazo mfilisi ameshindwa kuuza zikamilikiwa tena na wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa nyakati mbalimbali kuanzia mwaka 1999/2000 hadi 2001/2002, Serikali ilivilipia madeni Vyama vya Ushirika vya *KCU, KDCU, NCU, SHIRECU* na *BCU* kwa nia ya kuviwezesha kukopesha na kuendelea kutimiza majukumu yake kwa wanachama kama ambavyo ilielezwa katika hotuba ya Bajeti ya Wizara yetu ya mwaka 2004/2005. Hatua hii ilitokana na mapendekezo ya Kamati ya kumshauri Mheshimiwa Rais juu ya kufufua, kimarisha na kuendeleza Ushirika nchini ambayo ilibaini kwamba mojawapo ya matatizo sugu ya vyama vya ushirika ambayo yanahitaji kushughulikiwa haraka ilikuwa ni ukosefu wa mitaji.

Mheshimiwa Spika, wanachama wa ilivyokuwa *MBICU* walikuwa wamekatishwa tamaa na uongozi mbovu wa chama chao na kuamua kutotumia huduma za chama hicho, hatua iliyokikoshesha shughuli za kufanya na hatimaye kushindwa kuwajibika kwa wateja na wadau wake. Hali hii inaifanya *MBICU* kuwa na sababu tofauti za zile zilizopelekea vyama alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge kupata udhamini wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Serikali ilifanya uamuzi wa kukifilisi chama cha *MBICU* ili kulinda pia maslahi ya *third parties* kwani ni wajibu wa Serikali kufanya hivyo ili wananchi wawe na imani na sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mpango kabambe wa mageuzi ya Ushirika nchini, Serikali inachambua uhalali wa madeni mbalimbali ya Vyama vya Ushirika yakiwemo madeni ya *MBICU* na itashauriana na wanachama wa *MBICU* kuhusu namna ambavyo watashiriki katika kubeba mzigo wa madeni halali yatakayoinishwa na Serikali kama ambavyo ilifanyika kwa Vyama vya *KCU, KDCU, NCU, SHIRECU* na *BCU*. Baada ya utaratibu huu kukamilika ndipo itakapofahamika kama mali za *MBICU* zinazosimamiwa na mfilisi zinaweza kumilikishwa tena kwa wakulima.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mali za *MBICU* zilifilisiwa na bado mali zisizohamashika zipo, je, wakulima wa Mbinga wachukue hatua gani ili Serikali ikawafikiria mali hizo ziweze kuhamishwa na kumilikishwa na wakulima? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nimeeleza hapa kwamba tunaendelea na uchambuzi wa madeni ya Vyama vya Ushirika nchini ikiwepo na hiyo ya *MBICU* na baada ya uchambuzi huo itakapobainika kwamba baadhi ya madeni yatatakiwa yabebwe na wakulima na mengine yaweza yakachukuliwa hatua na Serikali ndipo hapo sasa itaamuliwa hizo mali ambazo sasa hivi zinashughulikiwa na mfilisi zinaweza kama zikamilikiwa na wakulima au zikafanyiwa vinginevyo.

Kwa hiyo, kwa hivi sasa wakulima waendeleo kusubiri wakati tunaendelea na zoezi ili ambalo Serikali inafanya kwa nia ya kuwasaidia.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Vyama vya Ushirika kwa nia njema walichagua viongozi wa kuongoza vyama hivi na hatimaye viongozi hawa kwa tamaa zao wakafilisi vyama hivi ikiwa ni pamoja na akiba na mikopo, je, Serikali haioni ni vyema kuwafilisi hawa waliofilisi ili wafidie hasara waliyoweka kwenye chama? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba katika baadhi ya vyama ambavyo viliingia kwenye ufilisi kusema kweli ilitokana na ubovu wa uongozi katika vyama vile na Serikali ilikuwa ikijitahidi sana kuhakikisha kwamba uongozi ule unasimamia vyama hivyo kikamilifu inavyotakiwa. Lakini kutokana na udhaifu wa uongozi huo vyama hivyo vilifilisika pamoja na hivyo ambavyo amevitaja Mheshimiwa Mbunge. Serikali inachofanya sasa hivi ni kuchambu hayo madeni ambayo sasa hivi yapo ili itakapobainika, yale mengine yaliyohusiana na uzembe pamoja na udhaifu wa uongozi hao watafilisi kama nilivyokuwa nimesema katika jibu la msingi.

Na. 68

**Utaratibu wa Kutangaza Bei ya Pamba Mei Mosi**

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE** aliuliza:-

Kwa kuwa miaka ya nyuma wakulima wa zao la pamba walikuwa wakitangaziwa bei katika sikukuu ya wafanyakazi yaani Mei Mosi kila mwaka; na kwa kuwa utaratibu huo hautolewi tena.

(a) Je, Serikali haioni kuwa mkulima bila ya kutangaziwa bei ya zao lake anashindwa na kukata tamaa kulima pamba?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kushindwa kutoa tangazo la bei kwa mkulima kabla ya msimu kuanza ni kumnyima haki yake halali?

(c) Je, Serikali haioni kuwa bei ya zao ndio msingi wa kwanza kwa mkulima wa zao la biashara ili apate moyo na ari ya kulima?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mbunge wa Meatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutangaza bei ya mazao ya mkulima mapema aliouelezea Mheshimiwa Mbunge ulikuwa ukitumika kabla ya kuanziswa kwa mfumo wa soko huru ambapo Serikali ilikuwa ikipanga na kutangaza bei ya mkulima kwa mazao hayo kabla ya kufunguliwa kwa msimu. Utaratibu huo ulitumika kwa sababu Serikali ilijihusisha moja kwa moja na ununuzi wa mazao hayo kupitia Bodi za mazao na Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa soko huru, Serikali ilijitoa katika ununuzi wa mazao na kuiachia sekta binafsi ambayo inahusisha makampuni binafsi na Vyama vya Ushirika. Jukumu la Serikali lilibakia katika kutunga na kusimamia sera, sheria na kanuni za ununuzi na uuzaji wa mazao. Chini ya mfumo huu, Serikali imeacha pia kupanga bei ya kununulia mazao. Bei ya kununulia baadhi ya mazao makuu kama vile pamba, korosho na tumbaku hivi sasa hupangwa na wadau wenyewe kwa kuzingatia vigezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na bei ya zao hilo katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa zao la pamba, wadau wake ambao hujumuisha Bodi la Pamba, wawakilishi wa Vyama vya Ushirika, wafanyabiashara, kupitia chama chao cha *Tanzania Cotton Association* na Serikali hukutana kabla ya kuanza kwa msimu na kukubaliana bei dira itakayotumika katika msimu huo. Hata hivyo Serikali hairidhiki na utaratibu huu wa kukubaliana bei dira hususan chini ya mfumo wa utandawazi na hali ya kubadilika badilika kwa bei kwa sababu unaweza kuleta madhara kama yale yaliyojitokeza kwa zao la pamba katika msimu wa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tabia ya kupanda na kushuka kwa bei ya mazao katika soko la dunia, upatikanaji wa taarifa za mabadiliko ya bei kwa wakulima ni muhimu kama alivyosisitiza Mheshimiwa Mbunge. Ili kuboresha upatikanaji na

usambazaji wa taarifa hizo, Serikali inaimarisha Idara ya Masoko katika Wizara ya Ushirika na Masoko ili iwe na uwezo wa kuchambua mwenendo wa bei za mazao mbalimbali katika masoko ya ndani ya nje, kwa lengo la kutoa taarifa sahihi kuhusiana na dira ya bei ya mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inahamasisha na kuweka mazingira mazuri ya kuimarisha soko la ndani la mazao na kwa upande wa zao la pamba Serikali inahamasisha na kuhimiza uwekezaji katika viwanda vya nyuzi na nguo vitakavyoweza kutumia pamba nyingi inayozalishwa hapa nchini ili kuwawezesha wakulima wa pamba kupata soko la uhakika.

Sambamba na hatua hii Serikali pia imeainisha mbinu mbalimbali ambazo wakulima wanaweza kutumia mikakati kukabiliana na tatizo la bei. Mbinu hizo ni pamoja na kuuza kwa mkataba (*Forward Selling*), kuanzisha kilimo cha mkataba (*Contract Farming*); kutumia stakabadhi za mazao ghalani (*Warehouse Receipt System*) na pia kuanzisha bima ya anguko la bei za mazao.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko, napenda niulize swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa msimamizi mkuu wa uzalishaji wa zao la pamba ni Bodi ya Pamba chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula na hapo hapo anayetafuta masoko ya mazao ni Wizara ya Ushirika na Masoko ambayo ni Wizara tofauti inayosimamia uzalishaji, je, kwa utaratibu huo Serikali haioni kuwa hili ni kosa kubwa sana kiundeshaji kwa sababu ni Wizara mbili tofauti? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, bodi ya pamba ni chombo cha Serikali ambacho kiutendaji inasimamiwa na Wizara ya Kilimo na Chakula lakini kishughuli inasimamiwa na Wizara zote mbili kwa maana ya kwamba eneo la masoko tunashirikiana pamoja na wenzetu wa Wizara ya Kilimo na Chakula, kuhakikisha kwamba shughuli za Serikali zinakwenda sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, isitoshe Serikali ni moja kwa hiyo, suala la kusema kwamba kusimamiwa na Bodi ya Pamba na Wizara ya Kilimo na Chakula na huku shughuli zingine za masoko zinadhitiwa na Wizara ya Ushirika na Masoko, kusema kweli halileti mantiki ya kuridhisha kwa sababu Serikali ni moja na kwa sisi kwa Wizara hizi mbili tunafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu sana na kwa hiyo, hakuna lolote linaloweza kuathiri utendaji.

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, swali langu ni kwamba kwa kuwa msimu uliopita wa pamba wakulima waliweza kupewa bei ambazo zilikuwa zinasikitisha na baadaye Serikali ikatoa tamko hapa kwamba bei ya pamba iongezwe, lakini wakulima wote waliouza pamba hawakuongezewa bei hiyo. (Makofi)

Je, nini tamko la Serikali juu ya kauli ya Serikali iliyotolewa na Waziri Mkuu hapa Bungeni?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika utaratibu ule wa kutangaza bei dira ulitokea mkanganyiko baada ya mabadiliko ya bei ya pamba katika soko la dunia na kwa hiyo, bei iliyokuwa imetangazwa shilingi 300/= ikateremka kufikia shilingi 250/= kwa kilo na baada ya hapo kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kweli Serikali ilitoa tamko ya kwamba yatafanyika marekebisho kufikia shilingi 275/= kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, zoezi hilo limeendelea kutekelezwa na utekelezaji wake ilikuwa ni kwamba tuwasiliane sasa na wale wakulima wote ambao walikuwa wamepata yale mapunjo ili waweze wakalipwa ile tofauti. Hivi sasa tunavyozungumza baadhi ya Wilaya zimeshawasilisha orodha ya wakulima ambao wanadai ili iweze ikaunganishwa na wengine ili waweze kulipwa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ambazo zimekwisha kuwasilisha sasa hivi ni Bukombe, Misungwi, Kwimba, Maswa na Bunda, hizo zimekwisha wasilisha. Kwa hiyo, bodi ya pamba inaendelea kuwasiliana na Wilaya zingine ili ziweze zikawasilisha hizo orodha ili zoezi la kuwalipa liweze likafanyika.

Na. 69

### **Mawasiliano ya Simu za *Celtel***

**MHE. CHARLES H. KAGONJI** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi walio wengi katika Jimbo la Mlalo ni wafanyabiashara wa biashara mbalimbali na kwamba watu ni wengi zaidi katika nyanja ya biashara kuliko kwenye eneo la kilimo:-

(a) Je, kwa nini simu za *Celtel* bado hazijafika Jimboni Mlalo licha ya maombi ya muda mrefu?

(b) Je, Serikali inafahamu kwamba simu za mkononi ni rahisi kubeba na kuweza kutumika wakati wote hasa kwa wafanyabiashara kama wale wa Mlalo hivyo ifanye jitihada za makusudi kupeleka huduma hiyo Mlalo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Mlalo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *Celtel* imeshafanya uchunguzi wa awali wa soko (*Field Marketing Survey*) katika Jimbo la Mlalo na mji wa Lukozi mwezi Januari, 2004.

Aidha, tathmini hiyo ilifanywa tena mwezi Machi, 2004 na ilibaini kuwa mji huo una mazao ya mboga na matunda mbalimbali, mbao, kahawa na kadhalika. Hivyo basi, ni dhahiri kuwa wakazi wa eneo hilo hufanya biashara na miji ya Dar es Salaam, Tanga na Moshi na hivyo huhitaji mawasiliano ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, taarifa tulizozipata kutoka kampuni ya *Celtel* ni kwamba kampuni hiyo inatengemea kufikisha mawasiliano yake katika Jimbo la Mlalo na mji wa jirani wa Lukozi kabla ya tarehe Januari, 2005.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kuwa simu za mkononi ni rahisi kubeba na kuweza kutumika wakati wote siyo tu kwa wafanyabiashara bali kwa wananchi wote kwa ujumla.

Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeyahimiza makampuni ya simu kusambaza simu za mkononi. Kumbukumbu zetu zinaonyesha kwamba katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2000 huduma hii imesambaa nchini kama ifuatavyo: -

(i) Kampuni ya *Mobitel* hivi sasa ina wateja 260,000.

(ii) Kampuni ya *Vodacom* imeshasambaza simu 850,000.

(iii) Kampuni ya *Zantel* imesambaza wateja 80,000.

(iv) Kampuni ya *Celtel* imeshasambaza simu 380,000.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, tunamshukuru kwamba Kampuni hiyo sasa inakamilisha minara ya simu za mkononi mpaka pale Mlalo. Lakini kwa sababu maeneo ya Kaskazini mwa Jimbo hilo yana vigezo vingi na mahsus ambavyo vingefaa sana kwa kuongeza faida kwa Kampuni hiyo hasa kwa kutambua kwamba maeneo haya yana viwanda vya mbao zaidi ya 15, yana mashine za kusaga na kukoboa nafaka zaidi ya 30, shule za sekondari na taasisi mbalimbali.

Je, Wizara hii sasa kwa kuwa simu ziko karibu kuingia Mlalo, je, Wizara iko tayari kuishawishi Kampuni ya *Celtel* isogeze huduma zake katika kata za Shume, Rangwi, Sunga, Mtae, Mbaramu na pale Mlalo ambapo vigezo hivyo wanavyovisema pamoja na vijana wachapakazi wa biashara vipo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nafikiri Mheshimiwa Charles Kagonji, atakubaliana nami kwamba tumepata nafasi ya kutembea naye katika jimbo lake lote na tumeweza kurekebisha sehemu mbalimbali ambazo kulikuwa na kasoro na hitilafu za mawasiliano ya simu katika jimbo lake; na kama nilivyomhakikishia hapa mapema kwamba tunategemea kabla ya mwakani huduma za *Celtel* zitafika pale. Basi tuombe *Celtel* zifike sehemu ile na vijiji alivyovitaja kama hali ya tambarare na Jiografia itakubali na Teknolojia iliyopo nina hakika mawasiliano ya simu ya *Celtel* yatafika katika maeneo ya vijiji alivyovisema Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo tu moja la nyongeza.

Kwa kuwa shughuli hizo za kibiashara zinazofanywa na wananchi wa jimbo hilo la Mlalo zinafanana sana na shughuli za kibiashara zinazofanywa na wananchi wa eneo la Madaba kule Songea vijijini, eneo la Kigonsera kule Mbinga na eneo la Bukene kule Tabora, je, Mheshimiwa Waziri anawaambia nini wafanyabiashara wa maeneo hayo niliyoyataja na sehemu nyingine za Tanzania katika kuwasogezea huduma hiyo ya simu za mkono ili waweze kuboresha huduma zao za kibiashara? (*Kicheko/Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana nae kwamba shughuli zinazofanyika kule Mlalo zinafanyika vile vile katika mji wa Songea na vijiji ambavyo amevitaja Mheshimiwa Mbunge na nilipata bahati ya kutembelea maeneo hayo.

Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge nia ya Serikali ni kuona kwamba huduma za simu zinawafikia walengwa vijijini kule waliko. Tutaendelea kuwahamasisha ndugu zetu watoa huduma za simu za mikononi na simu za kawaida kuona kwamba wanasambaza huduma zao ipasavyo na zinawafikia watefa wote ili wafanyabiashara ziwe ndogondogo ziwe kubwa, wafaidike na matunda haya ya Teknolojia ya kisasa.

Na. 70

### **TRENI IENDAYO SINGIDA**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa mara nyingi treni ya kwenda Singida husubiri sana pale Manyoni mahali ambapo wasafiri hawawezi kupata huduma za kutosha ya chakula kwa kuwa hakuna hoteli nyingi za kutosha. Je, Serikali haioni ni vyema ikawa inasubiri Saranda ambako chakula safi na cha kutosha kinapatikana?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa ni vigumu kwa Shirika la Reli Tanzania kusimamisha treni kituo cha Saranda kwa treni inayokwenda Singida badala ya kituo cha Manyoni kwa sababu zifuatazo:-

(a) Manyoni pana yadi kubwa zaidi ya Saranda kwa hiyo, kiutendaji gari likisubiri Manyoni magari mengine yanaweza kupishana bila usumbufu.

(b) Kwa usalama na kuepusha ajali ambazo zilikwisha wahi kutokea ni salama zaidi kuweka gari la abiria Manyoni.

(c) Saranda ndiyo stesheni yenye maji na magari yote huwekwa maji hapo na endapo Shirika litaweka gari katika kituo hicho patakuwa na msongamano mkubwa na hivyo kushindwa kutoa huduma hiyo vizuri.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kwa kuwa Manyoni ni Makao Makuu ya Wilaya, chakula na vinywaji vile vile vinapatikana hapo bila matatizo, napenda niendeleo kuwahamasisha mamalishe wa Manyoni wasipoteze nafasi hii muhimu ya kijiendeleza kibiashara.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Nimeridhika na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi.

(i) Lakini je, Serikali itakuwa tayari kupanga ratiba yake vizuri ili treni zikutane Manyoni kwa wakati ili wananchi wasikae sana?

(ii) Nakubaliana nae kwamba Manyoni ni Makao Makuu ambayo kuna hoteli nyingi, lakini hizo hoteli ziko mbali na stesheni je, Waziri atakubaliana nami kwamba wahamasishe watu, wafungue kantini pale stesheni ili wananchi wasiwe wanapata taabu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kwamba tunakubaliana nae kama kuna ratiba zinachelewa basi tutahakikisha kwamba ratiba zile zinafata wakati na wananchi wasichelewe tena wanaosafiri.

Pili nadhani labda nimwombe Mbunge wa Manyoni anisaidie katika hili kwamba kuhamasisha akina mama ntilie ili waweze kutoa huduma karibu, wahamasishe mamalishe ili watumie nafasi hii vizuri ya kutoa huduma na wao kujipatia kipato. Naamini tutashirikiana katika hili.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa treni hupoteza muda mwingi pale Manyoni kama ilivyoulizwa katika swali la msingi; na kwa sababu hiyo hulazimika kusimama dakika moja moja tu katika vituo vingine wakati inaenda Singida na kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi hasa akina mama wenye watoto wadogo na wakati mwingine watoto hao wadogo wanaachwa chini, mama anapanda.



Je, Serikali haioni kama ni busara kulitaka Shirika la Reli kubadilisha utaratibu wa kusimama dakika moja na isimame walaua dakika tatu katika vituo vidogo kuondoa usumbufu kwa akina mama?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, inawezekana kuna kuchelewesha kidogo shughuli mbalimbali pale, lakini nafikiri akumbuke Mheshimiwa Mohamed Missanga, kuwa pale Manyoni ni stesheni kubwa ambayo tunaunganisha mabehewa na kukata mabehewa, shughuli hii huwa inachukua muda kidogo, lakini napenda nimhakikishie kwamba nitawasisitiza wafanyakazi wa huduma za *TRC* wahakikishe kwamba wanafanya shughuli zao kwa wakati na kuwapa nafasi abiria waweze kupata huduma ya usafiri inavyofaa.

Na. 71

### **Sheria za Mirathi**

**MHE. KHADIJA SALEH NGOZI** aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya wananchi wanaoishi vijijini hawazifahamu sheria za nchi ikiwa ni pamoja na sheria za mirathi na hivyo kusababisha migongano ya mara kwa mara; na kwa kuwa baadhi ya mahakama hupata mwanya wa kutowatendea haki wananchi hususan wanawake:-

(a) Je, msimamizi wa mirathi huteuliwa na nani?

(b) Je, haki zake ni zipi kama msimamizi mkuu wa mirathi?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Msimamizi wa mirathi huteuliwa na Mahakama husika ambako mirathi ya marehemu imefunguliwa. Uteuzi huo hufanywa baada ya wana ukoo wa marehemu kumpendekeza mtu miongoni mwao au hata kutoka nje kuwa msimamizi wa mirathi.

(b) Haki au majukumu ya msimamizi wa mirathi huwa ni mengi na miongoni mwake ni kutambua na kukusanya mali zote zilizoachwa na marehemu, kuzifanyia tathmini mali hizo ili ziweze kugaiwa kwa warithi husika, kulipa madeni ambayo marehemu alikuwa akidaiwa na kudai madeni yote ambayo marehemu alikuwa akidai. Hatimaye ni jukumu la msimamizi wa mirathi kugawa mali za marehemu kwa warithi wake kwa mujibu wa sheria ambayo warithi wameamua itumike au iliyoamuliwa na Mahakama itumike katika kugawa mali alizoacha marehemu.

**MHE. KHADIJA SALEH NGOZI:** Kwa kuwa wasimamizi wa mirathi mara nyingi hawagawi mali ya mirathi kwa wahusika kama inavyostahili, je, Serikali haioni iko haja ya kuweka viwango maalum kwa kuwagaiya warithi wahusika?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, jibu hilo halina ukakasi na ningependa kumjibu Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama haina pesa wala Serikali haina pesa, pesa ambazo huwa zinasimamiwa na Mahakama ni pesa ambazo zinatokana na mali za marehemu. Kwa hiyo, kuweka kiwango mahususi kwamba hicho ndio walipwe wale ambao ni warithi haitawezekana kwa sababu pesa hizo zinatokana na yule ambaye amefariki na Serikali au Mahakama haina kiwango cha pesa cha kuweza kuwalipa wahusika.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Sambamba na swali la msingi kwa Wilaya Nkasi ambayo haina hakimu hata mmoja wa Mahakama ya Wilaya wala Hakimu wa Mahakama ya mwanzo.

Je, Serikali iko tayari kutuletea Hakimu haraka iwezekanavyo ili pamoja na kufanya shughuli zingine ambazo ni za kusimamia masuala ya mirathi pia aweze kusimamia masuala mazima ya Utawala Bora katika Wilaya hiyo?

**SPIKA:** Ni swali jipya, lakini unaweza kulijibu.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, swali lake limefika, pamoja na kushughulikia masuala ya mirathi lakini la msingi ambalo anataka kuniambia hapa ni kwamba hawana Mahakama, Mahakimu wa kutosha na ningependa nimuahidi kwamba suala hilo tutalishughulikia kuhakikisha kwamba Mahakimu hao wanapatikana.

Na. 72

### **Majosho Wilayani Kyela**

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE** aliuliza:-

Kwa kuwa, ili ufugaji wa ng'ombe na wanyama wengine ufanikiwe na kumnufaisha mfugaji, maji na majosho ni vitu muhimu na nyeti.

(a) Je, Serikali ina majosho mangapi yanayofanya kazi katika Wilaya ya Kyela?

(b) Je, endapo Halmashauri ya Wilaya imeshindwa kuendesha majosho kutokana na uwezo mdogo wa mapato, msimamo wa Serikali hii ni ipi?

(c) Je, Serikali inakubaliana nami kwamba kushindwa kwake kujenga na kuendesha majosho Wilayani Kyela ni kuwaongezea umaskini wananchi kinyume kabisa na jitihada za Serikali na makakati wake wa kupunguza umaskini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI k.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshiwa John Mwakipesile, naomba nifanye ufafanuzi kidogo wa swali namba 61 ambalo aliuliza Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, la nyongeza.

Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, aliuliza swali la nyongeza kwamba wapinzani wanamtuhumu DC wa Mtwara kwamba ameuza chakula cha njaa. Sikulijibu, nimefanya utafiti wa kina sasa hivi nimetoka nje nataka kujibu sasa kwa uhakika kwamba tani 23 zilitolewa na CARTAS na Serikali zikatolewa kwa wananchi wa Mtwara na ziligaiwa na Kamati ya Maafa.

Mheshimiwa DC, Sadick hakuhusika kwa namna yoyote na wala hakuuza chakula. Nataka Mheshimiwa Abdillahi Namkulala na wananchi wa Mtwara waridhike kwamba maneno wanayosikia ni uzushi na hayahusiani na DC wa Mtwara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Mwakipesile, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Wilaya ya Kyela inayo jumla ya majosho 12 ambayo yote hayafanyi kazi. Majosho yapo katika vijiji vya Pimbi, Makwale, Kapwili, Isaki, Ipinda, Lugombo, Mababu, Ngana, Tenende, Kasala, Mangala na Sinyanga. Josho la Makwale lilikarabatiwa mwaka wa fedha 2003/2004. Majosho Isaki na Sinyanga yalikarabatiwa mwaka huu wa fedha 2004/2005. Hivyo majosho haya matatu yataanza kufanya kazi baada ya ukarabati huo.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela haijashindwa kuendesha majosho yake. Halmashauri ya Wilaya hiyo kwa kushirikiana na Serikali imetengewa shilingi 15,152,239/= kwa ajili ya kukarabati majosho ya Isaki na Sinyanga. Msimamo wa Serikali kwa sasa ni kutekeleza sera ya ubinafsishaji wa baadhi ya huduma za jamii ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa majosho.

Kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2004 majosho ya Makwale, Kapwili, Sinyanga, Pimbi na Ipinda yameendeshwa na vikundi vya wananchi, Chama cha Ushirika cha Kyela (*KYERUCU*) na watu binafsi, lakini mafanikio hayakuwa mazuri kutokana na ama uongozi mbaya wa vikundi na kuvunjika kwa Chama Cha Ushirika ama uchakavu wa majosho yenyewe.

Naomba kuzishauri Halmashauri za Wilaya ya Kyela na Halmashauri nyingine nchini kutoa kipaumbele kwa ujenzi na ukarabati wa majosho kwa kutumia fedha za *DADPs* na vyanzo vingine vya fedha. Aidha, naziomba Halmashauri zote nchini

ziendelee kuhamasisha vikundi vya ufugaji na watu binafsi kuchangia katika kuendesha majosho yaliyopo kwenye maeneo yao.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haijashindwa kujenga na kuendesha majosho. Katika Wilaya ya Kyela, Serikali imetekeleza mikakati mbalimbali na kuwashauri wafugaji kutumia pampu za mkono kama njia mbadala ya kuzuia magonjwa yanayoenezwa na kupe na mbung'o, kujenga majosho uchanjaji wa mifugo ili kuzuia ndigana kali na ufugaji wa ndani (*zero grazing*) ili kuongeza uzalishaji wa mifugo na kuwaongezea wafugaji kipato.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya juhudi hizo yamekuwa ni ongezeko la ng'ombe wa maziwa wanaofugwa ndani kutoka ng'ombe 3,129 mwaka 2001 hadi ng'ombe 4,485 mwaka 2003. Pia pato la wananchi wa Wilaya ya Kyela ni shilingi 450,000/= kwa mwaka ambalo ni pato la juu la wastani wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge akubaliane nami kuwa Serikali yetu ni makini katika kuboresha hali ya kipato cha wananchi wake kwa kuwawekea mazingira mazuri ya kazi na tutaendelea kusaidiana hilo kadri uchumi wa nchi unavyoendelea kukua.

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwa majibu yake mazuri, nina swali moja tu la nyongeza, kwa kuwa majosho yote kumi na mbili hayafanyi kazi kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwa kuwa sasa hivi amesema wamepeleka shilingi milioni 15 ambazo kwa kweli ningependa kuichukua nafasi hii kuishukuru Serikali.

Je, Waziri haoni kwamba hizi shilingi milioni 15 hazitoshi kwa kukarabati majosho yote hayo kumi na mbili ambayo hayafanyi kazi na ningepomba aongeze hizo fedha?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI k.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO):** Ni kweli majosho yote kumi na mbili yanakarabatiwa lakini Serikali imejitahidi kutoa kiasi kidogo hicho walichokitamka, lakini njia ya kudumu ya kufanikisha ukarabati wa majosho haya na matumizi yake ni kuunda ushirika wa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, wafugaji lazima waungane ili kuweza kuyaendesha haya majosho kwa faida yao na mambo haya yamefanyika katika wilaya nyingi sana na yamefanikiwa.

Mheshimiwa Spika, nawakaribisha waheshimiwa wafugaji wa Kyela waende kujifunza ushirika uliofanikiwa katika Kata ya Maoninga jimbo la Ismani wamefanikiwa sana katika jambo hili ni vizuri kwenda kujifunza. (*Makofi*)

Na. 73

**Mfumo wa Mabomba ya Maji katika Mji wa Lindi**

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imetoa fedha kwa ajili ya ufufuaji vyanzo vya maji ya uhakika katika Mji wa Lindi na kuwa na matumaini makubwa ya kupata maji ya kutosha, lakini tatizo lingine la Mji wa Lindi ni uchakavu wa mfumo wa mabomba ya maji yaliyoko ardhini yaliyowekwa kwa zaidi ya miaka 50 iliyopita na kwamba kwa hali yoyote ile hayataweza kusafirisha maji kwa maji ya uhakika yakipatikana na vile vile kulingana na ongezekao kubwa la watu kwenye maeneo hayo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mfumo wa mabomba ya maji sambamba na zoezi la kufufua vyanzo vya maji ili kuwaondolea kero wananchi walioko katikati ya Mji wa Lindi kwenye maeneo ya Ndovo, Makonde na Msinjahili?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI k.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mbunge wa Lindi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imetoa fedha kwa ajili ya ufufuaji wa vyanzo vya maji ya uhakika katika Mji wa Lindi. Katika kutekeleza mradi huu Wizara yangu imebuni na kutekeleza mradi wa dharura kwa maji mjini Lindi kama ifuatavyo:-

(i) Chanzo cha maji cha Liwayawaya kimekarabatiwa na pampu mpya mbili zimefungwa kwa gharama ya shilingi milioni 15.

(ii) Visima virefu vipya 13 vimechimbwa katika maeneo ya Mitwero na Kitunda kwa gharama ya shilingi milioni 227. Aidha, visima vitatu vimechimbwa mwaka 1999/2000 vimesafishwa. Kati ya visima vyote hivyo, visima kumi vimekubalika kutumika na vina uwezo wa kutoa maji kiasi cha lita milioni tano kwa siku ukilinganisha na lita 850,000 kwa siku kabla ya mradi.

(iii) Wizara ilitumia shilingi milioni 40 kununua pampu tatu kwa ajili ya visima virefu vitatu na tayari vimefungwa. Aidha, mabomba yenye urefu wa mita 1,500 ya kutoa maji kutoka kwenye visima hivyo hadi kwenye tanki yamenunuliwa na kufungwa.

(iv) Wizara pia ilitumia shilingi milioni 53 kununua na kufunga jenereta lenye uwezo wa kutoa umeme wa *KVA 135* kwa ajili ya kuendesha pampu za Kitunda.

(v) Shilingi milioni 27 zilitumika kununua tanki lenye ukubwa wa meta za ujazo 500 na kujengewa.

(vi) Bomba kuu jipya la maji ya mtiririko la kipenyo cha milimita 150 lenye urefu wa mita 1,700 na mabomba madogo ya kuunganisha visima na matanki yamenunuliwa na kulazwa kwa gharama ya shilingi milioni 173 na wakati huo huo bomba kuu la zamani la

kipenyo cha milimita 150 lenye urefu wa mita 3,250 limekarabatiwa. Kadhalika bomba kuu lingine la kipenyo cha milimita 200 lenye urefu wa mita 1800 chini ya bahari hadi kituo cha kusukuma maji cha *Dockyard* kimekarabatiwa.

(vii) Bomba kuu lenye kipenyo cha milimita 250 limekarabatiwa urefu wa mita 1,200 kwa gharama ya shilingi milioni 15.

(viii) Ujenzi wa nyumba tatu za wafanyakazi eneo la Kitunda unaendelea na zitagharimu shilingi milioni 25.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kazi zilizokwishafanyika zimegharimu kiasi cha shilingi milioni 650. Kazi ambazo zimebaki ili mradi huo ukamilike ni pamoja na kufunga mitambo ya visima virefu vitatu eneo la Kitunda, kulaza bomba kuu la maji ya mitiririko la kipenyo cha milimita 150, kukarabati kituo cha kusukuma maji eneo la *Dockyard* na kukamilisha ukarabati wa bomba la kipenyo cha milimita 250 la kupeleka maji hadi tanki kubwa la kuhifadhi maji lililoko eneo Wailesi kazi hizi ambazo zitagharimu jumla ya shilingi milioni 150 zinaendelea kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba mfumo wa mabomba ya maji katika mji wa Lindi ni wa zamani na umechakaa. Hata hivyo kutokana na ufinyu wa Bajeti, Serikali na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Lindi zinaendelea kufufua mtandao wa mabomba yote chakavu katika mji wa Lindi yakiwemo maeneo ya Ndovo, Makonde na Misingahili ambapo jumla ya mita 1,200 za bomba kuu zimekarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, kadhalika Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Serikali ya Japan ili tuweze kupata chanzo kipya cha maji kitakachokidhi mahitaji ya maji ya muda mrefu kwa mji wa Lindi pamoja na kuimarisha na kupanua mfumo wa maji safi na ujenzi wa mfumo wa uondoaji majitaka.

Na. 74

### **Barabara ya Iringa - Minjingu**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Iringa - Dodoma - Minjingu ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu na ukuaji wa Mji wa Dodoma ambao ni Makao Makuu ya nchi; na kwa kuwa barabara hiyo ni mbaya sana:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoia Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara ya Iringa - Dodoma - Minjingu kwa maendeleo ya Taifa letu hasa ikizingatiwa kwamba ni sehemu ya barabara ya *The Great North Road*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inajitahidi sana kuhakikisha kwamba sehemu zote za nchi hii pamoja na nchi jirani na nyingine za Afrika zinakuwa na mawasiliano mazuri hasa ya barabara ikiwa ni pamoja na mji wa Dodoma kwa lengo la kukuza uchumi na kuleta maendeleo katika maeneo zinapopita barabara za lami. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali pamoja na baadhi ya wahisani kutotimiza ahadi wanazozitoa, imebidi miradi itekelezwe kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa barabara ya Dodoma - Minjingu na Dodoma - Iringa ambayo ni sehemu ya *The Great North Road* juhudi zimekwishafanyika ambapo barabara hii imejumuishwa katika barabara zitakazojengwa kwa mpango wa Jumuiya ya Ushirikaiano wa Nchi za Afrika Mashariki.

Kwa kupitia mpango huu, barabara za Ukanda wa Tunduma - Iringa - Dodoma - Arusha - Namanga - Nairobi - Isiolo - Moyale zimepewa umuhimu namba moja katika ratiba ya utekelezaji. Chini ya mpango huu, Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), imekubali kufadhili ukarabati wa sehemu ya Namanga - Arusha yenye urefu wa kilometa 105. Utekelezaji wa mradi huu upo kwenye hatua ya usanifu ambao utafuatiwa na utishaji wa zabuni za ujenzi mwaka wa fedha 2005/2006.

Aidha, kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka wa fedha 2004/2005, barabara ya Dodoma - Iringa yenye urefu wa kilometa 267 itafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Shilingi milioni 900 zimetengwa kwa kazi hiyo. Vile vile, barabara ya Dodoma - Babati yenye urefu wa kilometa 261 nayo itafanyiwa usanifu chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia, jumla ya shilingi bilioni 1.51 zimetengwa kwa kazi hiyo.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali ya nyongeza, aidha, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kwa muda mrefu Serikali ilikuwa ikitegemea fedha za wafadhili kwa ajili ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami; na kwa kuwa fedha hizi za wafadhili hazipatikani, je, Serikali haioni ni busara sasa itenge fedha za ndani kuweza kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Pascal Degera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa fedha za wafadhili mara nyingi imekuwa ni vugumu kuzipata kwa muda unaotaka na pengine usizipate kabisa, lakini kama utakumbuka katika Bajeti iliyopita tulitoa kitabu cha nyongeza na barabara hii ya kutoka Arusha - Dodoma, Dodoma - Iringa, tumeiweka wazi kwa mpango wa *BoT* ili kama wapo watu wenye fedha wanataka kutengeneza barabara hii waje. Pale ambapo itashindikana kabisa basi Serikali itachukua ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na kuufanyia kazi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yote yamejibiwa, sasa tunaendelea na kazi nyingine.

Kwanza matangazo ya vikao vya leo, lakini kabla ya matangazo ya vikao vya leo nimeambiwa na Makatibu Mezani kwamba kumetokea kasoro ndogo tu ya utendaji katika kugawa makaratasi ya kushughulikiwa ndani ya Bunge hili leo asubuhi, nayo ni kwamba karatasi zilizogawiwa ni hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Wilson Masilingi, wakati akiwasilisha Bungeni Azimio la Kuridhia Mkataba wa Umoja ni hotuba ya Waziri ndiyo iliyogaiwa badala ya kugawa Azimio lenyewe.

Sasa kumetokea matatizo hayo ya utendaji, nitawaomba sasa wahudumu wa Bunge wagawe Azimio lenyewe ambalo litawasilishwa na si hotuba ya Waziri.

Matangazo ya vikao vya leo kuna Kamati tatu zikazofanya vikao siku ya leo, ya kwanza ni Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti anawatangazia Wajumbe wake kwamba kutakuwa na kikao saa tano asubuhi hii ukumbi namba 231. Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Kamati ya pili ni Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa George Lubeleje, Makamu Mwenyekiti anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba kutakuwa na kikao saa tano asubuhi vilevile chumba namba 133 ili kushughulikia Muswada wa Sheria (*The Regional Laws* *Miscellaneous Amendments*). Hiyo ni Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Kamati ya mwisho ni Kamati ya Fedha na Uchumi, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Lephy Gembe, anaomba Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi wakutane leo saa tano asubuhi hiyo hiyo chumba namba 231. Mwisho wa matangazo ya vikao. Sasa tunaendelea na *Order Paper*, Katibu.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **MAAZIMIO**

**Azimio Kuridhia Mkataba wa wa Umoja wa Afrika kuhusu Kupambana na Rushwa (*The African Union Convection on Preventing and Combating Corruption*).**



**Azimio la kuridhia Mkataba wa Kimataifa Dhidi ya Rushwa**  
*(The United Nations Convention Against Corruption)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha Azimio la Kwanza linalohusu Mkataba wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa, naomba nitoe maelezo machache mbele ya Bunge lako Tukufu.

Kwanza kabisa napenda kutoa shukrani za dhiti kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Alhaji Athumani Janguo na Msaidizi wake Mheshimiwa George Lubeleje na Kamati nzima kwa uchambuzi na ushauri tulioupata.

Pili, natoa shukrani kwa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano ambao tumeupata katika kuandaa Maazimio, mwisho nawashukuru wataalam wa Ofisi ya Rais, Ikulu wakiongozwa na Mheshimiwa Katibu Mkuu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa msaada waliotupatia kuandaa Maazimio haya.

Mheshimiwa Spika, rushwa ni tatizo la dunia na hivyo Afrika ambapo nchi zake zinapita katika kipindi cha mpito cha kujenga uchumi wake na kuimarisha utawala bora, kuheshimu haki za binadamu, kudumisha demokrasia na kushirikisha wananchi wake katika maendeleo yao lazima iweke mikakati ya kuikabili.

Katika kutambua hilo viongozi wa wakuu wa Umoja wa Nchi za Afrika katika mkutano wao wa tarehe 12 Julai, 2003 Mjini Maputo, Msumbiji walipitisha na kuwekea saina mkataba wa Umoja wa Afrika wa kuzuia na kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, maelezo haya ambayo tunayatoa kwa kifupi kabisa yanalenga kuwashawishi Waheshimiwa Wabunge kutafakari maudhui ya Mkataba, kuyaafiki na hatimaye kuridhia Mkataba huo. Kuridhia Mkataba huo kutaiweka nchi yetu katika nafasi nzuri ya kushirikiana na nchi nyingine za Kiafrika katika kupambana na rushwa, pia nchi yetu kwa kushirikiana na nchi nyingine itakuwa katika nafasi nzuri ya kuwanasa wala rushwa wa aina yoyote ndani na nje ya nchi. Ni misingi hii Tanzania ikubali kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, malengo ya mkataba huu yametamkwa katika Ibara ya pili ya Mkataba ikiwa ni pamoja na kuanzisha na kuimarisha taratibu za kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa, kushirikiana miongoni mwa nchi za Kiafrika, kuhakikisha kuna hatua madhubuti za kuzuia na kupambana na rushwa na makosa yanayohusiana na rushwa, kuratibu na kupatanisha sera na sheria za nchi za Afrika kwa madhumuni ya kuzuia na kupambana na rushwa na kuanzisha mazingira ya uwazi na uwajibikaji katika uendeshaji wa kazi za umma.

Mheshimiwa Spika, misingi ya mkataba huo imeainishwa katika Ibara ya tatu ya Mkataba ikiwa ni pamoja na kuheshimu demokrasia na taasisi zake, ushirikishwaji,

utawala wa sheria, utawala bora, kuheshimu haki za binadamu, uwazi na uwajibikaji, kuzingatia haki katika nyanja za kijamii na kiuchumi na kukemea na kukataa vitendo vya rushwa na vya jinai vinavyohusiana na rushwa bila hofu ya kuadhibiwa.

Mheshimiwa Spika, vitendo vya rushwa vimeainishwa kwenye Ibara ya nne ya Mkataba, vingi ni kama vilivyo katika sheria ya kuzuia rushwa ya Tanzania, tofauti kubwa ipo katika kipengele (g) cha Ibara hiyo kinachoeleza kosa la kujitajirisha isivyo halali kulinganisha na kifungu cha tisa cha kuzuia rushwa kinachozungumzia kuwa na mali inayotokana na vitendo vya rushwa.

Mkataba unaelekeza nchi wanachama kuweka sheria na kuchukua hatua zingine za kukidhi malengo yaliyotamkwa katika Ibara ya pili ya Mkataba, Tanzania tayari imekwishatekeleza sheria na hatua zilizotamkwa katika Ibara ya tano ya Mkataba huo. Kwa mfano, Tanzania tayari inayo sheria ya kuzuia rushwa ambayo itarekebisha kuzingatia vipengele vya makosa yaliyopo kwenye mkataba ambayo hayapo kwenye sheria yetu.

Kipengele cha pili cha Ibara ya 5 kuhusu udhibiti wa makampuni ya nje yaliyopo nchini kuheshimu sheria za nchi, sheria ya makampuni ya mwaka 2000 imezingatia suala hilo.

Mheshimiwa Spika, tunayo Taasisi ya Kuzuia Rushwa inaendelea kuimarishwa kama kipengele cha tatu cha Ibara ya tano ya mkataba huu kinavyoagiza. Kipengele cha nne kimezingatiwa katika sheria ya umma, sheria ya ununuzi wa mali za umma na sheria ya Mamlaka ya Mapato.

Aidha, marekebisho ya sheria ya Kuzuia Rushwa yatazingatia kuwalinda watoa habari (*Informance Witnesses and Wiser blowers*) kama kipengele cha tano kinavyoagiza. Marekebisho ya sheria hiyo yatazingatia pia kuwaadhibu wale wanaotoa taarifa za uongo dhidi ya wananchi wasio na makosa.

Mwisho, zipo taratibu za Taasisi ya Kuzuia Rushwa, Wizara, Idara, Wakala wa Mikoa na Wilaya, kuwaelimisha wananchi juu ya athari za rushwa hatua hizi zimeendelezwa kwenye shule, vyombo vya habari na Taasisi za wananchi kama kipengele cha nane cha mkataba huu kinavyoelekeza. Hatua hizi zitaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine kama kuweka sheria ya kuyafanya makosa ya jinai, vitendo vya mapato ya kificho au yale yanayotokana na rushwa yanaendelea kuchambuliwa na sekta ya sheria ili kuona namna gani Ibara ya sita ya mkataba huu itakavyotekelezwa.

Aidha, Ibara ya saba imeanza kutekelezwa kwa viongozi kutamka mali zao kwa Kamishna wa Maadili kama sheria inavyoagiza kwa watumishi wa umma na kila Wizara, Idara, Wakala inao (*Fork Persons*) watu ambao ni maafisa wetu wanaowasiliana na vyombo vyetu, wanaoratibu mkakati wa Kitaifa kupambana na rushwa na mpango maalumu wa utekelezaji wake. Karibu zabuni zote za Serikali zimewekewa sheria na kanuni za wazi katika zabuni na utekelezaji wake unaendelea kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwisha agiza idara zote na taasisi za Serikali kuwa na maafisa habari ambao watatoa habari za idara kwa vyombo vya habari na wadau wengine, Ikulu kipo kitengo cha mawasiliano chini ya Ofisi ya Rais kukidhi matakwa ya Ibara ya tisa ya mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, sheria ya vyama vya siasa imeweka utaratibu wa namna ya vyama kupata mapato ikiwa ni pamoja na ruzuku, hata hivyo bado mjadala unaendelea katika eneo hili kupata utaratibu muafaka kwa wadau wote isipokuwa fedha inayotolewa kupokelewa kwa njia za rushwa au kinyume cha sheria ni makosa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutafakari utaratibu mzuri wa mapato ya vyombo vya siasa kwa kuzingatia Ibara ya 10 ya Mkataba.

Mheshimiwa Spika, sekta binafsi inaendelea kushamiri na kuanza kuchukua nafasi yake katika uchumi wa Taifa hivyo sheria ya manunuzi (*Public Procurement Act of 2001*) na sheria ya makampuni kwa pamoja zina nia ya kudhibiti makampuni yasitumie rushwa kupata zabuni au mashindani yasiyo ya haki.

Aidha, Mkakati wa Kitaifa wa kupambana na rushwa na mpango wake unayo malengo ya kufanya sekta binafsi kuwajibika na mapambano dhidi ya rushwa miongoni mwake. Sheria ya kuzuia rushwa inamhusu mtu yeyote anayetoa au kupokea rushwa awe afisa wa umma au mtu binafsi, hiyo ni kwa mujibu wa Ibara ya 11 wa Mkataba.

Taasisi za wananchi (*Civil Society Organizations*) na vyombo vya habari wamepewa nafasi muhimu katika mkakati wa kupambana na rushwa ingawa baadhi ya Taasisi za wananchi ni changa na uwezo wao ni mdogo lakini zimeanza kushiriki katika vita dhidi ya rushwa kwenye shule na sehemu za kazi. Vyombo vya habari siyo tu kuwa ni vingi bali pia uhuru na utaalumu wa vyombo hivi unaimarika hususan katika kufichua rushwa na kashfa mbalimbali kwa mujibu wa Ibara ya 12.

Maeneo mengine ya Mkataba kama ya Mamlaka kwa mujibu wa Ibara ya 13, hakikisho la mashitaka ya haki kwa mujibu wa Ibara ya 14, kulegesha mkosaji kwa mujibu wa Ibara ya 15, usiri wa mabanki kwa mujibu wa Ibara ya 17 na ushirikiano kwa mujibu wa Ibara ya 18 na 19 zipo taratibu za Kitaifa na Kimataifa ambazo Tanzania inazifuata na itaendelea kuzihusha kulingana na Mkataba huu na mingine iliyopo. Ibara ya 20 na 28 ni maelekezo ya utekelezaji baada ya Mkataba kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache mbele ya Bunge lako Tukufu, kwa idhini yako naomba nisome Azimio kama lilitavyo:-

KWA KUWA Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa nchi za Afrika na ambazo zimeamua kujiunga na Mkataba wa Umoja wa nchi za Kiafrika kuimarisha juhudi za kuzuia na kupambana na vita dhidi ya rushwa kwa ufanisi zaidi ikiwa ni pamoja na kuwatambua na kuwachukulia hatua za kisheria wala rushwa;

KWA KUWA mkataba wa Umoja wa Nchi za Afrika wa kuzuia na kupambana rushwa una lengo la kuunganisha juhudi za pamoja katika kupambana na rushwa; na kwa

kuwa Tanzania itapata manufaa zaidi hasa baada ya kubuni sera ya kuzuia na kupambana na rushwa nchini kama ilivyotamkwa kwenye Ibara ya tano ya mkataba na kwamba Tanzania inacho chombo cha kudhibiti na kupambana na kuzuia rushwa;

KWA KUWA kwa kwa kuridhia Mkataba huo Tanzania itafaidika na ushirikiano wa Kimataifa katika kupambana na rushwa ikiwa ni pamoja na kurejesha wahalifu, kusaidia na kusaidiwa kwenye masuala ya kisheria katika kukamata mali na mapato yaliyopatikana kwa njia za rushwa na kurejesheana mali mapato hayo kwa nchi mwanachama;

KWA KUWA Ibara ya 19 ya Mkataba huu inasisitiza ushirikiano wa Kimataifa katika kupambana na rushwa, kudhibiti ufujaji wa fedha chafu, Tanzania itaendelea kuimarisha vyombo vyake vya dola na usimamizi wa Mabenki ili kuona kwamba mashirikiano hayo yanatokomeza tatizo la rushwa na ufuaji wa fedha chafu.

KWA HIYO BASI na kwa kuzingatia umuhimu wa faida ambazo zitapatikana kutokana na kuridhia mkataba wa Umoja wa Nchi za Kiafrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa, kwa mujibu wa Ibara ya 63, fasili ya 3(a) ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Bunge hili sasa linaazimia kuridhia Mkataba wa Umoja wa Nchi za Kiafrika wa kuzuia na kupambana na rushwa kwa mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako naomba niendelee na Azimio linalofuata.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi za kwanza kuweka saina Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kuzuia na kupambana na rushwa, tukio lililofanyika mjini Merida, Mexico tarehe 9 Desemba, 2003. Mkataba huo wa Umoja wa Mataifa unayo mambo ambayo baadhi yake Tanzania tayari imekwisha yatekeleza kwa msukumo wa mazingira ya ndani ya nchi.

Madhumuni ya maelezo yangu ni kuwaomba kutafakari maudhui ya Mkataba, kuyaafiki na hatimaye kuridhia Mkataba huu.

Shabaha muhimu katika mkataba huu ni kuwezesha na kuimarisha juhudi za kuzuia na kuendesha vita dhidi ya rushwa kwa ufanisi zaidi nchi zote za Umoja wa Mataifa zikishirikiana na kuongeza na kusaidia juhudi za Kimataifa katika kuzuia na kupambana na rushwa ikiwa ni pamoja kuwatambua na kuwachukulia hatua za kisheria wala rushwa.

Pia kuwa na utaratibu wa kurejesha Serikalini mali zinazopatikana kutokana na vitendo vya rushwa, kadhalika mkataba unalenga katika kujenga na kuimarisha tabia ya uadilifu, uwajibikaji na usimamizi unaofaa katika kuendesha shughuli za umma pamoja na usimamizi wa mali ya umma.

Mheshimiwa Spika, sura ya pili ya Mkataba inaweka utaratibu wa kila nchi kuweka sera za kuzuia na kupambana na rushwa kwa mujibu wa Ibara ya tano, kuwa na

chombo cha kupambana na rushwa Ibara ya sita na kuwa na kanuni za maadili kwa mujibu wa Ibara ya nane.

Mbali na vyama vya siasa kujiwekea sera za kupambana na rushwa katika Ilani za vyama Serikali tayari inao Mkakati wa Kitaifa wa kuzuia na kupambana na rushwa na mpango maalum wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya tano, sita na nane, mkakati huo unaagizwa unandaliwe na nchi wanachama na sisi tayari tumeanza kutekeleza utaratibu huo, utaratibu wa kutekeleza Ibara ya saba ya Mkataba huu katika sekta ya umma unaendelea kuzingatiwa katika Mpango wa Kurekebisha Sekta ya Umma (*Public Sector Reform Program*).

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ibara ya tisa inayohusu manunuzi ya umma na usimamizi wa fedha za umma, Serikali inaendelea kuimarisha taratibu zilizopo kwenye sheria za manunuzi (*Public Procurement Act*) na sheria ya Fedha za Umma (*Public Finance Act*) za mwaka 2001 zilizopitishwa na Bunge hili Tukufu na kwenye marekebisho ya sekta ya fedha kwa ujumla. Bajeti hivi sasa inadhibitiwa kwa ufanisi zaidi, hatua kuhusu Mahakama na mashtaka katika Ibara ya 11 yanazingatiwa katika marekebisho ya Sekta ya Sheria (*Sector Reform Program, Legal Sector Reform Program*). Mjadala juu ya kudhibiti maadili na rushwa katika sekta binafsi kwa mujibu wa Ibara ya 12 unaendelea ndani na nje ya Serikali

Mheshimiwa Spika, sura ya tatu ya mkataba inaeleza juu ya kuyafanya makosa ya jinai, vitendo vya hongo kwa watumishi wa umma kwa mujibu wa Ibara ya 15, hongo kwa afisa wa nchi za nje au taasisi za Kimataifa kwa mujibu wa Ibara ya 16, ubadhilifu au kutojali majukumu kwa mujibu wa Ibara ya 19, kujitajirisha kwa njia haramu hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 20, ubadhilifu katika sekta binafsi kwa mujibu wa Ibara ya 22, kuwa na mapato haramu kwa mujibu wa Ibara ya 23, kuficha makosa kwa makusudi kwa mujibu wa Ibara ya 24 ya mkataba huo na kuzuia haki kwa mujibu wa Ibara ya 25.

Baadhi ya makosa hayo yapo katika sheria mbalimbali za nchi kama kanuni za adhabu (*Pin Code Cap. 16*) makosa mengine kama *laundrying proceeds of claim* kwa mujibu wa Ibara ya 23 yatafanyiwa marekebisho baada ya mkataba kuanza kutumika kama sheria ya nchi, Ibara ya 26 hadi ya 42 ni mchakato wa namna ya kuimarisha taratibu za kimahakama na mambo ya kuzingatia wakati huo.

Mheshimiwa Spika, sura ya nne ya mkataba inahusu ushirikiano wa Kimataifa katika masuala ya rushwa ikiwa ni pamoja na kurejesha mhalifu kwa mujibu wa Ibara ya 44, kusaidiana kisheria kwa mujibu wa Ibara ya 46, kuhamisha mashitaka kwa mujibu wa Ibara ya 47, ushirikiano wa Taasisi zinazopambana na rushwa katika uchunguzi au upepelezi wa pamoja, kubadilishana habari na kupeana ustadi na ujuzi. Taratibu zilizoainishwa katika sura hii ni zile zinazofuatwa Kimataifa kwa hiari lakini sasa baada ya mkataba kuanza kutumika basi nchi ikiwa ni pamoja na nchi yetu Bunge likiridhia tutatunga sheria za kuutekeleza.

Mheshimiwa Spika, sura ya tano inahusu namna ya kupata tena mali iliyopotea kwa njia za rushwa au zisizohalali, hatua hizi ni pamoja na nchi mwanachama kuruhusu nchi nyingine iliyopoteza mali kwa njia hizo ipate mali yake kupitia kufungua shauri la madai kwa mujibu wa Ibara ya 53 au kupitia ushirikiano wa kimataifa wa kumnyang'anya mhalifu na kuirudisha kwa nchi alikoitoa au kuiba kwa mujibu wa Ibara za 54, 55, 56, na 57.

Aidha, kwa madhumuni ya kunyang'anya mali nchi zinapaswa kuwa na kitengo cha utambuzi wa fedha (*Financial Interagency Unit*) kwa mujibu wa Ibara ya 58, sura ya sita inahusu misaada ya kiufundi na kubadilisha habari hususan mafunzo kwa mujibu wa Ibara ya 60 na uchambuzi wa pamoja wa habari juu ya rushwa sura ya saba ya mkataba ni taratibu za kutekeleza mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kuridhia kwa mkataba huu kutasaidia Tanzania kushirikiana na Mataifa mengine kupambana na rushwa ndani na nje ya nchi, pia nchi itaweza kuwajua watu wanaoishi nje ya nchi wanaofanya vitendo hivyo hapa nchini. Kadhalika Tanzania itaweza kurejesha nchini iwapo hilo litatokea mali iliyotoroshwa au itakayotoroshwa nje ya nchi yetu na kuwabana na kuwarejesha nchini watu wanaotorosha mali za nchi yetu nje ya nchi kwa sababu ya kuhusika na vitendo vya rushwa, Mabadiliko haya yatazingatiwa katika zoezi la kurekebisha sheria ya makosa ya rushwa linaloendelea.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya mafupi kwa idhini yako naomba kusoma Azimio lenyewe:-

KWA KUWA Tanzania ni moja ya nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa na kwa kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi za kwanza kuweka saina katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kuzuia na kupambana na rushwa huko Mexico, mnamo tarehe 9 Desemba, 2003 ili kuimarisha juhudi za kupambana na vitendo vya rushwa kwa ufanisi zaidi;

KWA KUWA Mkataba wa kuzuia na kupambana na rushwa unalenga katika kuvifanya vitendo vya hongo kwa watumishi wa umma, maofisa wa nchi za nje au taasisi za Kimataifa, ubadhirifu wa wizi;

NA KWA KUWA kwa kujiunga na Mkataba huu Tanzania itaweza kushirikiana na Mataifa mengine katika kupambana na rushwa ndani na nje ya nchi na vili vile kuwatambua watu walioko nje ya nchi wanaofanya vitendo vya rushwa nchini, biashara ya ushawishi, kujitajirisha kwa njia haramu na kuwa na mapato haramu na ubadhirifu katika sekta binafsi mambo ambayo tayari ni makosa kwa mujibu wa sheria mbali mbali za nchi yetu kuwa ni makosa ya jinai;

KWA KUWA kujiunga na Mkataba huo Tanzania itajiweka mazingira mazuri zaidi katika kupambana na rushwa hasa baada ya kuweka sera za kuzuia na kupambana na rushwa nchini na kwamba Tanzania tayari inacho chombo kilichoundwa mahsusi kwa madhumuni hayo;

KWA KUWA kwa kujiunga na mkataba huu Tanzania itafaidika kwa kushirikiana na Mataifa mengine katika kupambana na rushwa ndani na nje ya nchi na vilevile kuwatambua watu walioko nje ya nchi wanaofanya vitendo vya rushwa nchini;

KWA KUWA kwa mujibu wa Mkataba huu Tanzania itaweza kupata tena mali iliopotea kwa njia za rushwa iwapo itabainika au njia zisizo halali kwa kuziwajibisha nchi wanachama kuruhusu nchi zilizopoteza mali kurejeshwa mali zao kwa njia ya mashauri, ya madai ya taratibu ya ushirikiano wa Kimataifa;

KWA KUWA nchi pia inanufaika na misaada ya kiufundi, ubadilishanaji wa habari, mafunzo na uchambazi wa pamoja wa habari zinahohusu rushwa;

KWA HIYO BASI kwa kuzingatia umuhimu huo na kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Kumi na Saba sasa linaazimia kuridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kuzuia na kupambana na rushwa (*The United Nations Convention Against Corruption of 2003*).

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja ya kuwasilisha maazimio haya mawili imetolewa na imeungwa mkono sasa tunaendelea kwa mujibu wa utaratibu wetu namwita mwakilishi wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala, Makamu Mwenyekiti atoe maoni ya Kamati yake.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii nitoe maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa mujibu wa kanuni namba 70, kifungu cha 2, kanuni za Bunge toleo la mwaka 2004 sasa naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba Sheria na Utawala baada ya kukamilisha kazi ya kuufikiria Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Rushwa (*African Union Convention and Preventing and Converting for Corruptions and United Nations Convention Against Corruption*) iliyoletwa mbele ya Kamati yangu na Serikali tarehe 25 Oktoba, 2004.

Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu rushwa ni suala nyeti linalogusa maisha ya kila siku ya mwananchi na ndiyo maana tunasema rushwa ni adua wa haki, itokeapo mwananchi ananunua huduma katika nchi yake ambaye ni haki yake ya

kimsingi basi hata heshima ya Taifa lake hushuka. Kwa sababu hiyo basi jitihada zozote zile ziwe za Kimataifa, Kikanda au Kitaifa za kupambana na rushwa hazina budi kuungwa mkono.

Mheshimwa Spika, kwa mantiki hiyo Kamati yangu inaupongeza Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika kwa kuliona tatizo hili na kuanzisha Mikataba hii yenye lengo la kushirikisha nchi zote duniani, Taasisi na Asasi mbalimbali kukabiliana na tatizo hili kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea maelezo ya Mheshimiwa Waziri, Kamati yangu imeitafakari kwa kina maudhui ya mikataba hii miwili, kubwa lililojitokeza katika matatizo yetu ni kuwa nchi yetu ilikwishapiga hatua kubwa katika kutunga sheria dhidi ya rushwa kwa muda mrefu. Kati ya sheria hizo ni Sheria ya rushwa ya mwaka 1971, Sheria ya Uhujumu Uchumi ya mwaka 1984, Sheria ya Fedha yaani *The Public Finance Act 2001* na Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2001 yaani *The Public Procurement Act 2001*.

Pamoja na kuwepo kwa sheria hizi, Kamati yangu inakiri kuwa bado tatizo la rushwa limeendelea kuongezeka siku hadi siku na hasa kushamiri kwa rushwa zinaoelezwa kwenye mikataba ambazo ndizo hasa zinazobomoa uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaamini kwamba kuwa na Mikataba ya sheria nyingi zinazokabiliana na rushwa peke yake hakutoshi, Kamati yangu inadhani na kuamini kuwa utekelezaji wake unakwama kwa kiasi fulani kwa sababu hatujajielekeza hasa kwenye chanzo cha tatizo la rushwa.

Pamoja na kuwa na mikataba ya sheria hizi tungekuwa na Mikataba pia ambayo itashughulikia uchumi wa Mwafrika au Mtanzania, Mikataba hii izielekeze nchi zetu jinsi ya kuwawezesha wananchi ili waepukane na vishawishi. Tunadhani wananchi wawezeshwe kiuchumi kwa vile katika dunia ya leo umaskini unachangia sana katika kuendeleza rushwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia iliangualia kwa makini Taasisi ya Kuzuia Rushwa. Kwanza Kamati inakiri kuwa chombo hiki kinajitahidi kufanya kazi kwa uwezo wake wote, hata hivyo Kamati imebaini kuwa kuna sheria na taratibu nyingi ambazo zinakibana chombo hiki kisiwe na meno na hivyo kutofanya kazi yake ipasavyo. Kwa mfano, chombo hiki kinaweza kufungua mashtaka dhidi ya mtu fulani lakini Mkurugenzi wa mashitaka anayo mamlaka ya kisheria kufuta mashtaka kwa kulinda maslahi ya umma.

Kamati inapendekeza kuwa Taasisi ya Kuzuia Rushwa kiwe chombo kinachojitegemea ili kiwe na nguvu za kujiamulia mambo yake chenyewe.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo Kamati yangu iliangualia kwa makini ni kuhusu matamko ya mara kwa mara ya Serikali kuwataka wananchi watoe ushahidi pale wanapoonekana kutuhumu ama Serikali, mtumishi wa umma au chombo chochote cha



umma. Ingawa wakati mwingine kauli hizo hutolewa kisiasa zaidi. Kamati yangu inaamini kuwa kwa hali yoyote ile mtu binafsi hawezi kukusanya ushahidi kama kinavyoweza kukusanya chombo cha dola. Anachoweza ni kutoa taarifa kwa vyombo vinavyohusika. Kiutaratibu ni dola tu ndiyo yenye uwezo wa kuchunguza, kuhoji, kutia nguvuni na kukusanya vyanzo vyote vya ushahidi.

Kamati inashauri kuwa Serikali iepuke kutoa kauli za namna hii kwani kumpa mwananchi jukumu hili kwanza ni kumtisha na kumfanya aogope kabisa kuingilia suala la rushwa hata kama anazo taarifa muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu pia iliongelea juu ya kukomaa kwa rushwa kupitia mbinu za fedha chafu. Bila shaka Waheshimiwa Wabunge kupitia semina mbalimbali wanakumbuka kuhusu dhana hii ya fedha chafu. Hata hivyo, Kamati yangu inaamini kuwa baadhi ya watu wanaocheza mchezo huu ama wanajificha migongoni mwa watu wenye nyadhifa kupitia Vyama Siasa au Serikalini kwa kuwa hili ni eneo mojawapo la hatari kwa uchumi nchi. Kamati inashauri Serikali ilianganalie kwa makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu pia iliongelea juu ya upungufu unaojitokeza katika sheria ya manunuzi ya mwaka 2001 *(The Public Procurement Act, 2001)*, hususan kutoshirikishwa kwa Madiwani katika Baraza la *Tender* la Halmashauri za Wilaya, Jiji au Manispaa. Kamati inaamini kuwa kuwaachia watendaji peke yake katika Baraza la *Tender* kunaweza kufanya wakatamia nafasi hiyo kujiingiza katika vitendo vya rushwa. Hivyo, Kamati inashauri kuwa Sheria hii ifanyiwe marekebisha ili angalau baadhi ya wawakilishi au wananchi nao wahusishwe ili waweze kusimamia vyema miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo Kamati yangu ililiongelea kwa kirefu ni udhaifu wetu uliopo katika kudhibiti fedha za kigeni katika maduka ya biashara ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, sote sisi ni mashahidi kuwa maduka mengi ya binafsi yanayojishughulisha na biashara za fedha za kigeni hayatoi risiti bila mteja mwenyewe kudai, hali hii ni tofauti na nchi nyingine za wenzetu. Ukienda kununua fedha katika maduka yao wao hukupa risiti hapo hapo na rekodi yake huenda Benki Kuu, lakini hapa kwetu ni tofauti. Fedha zinanunuliwa na kuuzwa ovyo ovyo na hatujui kama Benki Kuu wana taarifa za kiasi cha fedha zinazouzwa na kununuliwa kwa siku.

Mheshimiwa Spika, sekta muhimu kama hii si ya kuachwa hivi hivi, kwani inaweza kufungua milango ya rushwa, matumizi mabaya ya fedha na kuikosha Serikali mapato. Kamati yangu inashauri kuwa Serikali ianganalie kwa makini suala hili na kufuatilia wote wanaokiuka utaratibu na kuwahamasisha wananchi wawe wakidai risiti.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu pia ilijielekeza katika eneo la madini. Bunge lako Tukufu litakumbuka kuwa katika semina kadhaa za madini huko nyuma tulielezwa kuwa licha ya Tanzania kuwa na madini mengi inapokea asilimia ndogo ya mrahaba.

Aidha, iliwahi kuelezwa kuwa sisi tunatofautiana na wenzetu wa nchi nyingine kwa kuwa hatuna hisa kwenye madini yaliyo nchini na kwamba mapato yetu ya hisa yaani *three rate share* ya madini hayako wazi, jambo ambalo linaleta mazingira ya rushwa. Kamati inaishauri Serikali itupie macho eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo maeneo ya jumla ambayo Kamati yangu iliyaangalia na kutoa maoni, yale ambayo sikuweza kuyaongelea natumaini Waheshimiwa Wabunge wa Kamati yangu watayazungumzia wapatapo nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Wilson Masilingi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora pamoja na wataalam wake kwa kuwasilisha maelezo yao kwa ufasaha mbele ya Kamati yangu.

Mwisho, kabisa nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu kwa uchambuzi wa kina wakati wote wa kujadili Mikataba hii, uelewa na uzoefu wao katika masuala ya rushwa, Kitaifa na Kimataifa umesaidia sana kuboresha maoni ya Kamati na kuisaidia Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi kuwatambua wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambao ni Mheshimiwa Athumani Janguo, Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Salim Omar Ali, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa. Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Ramadhani Hashim Khalfan, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Paschal Degera na Mheshimiwa Nimrod Mkono.

Naishukuru pia Ofisi ya Katibu wa Bunge kwa kuihudumia Kamati vizuri bila kuwasahau Makatibu wa Kamati hii Ndugu Ernest Zulu na Ndugu Charles Mloka, kwa kuwa makini katika kufuatilia maoni ya Kamati na kuyatayarisha kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5) (b) (c) na 81(1) Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Maazimio haya kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge hili, kwani Tanzania ilikwishakubaliana na mambo yote yaliyomo kwenye Mikataba yenyewe na ndiyo sababu yalikwishasainiwa. Kutekeleza Mikataba hii itaisaidia Tanzania iweze kupambana na rushwa ya Kimataifa inayokuja kuharibu uchumi wetu na kutuchagulia viongozi na hivyo kuwanyima haki Watanzania ya kujiamulia mambo yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Azimio hili kifungu cha kwanza kipengele kinachosema: *“Illicit enrichment,”* tunashukuru na wenzetu wameliona tatizo hili na hapa kwetu tunasheria hiyo, lakini inazunguka mno licha ya kuwa mambo yako wazi, utekelezaji wake hapa kwetu ni mgumu. Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie jambo hili kwani hali ni mbaya sana hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha pili cha madhumuni, kipengele cha nne kwenye haki ya kisiasa, hii vile vile ipo kwenye Katiba yetu, lakini kwa sasa wakati tunaelekea kwenye uchaguzi kunatokea mambo ya uvunjwaji wa haki hii kwa wagombea uongozi wa vyama vya Upinzani kubambikizwa makosa na kuwekwa ndani, uchaguzi unapomalizika na wao wanaachiwa huru, hii inawanyima haki zao za Kikatiba za kuchagua na kuchaguliwa.

Kambi ya Upinzani, inamwuliza Mheshimiwa Waziri analishughulikiaje hili la viongozi kutumia mamlaka walizopewa na wananchi kuwanyima haki wananchi?

Mheshimiwa Spika, kipengele cha tano, kifungu hicho cha madhumuni, kinachosema uwazi na uwajibikaji katika masuala ya umma. Hapa tunaomba kama Serikali ilivyosaini Azimio hili basi ilitekeleze vizuri. Kambi ya Upinzani, inaamini kuwa kutenda kosa sio kosa bali kurudia kosa ni makusudi, sasa Mikataba iliyowekwa kwa manufaa ya watu binafsi basi wawajibishwe na isijirudie tena.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha nne kuhusu mtazamo wa matumizi ya sheria hii kipengele cha 1(a). Kambi ya Upinzani Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi kuhusu *comissions* za 10% kwenye biashara zinazofanywa na watumishi wa umma na viongozi wa Serikali kulingana na Azimio hili tunaloliridhia.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha nne kipengele cha 1(f) na kifungu cha 11, kipengele 2 na 3 kinachohusu ushawishi katika kutoa maamuzi kwenye utendaji kazi wa watumishi wa umma na Serikali, sheria ya rushwa ipo lakini utekelezaji wake hatujui kwa *PCB* wanajua jinsi *tender* za Idara za Serikali zinavyotolewa na malalamiko ni mengi, mfano ni ule wa *Computer* za Wizara ya Elimu na Utamaduni. Sio hayo tu kandarasi kubwa za wageni ndipo zinapopata kazi na kandarasi za wazawa zikashindwa, kwani *consultants* wana *over* na *under specify* mahitaji ya *tender* na wao ndio wakaguzi wa kazi zenyewe.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri *Consultant* aliyetayarisha *specifications of tender* asihusike katika ukaguzi, ateuliwe *consultant* mwingine kabisa bila ya wale waliofanya kazi kuelewa wakati wa *commissioning* kazi. Hii itasaidia

kupunguza kwa kiasi kikubwa kuondoa mazingira ya rushwa na kununua bidhaa ambazo haziendani na mahitaji yaliyotajwa kwenye *tender document*.

Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri atueleze utekelezaji wake kwani tunaridhia sheria ambazo sisi tunazo ila tunashindwa kuzitumia, je, hizo zingine tutawezaje kuzitumia?

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 7 kipengele cha 5, Kambi ya Upinzani inashauri kuwepo na sheria ya uanzishwaji kwa wapelelezi binafsi (*Private Investigators*) watakaofanya kazi bila ya kuingiliwa na vyombo vya Serikali ambavyo mara zote hushindwa kutoa ushahidi kwa kuingiliwa kiutendaji na wale wanaotuhumiwa. Mfano, akituhumiwa Mheshimiwa Rais, kuwa anakula rushwa, ni chombo gani kitafanya uchunguzi hapa nchini kwetu?

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 10, kipengele cha 1(a) nadhani kifungu hiki naweza kukilinganisha na kile kifungu cha sheria za uchaguzi, *Section 109 of the Elections Act, 1985* kama wote tunavyofahamu siasa zote zinaishia kwenye kufanya uchaguzi ili vyama vikabidhiwe dola kwa ridhaa ya wananchi. Hivyo, kama kuna rushwa imetumika kupata mshindi, basi hata Serikali itakuwa ni ya wala rushwa. Vipengele vidogo vya 109(a) na (c) vinaruhusu rushwa kwenye kugombea nafasi za kisiasa, kwani haitoa mipaka ya matumizi ya pesa kwenye kampeni za uchaguzi. Sheria hii inahalalisha rushwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inauliza ni kwa vipi kiongozi aliyeshinda kwa rushwa ataweza kuzuia na kupigana na rushwa? Kama sheria ya nchi inaruhusu rushwa, hizo nyingine za Kimataifa tutazitekeleza vipi?

Mheshimiwa Spika, Azimio hili la Umoja wa Mataifa kuhusu kuzuia rushwa linahusika na mahusiano kati ya rushwa na aina nyingine za uhalifu, moja kati ya hayo ni uhalifu wa kiuchumi (*economic crime*).

Kambi ya Upinzani inauliza, nchi changa kama yetu inapotokea suala kama ambavyo Kampuni ya nchi ya Malaysia (*IPTL*) inavyotufanyia baada ya kuingia kwenye Mikataba ya kiudanganyifu inayosababisha uchumi na pesa za walipa kodi wa Tanzania kufilisiwa, Umoja wa Mataifa unashiriki vipi kwa hili lenye mazingira ya rushwa?

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 1, Kipengele cha (b): “*To promote, facilitate and support international cooperation and technical assistance in the prevention of and fight against corruption, including in asset recovery.*”

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inadhani huu unaweza kuwa mwanzo mzuri kama kutakuwepo na kanuni au mwongozo wa Azimio hili, kuhusu pesa na mali za rushwa zinazowekwa kwenye mabenki ya nje na wanaoweka na kumiliki mali hizo waangaliwe ni vipi wamewekeza huko wakati mabenki ya nchi zao yapo?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inadhani Mataifa makubwa ndio yanayokumbatia rushwa na kuhamasisha viongozi wa nchi changa kupokea rushwa na

kuwekeza kwenye Mataifa hayo. Mifano ya watumishi wa Serikali kununua mali zisizohamishika kwenye Mataifa yao bila wao kuuliza kipato chao, nadhani Waheshimiwa mifano hiyo tunayo!

Mheshimiwa Spika, mwisho, nashukuru kwa kunisikiliza na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi ya kushiriki katika kuchangia Azimio hili muhimu.

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali kwa jumla kwa juhudi kubwa ambayo inasimamia katika mapambano dhidi ya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sizungumzii hili kwa kubahatisha Mheshimiwa Wilson Masilingi ni mmoja katika Mawaziri ambao huwa wanakutana na Kamati yetu ya Ulinzi na Usalama na taarifa zake zote ambazo huwa anatufikishia juu ya kupambana na rushwa ni taarifa sahihi na tunamuunga mkono asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naishukuru sana Serikali kwa kuleta Mikataba na Maazimio haya ambayo ni Maazimio muhimu kwa Taifa letu na kwa Afrika na dunia kwa jumla. Nalisema hili kwa sababu suala la rushwa ni tatizo kubwa ambalo linaweza kudhoofisha maisha na maendeleo ya wananchi wetu na nchi kwa jumla. Kwa hiyo, Serikali ilivyoleta Azimio hili imeonyesha malengo sahihi katika kuwakomboa wananchi katika kujijengea maisha ambao yatawasaidia kuondokana na unyonge.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mimi nataka niungane na wale wanaosema kwamba kweli rushwa ni adui wa haki, na kwa kweli huwezi kununua haki. Haki anastahili kila mtu kwa mujibu wa sheria na Katiba ya nchi yetu inavyoelekeza. Kwa hiyo, Serikali inapoweka mikakati ya kupambana na rushwa tunastahili kuiunga mkono ili iweze kufanikiwa kwa mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikinukuu katika moja ya Mikataba hii inasema: “Mkataba wa Umoja wa Nchi za Kiafrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa una lengo la kuunganisha juhudi za pamoja katika kupambana na rushwa.” Mimi nataka nipongeze malengo haya makuu.

Mheshimiwa Spika, lakini nina wasiwasi kama mikakati hii itaweza kufanikiwa. Kwa sababu tukiangalia nchi zetu nyingi za Kiafrika ziko katika matatizo ya migogoro mikubwa sana ya kivita sasa hivi na hali ya uchumi wao ni duni sana. Sijui kama tutaweza kufanikiwa katika kufanikisha hili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ningelimwomba kwamba kama Serikali yetu iweze kusimamia umoja katika mabara yetu ya Afrika.

Vile vile tunaitaka Umoja wa Mataifa itusaidie kwa hili kwa sababu bila usalama katika Bara la Afrika hatuwezi kufanikiwa haya malengo ambayo tumeyapanga hapa.

Kwa hiyo, mimi ningetaka kuishauri Serikali ili tuweze kufanikiwa ni kuweza kuhimiza Umoja katika Afrika na kuuomba Umoja wa Mataifa ukatusaidia kuondoa tatizo la umaskini katika Afrika na maradhi na mambo mengine yote yale. Mimi naamini kama Afrika itakuwa salama malengo yote yataweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nichangie nimenukuu hii Ibara 19 Mheshimiwa Waziri ametwambia kwamba: “Mkataba huu unasisitiza ushirikiano wa Kimataifa katika kupambana na rushwa, udhibiti na ufuaji wa fedha chafu.”

Mheshimiwa Spika, nchi inaweza ikapoteza mwelekeo wake wa uchumi kama fedha haramu au fedha bandia zitakuwa zimeenea kwa kiasi kikubwa sana. Sasa hivi katika nchi yetu tunasikia kwamba kuna fedha haramu na baadhi ya fedha hizo nyingi zinatoka katika nchi zetu hizi za Afrika, sasa hili sijui tutaliangalia vipi? Kwa sababu hapa sasa hivi inahitajika nguvu ya pamoja na sasa hivi imeshaanza kuwepo dhana au shutuma kubwa kwamba baadhi ya nchi za Afrika zinashiriki kuingiza fedha chafu katika nchi yetu ya Tanzania na nyingine ni majirani zetu hapa. Kwa hiyo, hili kwa mujibu wa Mikataba hii ningeliomba nchi zetu za Kiafrika tuwe wakweli katika kusimamia na kufanikiwa mipango hii na malengo haya makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa wale raia wa nchi hizi ambao watakatwa kwamba wameingiza fedha haramu kwa nchi nyingine ya Kiafrika wachukuliwe hatua ambazo ni kali ili kuzuia wale wengine wasiweze kushiriki katika mchezo huu ambao hauna maana sana.

Mheshimiwa Spika, katika Maazimio haya tumeelezwa kwamba rushwa tatizo la dunia. Kwa hiyo, kitu ambacho kitakuwa katika dunia kwa kweli kinahitaji mkakati wa pamoja na bila kupata msaada wa Mataifa makubwa hatuwezi kufanikiwa.

Kwa hiyo, kama suala liko hivi tunaomba yale Mataifa yote makubwa yenye uwezo yaweze kutupatia misaada ya dhana na vijana wetu kuweza kwenda kusoma na katika maeneo mengine ili tuweze kufanikisha vita hivi kwa mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeelezwa kwamba ili tuweze kufanikiwa katika mapambano haya tunahitaji mambo yafuatavyo:-

Kuwepo kwa amani katika Bara la Afrika na duniani kwa jumla. Waafrika tuungane kuondoa migogoro ya vita ya wenyewe kwa wenyewe, tuondoe umaskini na maradhi. Hili nalirudia kama mambo manne haya tutayafanyia kazi tutapata mafanikio makubwa. Nadhani kuthibitisha kwamba malengo haya ambayo tumeyakusudia tunaweza kufanikisha.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mkataba huu tunaeleza kwamba Tanzania itaweza kupata tena mali iliyopotea kwa njia za rushwa au njia zisizo halali. Mimi nataka nimwulize Mheshimiwa Waziri, tuseme kama zile fedha zetu zilizoibiwa kwenye Benki

Moshi na nyingine zikatoroshewa Kenya, zitaweza kurudi Tanzania? Je, Mikataba hii inahusisha fedha kama zile?

Lingine, tuseme kama kuna viongozi wa Kiserikali pamoja kwamba katika nchi yetu sisi hakuna shutuma hizo, wamewekeza fedha nyingi katika nchi za nje na Serikali au wananchi wakafanya utafiti na wakajua kwamba kuna fedha yao nyingi sana imetoroshwa nje ya nchi, je, Mikataba hii itaweza kusaidia kurejesha fedha hizo ndani ya nchi? Kuhusu hayo naomba nipatiwe ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, nataka nirudie kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri na nimtakie mafanikio makubwa. Naunga mkono Azimio hili kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nashukuru sana kupata nafasi ya kuchangia katika Maazimio yote haya mawili kwa sababu yanafanana.

Kwanza, kabla sijafanya hivyo juzi juzi hapa tukiwa Bungeni tulijadili sana masuala yaliyokuwa yanahusu kwanza UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wakaonyesha kabisa kabisa kutoridhishwa sana na matangazo ambayo vijana wetu wa kikundi cha *ISHI* walikuwa wanafanya. Kama kawaida yetu ya kuishauri Serikali tukashauriwa kwamba yale matangazo hayafai na hayaendani na maadili ya nchi yetu. Bahati nzuri sana Ofisi ya Waziri Mkuu walielewa jambo hili ambalo tumelipigia kelele muda mrefu kwa sababu kazi ya Bunge ni kushauri.

Wakati wa Kikao cha Bajeti, mimi nilipigia kelele sana na nikapata barua nyingi na simu nyingi sana na hata juzi tulipochangia hapa mtu wa kwanza kutupongeza alikuwa Mheshimiwa Ole Molomet, ni Mkuu wa Wilaya wa Kiteto alinipigia simu na tuliongelea naye kwa muda mrefu juu ya suala hilo. Akasema wanashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wamefikia hatua hiyo na baadaye watu wa Mererani walinipigia simu. Kwa hiyo, inaonekana nchi nzima matendo ya kuiga vitu vya nje katika utamaduni wetu hatutaki. Mheshimiwa Spika, Bunge hili Tukufu lilishauri na Serikali imekubaliana. Kwa hiyo, nataka nipongeze sana hatua ambayo Serikali inachukua kuhusu hivyo vitendo vya usione soo.

Lakini zaidi ya hayo kabla sijachangia hili, ni kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu yeye alisahihisha kabisa katika mazungumzo yake kule Singida akasema siyo usione soo, sema ona soo, kwa maana ametuunga mkono. Tunampongeza sana sana. Nafikiri wanaohusika wataendelea kufanya kazi nzuri kwa ajili ya kuelimisha umma wetu, tusifuate mambo mengine ya miradi, tufuate hilo.

Katika hilo tunaomba sana ndugu yetu Taji Liundi anayehusika na mambo haya nimemsikia leo akizungumza na watu wa *BBC* asiendeleo kubishana na Bunge, Bunge linatoa ushauri, yeye akubaliane kwamba Bunge linatoa ushauri na asiendeleo kubishana Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nichangie kuhusu kuridhia hiyo Mikataba. Kwanza, naunga mkono na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora. Kwanza, amewasilisha Maazimio yote mawili kwa ufasaha sana na kwa kweli kila mmoja ameelewa kipi kinatakiwa kufanyika. Kwa sababu katika ulimwengu wa leo, lazima ufanye kazi kwa pamoja kama makundi ya pamoja. Kama watu wote wanapigia kelele jambo moja maana yake ni kwamba limewakera watu wengi na kwa hiyo, mnaweza mkawa na nguvu za pamoja kutatua matatizo haya kama hasa hili la UKIMWI. Kenya wapige kelele, Uganda wapige kelele, Zambia wapige kelele na baadaye Afrika nzima na baadaye ulimwengu mzima, basi tutafika mahali suala la rushwa nalo pia vilevile tunapiga kelele, nafikiri watu wanaokula rushwa watafika mahali waseme kelele zimezidi tuache kula rushwa.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nina machache ya kuchangia. Kwanza, niseme Mikataba hii tunaridhia tunashukuru, nikaandika ni kwa vipi umoja huu utafanya kazi katika Tanzania, lakini nikapata jibu katika aya iliyofuata kwamba Tanzania itapata manufaa kwa kuendeleza utaratibu wa nchi kwa kuweka sera za kuzuia na kuondoa rushwa nchini. Nikasema labda hapa mambo ya kiufundi na mambo ya misaada, maana tunahitaji misaada ya fedha katika kupambana na rushwa, tunahitaji vyombo mbalimbali, magari na nini, katika hili tunakubaliana kwamba tutahitaji misaada mbalimbali ili kuimarisha Taasisi zinazopambana na Rushwa na kwa kweli hapa tunaunga sana Serikali mkono.

Mheshimiwa Spika, sasa ni vipi tunapambana humu ndani licha ya kupata magari au fedha au nini, nadhani sasa ni suala letu sisi wenyewe Watanzania. Hii nataka niseme kwamba kwa sababu kuna maeneo yanayosababisha rushwa. Ni nafasi tu za watu, mtu anapata nafasi ya kuwa mkubwa mahali fulani na watu wengine wakiwa na hiyo nafasi wanaitumia vizuri sana kwa maana ya maendeleo ya nchi, lakini wengine wanaitumia nafasi hiyo vibaya pale pale.

Mheshimiwa Spika, tumeona watu wametumia nafasi zao katika kujitajirisha. Leo nimesikia kwenye *BBC* kuna Mbunge mmoja Kenya ameulizwa swali na yule mtangazaji kule, nadhani nao wana suala hili la mambo ya rushwa. Sasa mtangazaji akasema unasemaje, Mbunge akasema kuna Mawaziri wameingia mwaka mmoja na nusu, lakini sasa hivi wana magari ambayo Kenya ni shilingi milioni 18, wamenunua mashamba, wamenunua majumba, sasa yule Mbunge akasema utajiuliza katika *common sense* tu kwamba hivi huyu wa mwaka mmoja na nusu tu ameweza kumiliki vitu vyote hivyo na hizo fedha anazipata wapi? Sasa hayo ndiyo alikuwa anazungumza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema ni nafasi tu hata anaweza kuwa Mbunge, anaweza kuwa Katibu Kata au Mtendaji wa Kata anaweza kuwa mtu yeyote lakini nafasi. Lakini licha ya nafasi cheo ni tofauti na nafasi, lakini cheo nacho kinaweza kuwa ni cheo kikubwa tu, lakini kinatisha watu, watu wanakuja ofisini wanasema tumtazame kwanza kabla hatujaingia tumpoze roho kwanza, hivi vyeo vingine na ukakasi ni vikali, mtu anasema loo bwana unataka kwenda pale bora ungetanguliza



kwanza umpoze kwa chai inatamkwa labda kuhongwa, legeza roho ya mzee na hivi. Cheo fulani kina nguvu yake, kina madaraka na kina mamlaka makubwa.

Kwa hiyo, mtu anaona anaogopa, anataka kupeleka chochote kupoza, mzee kabla hajaongea nae na anaposema mzee siyo mzee ni mtu tu anaweza kuwa mdogo hata kwa umri lakini anaitwa mzee.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo fulani mtu mwingine anawekwa katika eneo ndiyo hiyo tunakwenda hiyo ya *procurement* hiyo mtu mwingine anaambiwa wewe mgavi mambo yote hapa, mgavi wa vifaa vya nchi na hivi uwe wewe unakaa eneo hili. Sasa eneo lingine sisi pale Halmashauri tulimfukuza binti mmoja alikuwa anasaidia mahali fulani sasa wale watu wa utumishi wakienda kutaka kumwona mkubwa mmoja yeye anasema huwezi kumwona nafasi haipo.

Kale kaeneo kale alikokaa akisema nafasi haipo sasa ukitaka ufanye chochote sema vizuri basi watu wengine wakaanza kabla hujamwona unapeleka labda shilingi elfu mbili, elfu tano, wanamwona. Sasa baadaye mkubwa mwenyewe akagundua akasema huyu aondolewe sisi tukamtoa. Lakini kaeneo fulani kamwanya fulani lakini nadhani haiwezi kuwa ngumu sana mimi nikitaka kwenda kumwona Rais bila shaka wale watanipitisha tu. Mtukufu Rais tukiitaka kwenda kumwona.

Lakini kama watakuwepo watu pale mlangoni kwamba ukitaka kumwona Rais lazima kaeneo haka huwezi ni lazima upite, u-*jump the hurdle* basi sasa hapo ndiyo unasema vieneo fulani navyo vina matatizo tunapoweka watu je huyu aliyewekwa hapa anafaa si muda ataanza kupokea vitu kusudi aweze kutoa nafasi ya u-fursa kwa watu hilo nalo ni tatizo.

Kwa hiyo, tatizo lingine la mwanya tu tuna mwanya au watu wakawaida raia wa kawaida kuwa wauwoga tu imekuwa *created* imekuwa hali fulani imeundwa imetengenezwa kiasi kwamba watu wakiona unatatizo wanasema lazima utoe chochote kwanza yaani hali fulani watu wanakuwa waoga wanakuwa wanashindwa kujiamini kwa hiyo wangeweza kusema tu hapa bwana bila hilo jambo fulani haliendi, hapa mradi kumeshaitwa kwa fulani jambo hilo haliendi.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka siku moja nilikuwa nafundisha mahali fulani lakini baadaye na mimi nikawa nafundisha walimu sasa nilikwenda ku-*access*, kufanya *assessment* ya mwanafunzi mmoja pale Iringa kuna shule moja iko juu makorongoni. Sasa nikawa nimekaa, kuna Mwalimu mmoja alielewa mwanafunzi wetu ambaye ni mwanafunzi Mwalimu kila mtoto anayechelewa anachapwa kiboko, sasa mimi nilikuwa nimeenda darasani nimekaa, watoto wakaanza kuingia akaanza kuniogopa labda naweza nikampa alama ndogo kwa sababu anafanya vurugu lazima afanye vizuri katika darasa.

Sasa akachapa wa kwanza, wa pili, wa tatu, lakini mtoto mmoja alikuwa ana bahati, akasimiki akaingia akakaa pembeni alikuwa sugu kidogo, yule anaendelea kuchapa wengine, baada ya muda yule kijana akasema Mwalimu vipi mbona mimi hujanichapa? Mwalimu akaanza kushangaa, nikasema ngoja nione kama Mwalimu atamchapa maana tendo la kuchapwa watoto limekuwa ni *enjoyment*, watu wamezoa

sasa, polisi fulani watakapo kuja ukimwona tu wewe tupia bahasha tu maana yule bwana bila hilo hamwelewani.

Sijui mtu fulani, mtendaji fulani wewe ukimwona tu tupia, sasa kuna kuunda uwoga wa namna fulani mahali fulani na watu wakaanza kuitika tu kufanya vitu hata kama wao hawapendi sasa inatakiwa elimu kubwa sana. Katika hilo na kwa nini watu wanafanya kwa sababu ya uroho tu, uroho wa watu wanataka utajiri, wanataka kutajirika haraka kama yule aliyekuwa anasema na sasa hapo tatizo lake ni athari kwamba kuna athari kubwa sana na ndiyo maana nadhani Mheshimiwa Wilson Masilingi au Serikali wameandaa haya Maazimio na wakieleza vuzuri sana kwamba mambo haya yako katika Afrika na katika ulimwengu mzima ili tuweze kupambana kwa pamoja. Ndiyo maana Serikali inaona na sisi tuingie kwenye mkataba na sema tunaunga mkono.

Kwa hiyo, bila kuwa na *mechanism* nzuri ya kupanga watu kwenye vyeo au kwenye nafasi ya kutoa elimu kwa wale ambao wamekata tamaa, wameshindwa kutojiamini bila kuwa na utaratibu mzuri huo basi haki inaweza isitendeke na kama tunavyojua.

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu kwamba tatizo la rushwa ni kwamba haki inanyimwa na wakati fulani hukumu zinaweza kutolewa kwa mtu mwingine ambazo zinaleta machungu sana hata katika familia. Mtu akapata hukumu ambayo hakustahili na kama anapata hukumu ya kufungwa kifungo cha maisha na pengine hakufanya ila watu wenye fedha wamekwenda wamehonga sasa unaweza kukuta familia nzima wanahuzunika na athari kwa familia au athari kwa jamii kwa sababu mtu mwingine anawekwa bila sababu kwenye hatia na wakati yule aliyetakiwa kufungwa anakuwa hajaenda kufungwa.

Sasa mimi ombi langu kwa Serikali kwanza ni elimu kabisa ya kutosha kabisa kwa watu kwamba hata akikuomba kataa rushwa usitoe na watu wawe na imani kwa sababu mwingine ukisema usitoe sisi Wabunge tunapita unakuta unashitakiwa mambo kama haya kwamba alikuja askari fulani akafanya hivi na hivi unamwambia usimpe lakini ukiondoka anasema utafanya nini bwana Mbunge atakuwa hayupo bora kutoa tu. Wanataka kuhonga watu kwa sababu wanaogopa Mbunge atakuwa hayupo bora kutoa tu sasa elimu ni lazima iingie na watu waelewe kwamba Serikali yao ya Chama Cha Mapinduzi ipo itawasaidia kama watawatoa watawataja watu wanao haribu utaratibu wa nchi yetu.

Lakini tunataka kuipongeza Serikali kwa kweli kwamba jitihada imefanya. Tume ya vyombo mbalimbali vya kuzuia rushwa tumefanya jitihada imebaki sasa tatizo tulilionalo ni hilo suala la mtu binafsi nadhani mzuia rushwa ni roho ya mtu tu ibadilike ile roho ya shetani ya kutaka kula kula tu, kutaka tu, ndiyo ibadilike lakini Serikali kwa kweli jitihada yake imekuwa kubwa na la mwisho katika hili tunaomba sana Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mahakama zetu sisi hatuzilaumu lakini zipo kesi nyingine zikitolewa watu wote wanasema hata mtu wa kawaida anaona hapa hata mimi ningehukumu zipo kesi nyingine kweli zinahitaji sheria yenu Mheshimiwa Wilson Masilingi, ni sheria yenu nyie mnajua wenyewe.

Lakini nyingine hata mtu wa kawaida tu anaona fulani leo anakwenda kufungwa, lakini unasikia hii bado, kesi hii haijaka sawasawa, inapigwa danadana hata haijaka sawasawa, hapa jamani mbona kitu hiki ni *very straight forward*. Hivi mengine tunaomba mtusaidie katika vyombo vyetu vya kutoa sheria sasa hivi watu wanaanza kukata tamaa, imefika mahali wanakukata tamaa kwa kweli sehemu zingine.

Mimi niko kwenye bodi moja, tumeshangaa sana mtu amekwenda kushtaki ile kampuni kabla hata hatujawasilisha majibu yetu kule wameshatoa hukumu ni milioni 55 mnalipa jamani, Hakimu gani anatoa kitu hata hajasikia upande wa pili?

Shilingi milioni hamsini sijui kuna kitu kinaitwa *gurnish order* imetolewa hii *gurnish order* inatolewa namna gani kuiba hela za Serikali jamani hivi hivi watu hao walishatibiwa zamani. Lakini ndiyo *gurnish order*, mimi kule Benki Kuu mkienda kukataa basi nakuja kuwatolea huko huko ninyi wenyewe mkashitakiwe nao wale wanaogopa wanatoa tumeshapoteza shilingi 55 milioni pale *LART*, tumeshapoteza mahali pengine hivi hivi mtu amekaa kwenye kiti tu.

Sasa tunaomba sana Serikali, vyombo vyetu vya kutoa sheria vitumike vizuri na elimu hii kwa wananchi iendele vizuri ili kusudi nchi iweze kujiunga sawasawa kwenye maeneo ambayo tunataka kuridhia mikataba hii vinginevyo tunaipongeza sana Serikali na naunga hoja mkono ni hoja nzuri.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdillahi Namkulala utafuatiwa na Mheshimiwa Ibrahimu Wankanga Marwa na Mheshimiwa Aridi Uledi, jiandae.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza niunge mkono kwa asilimia mia moja ila nina maeneo machache tu yakuchangia.

Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha hiyo hoja alisema kwamba sisi tunayo sheria yetu hapa nchini ya rushwa lakini tutaifanyia marekebisho kidogo ili iendane na huu Mkataba. Sasa mimi nilikuwa naomba wakati wa kufanya marekebisho wa sheria yetu tuliyonayo basi naomba izingatiwe suala la urasimu kwamba ni eneo linaloleta mvuto au changamoto ya kuomba na kutoa rushwa. Urasimu maeneo mengi umezidi mno kwa hivyo mtu unaona heri utoe chochote upate huduma mapema na eneo lingine nnaloomba lizingatiwe ni maamuzi ya Serikali. Maamuzi yanaweza yakawa mazuri lakini kama hayakufananuliwa vizuri watu wanaweza wakashuku kwamba kuna mawingu ya rushwa watu wakaona kumbe Serikali inakataza rushwa yenyewe ndiyo nambari moja kwa hivyo sisi wanatukataza tulate fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba hata na maamuzi, nitatoa mifano michache kwa mfano sina maana kwamba maamuzi haya yanajenga kuwepo na rushwa, natoa mfano kwamba inawezekana watu wakaelewa hivyo. Uamuzi wa kuwatoa Madiwani kwenye *tender* mimi mpaka sasa hivi sielewi kwamba wawepo watendaji tu na muomba rushwa wawili tu basi Diwani asiwepo kuna nini huko.

Kwa hivyo, unaweza ukashuku kwamba labda kuna mawingu hapa ya rushwa na Serikali inatetea kwa nini, inatukataza sisi tu lakini wenyewe wanawekeana maeneo ya rushwa kwa hivyo maamuzi kama hayo nilikuwa naomba katika marekebisho yetu tuyafanye kwamba maamuzi nayo yakitolewa basi ufafanuzi wa ufasaha utolewe mapema ili watu wasielewe kwamba rushwa hii inakatazwa tu lakini watu kama alivyosema Mwalimu Nyerere, kuna watu wanaimba kijamaa katika kucheza wanacheza kibepari.

Lingine la urasimu Idara yetu ya *pension* pale mfano, sisemi kwamba wanaomba rushwa lakini yaani urasimu uliopo pale heri utoe elfu hamsini upate huduma mapema unaweza ukakaa miezi sita pale. Kuna mpiga kura wangu mmoja *pension* yake ilikuwa inapelekwa Rombo, nikamsaidia kufuatilia ikawa inapelekwa kwa makosa kule sasa ikarudi kupelekwa Mtwara. Sasa kulikuwa na *cheque* kule Rombo imechacha nimemsaidia miezi sita, mimi nimenyoosha mikono, yeye mwenyewe ameendelea karibu mwaka na kitu hajapata hela yake ile na amekaa Dar es Salaam miezi miwili anafuatilia suala hilo kwa nini asitoe shilingi 40,000/= wakamharakishia akapata laki mbili zake?

Natoa mifano tu ya kwamba urasimu ukizidi unajenga mianya ya rushwa, sasa katika sheria hii basi suala la urasimu nalo liangaliwe kwamba ni maeneo ya kudai na kuomba rushwa. (*Makofi*)

Mfano wa mwisho tuliomba mkopo Mtwara Vijijini wa pembejeo, mfuko wa pembejeo ukatoa idhini mapema kabla msimu haujaanza kuna *group* la watu niliwapitishia *scout* wamepata fedha wamenunua *sulphur* wamepulizia korosho sasa hivi wanauza. *Group* lililopitia *Exim Bank* mpaka leo hawajapata hela, sasa msimu gani mpaka leo fedha hawajapata?

Sasa urasimu huu na kuchelewesha huduma namna hii kwa nini usitoe laki tatu ili ukapata milioni kumi na mbili zile ukanunua sulphur ukapulizia kirahisi. Ninachozumzia hapa ni kwamba marekebisho ya sheria tutakayoyafanya basi tuzingatie sana na kuweka taratibu za kupunguza urasimu wa kutoa huduma kwa jamii kwa sababu urasimu mtu anaweza akaona atoe chochote apate huduma mapema.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri katika marekebisho ya sheria tuzingatie maeneo kama hayo vinginevyo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante kwa kunisikiliza.

**SPIKA:** Ahansante, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mheshimiwa Aridi Uledi, jiandae na Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, jiandae.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Maazimio mawili ambayo yamewasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, kuzungumzia suala la rushwa sasa hivi kuna mambo ambayo mtu lazima ujiandae nayo kwamba hata kwenye muziki kuna miziki inaitwa imepitwa na wakati, inaitwa zilipendwa. Sasa suala la rushwa tumeliongea kwa muda mrefu awamu ya kwanza, utawala wa nchi hii wamezungumzia rushwa, awamu ya pili, imezungumzia rushwa na awamu ya tatu, tunaendelea kuzungumzia rushwa.

Mheshimiwa Spika, suala ambalo linanitua wasiwasi ni pale ambapo tunadhani hatuhitaji kuendelea kujadili na kusikiliza majadiliano yanayotolewa na wananchi kuhusu tatizo la rushwa kwenye nchi yetu. Sasa mimi nilidhani Serikali ingeacha, ingetoa nafasi wananchi wakajadili rushwa na Serikali isijipime yenyewe kwa kusema rushwa imepungua au imekwisha. Wananchi wataona kwamba nadhani sasa Serikali imefika mahali imechukua hatua za kutosha na dalili au hali ya malalamiko ya wananchi kuhusu tatizo la rushwa imepungua.

Sasa wakati wa kikao cha Bajeti mwaka huu Wabunge walizungumza kwa uchungu sana kuhusu tatizo la rushwa kwenye nchi yetu na Serikali baada ya kubaini hilo Waziri mwenye dhamana ya Utawala Bora akaja na kauli ya Serikali kuzimisha mjadala huu wa tatizo la rushwa kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa kama wananchi wanazungumza kwamba kuna tatizo la rushwa na anaye lalamikiwa ni Serikali nadhani kusikiliza pia ni sehemu ya busara ya Serikali kwamba wananchi wanalalamika tuna tatizo la rushwa. Sasa Serikali ni wajibu wake kujitizama na kujiangalia kwamba je, tunavyosemwa sisi kwamba bado hatujafanya kazi ya kutosha kupambana na rushwa tufanye nini lakini si sahihi na si busara kwa kweli kufika mahali na kuwakatisha tamaa wananchi kwamba wasiendeleo na mjadala wa suala hili la mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, mimi wakati wa Kikao cha Bajeti nilizungumza matatizo ambayo mimi nilitaka kusaidia Serikali kuhusu eneo ambalo lilikuwa na tatizo la rushwa na ushahidi ukiwepo. Baada ya kikao kile cha Bajeti nililetewa taarifa kwamba kazi ile imefanyika na nitapewa taarifa, leo ni mwezi wa kumi na moja zaidi ya miezi minne hiyo taarifa sijapata, sijui nini kinaendelea. Sasa nikiwa kama mwakilishi wa wananchi hiyo ndiyo *speed* ambayo ipo katika utekelezaji wa masuala haya.

Mheshimiwa Spika, tutaisaidia vipi Serikali kupambana na rushwa kama hata sisi ambao ni wawakilishi wa wananchi tukichukua hatua kama hizo bado hatua za Serikali zinakuwa taratibu na wakati mwingine hakuna taarifa tunayopewa? Kwa hiyo, mimi nasema bado Serikali ina wajibu wa kuongeza kasi ya kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu siyo malaika na kwa sababu siyo malaika hatuwezi tukajiamini tukaimba nyimbo za chereko chereko kwamba sisi tuko wasafi, hapana. Tuangalie Kenya waliokuwa kwenye Serikali leo ndiyo wako kwenye tuhuma kubwa kabisa kwenye rushwa. Sasa leo sisi tuko kwenye madaraka sawa tunaweza kutizamana tukaimba chereko chereko kwa sababu tuko kwenye madaraka lakini haimaanishi kwamba sisi ni wasafi na kwa maana hiyo tuwazuie wananchi pia wasitunyooshee vidole wakati wanaona dalili za rushwa zipo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi ni matumaini yangu kwamba Serikali itachukua hatua na bado itapokea mawazo yaliyo mazuri ili iweze kusaidiwa na wananchi wenye nia njema ya kupambana na rushwa. Nina hakika mtani wangu Waziri mwenye dhamana hii ya kusimamia Utawala Bora hatasimama tena kama alivyofanya wakati wa Bajeti na kutoa tamko lingine kwamba jamani kwa majina jamani tunafanya kazi hii hapana nadhani sasa tutasaidiana nae kwa sababu yuko *serious*, kwa hili tutasaidiana nae na tuweze kuhakikisha kwamba kazi ya kupambana na rushwa inakuwa kazi ya wananchi wote wa Tanzania na si kazi yakikundi au taasisi ya *PCB* peke yake.

Mheshimiwa Spika, mimi hoja hii ilivyokuja hapa nimesema ni hoja nzuri ya kuleta maazimio haya mawili katika Bunge letu hili na sisi tuwe sehemu ya mfumo ambao wenzetu tayari wamekwisha upitisha. Lakini nasema bado tuna kazi kubwa, mimi nasema sina wasiwasi na utendaji kazi wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa, lakini wasiwasi wangu ni muundo wa hii taasisi kwamba taasisi hii iko chini ya Ofisi ya Rais, nimelizungumza hili si leo zaidi ya miaka mitatu nalizungumza.

Mimi nasema hii taasisi ingeachwa iwe huru, Mheshimiwa Rais anaweza akateua Mtendaji Mkuu wa taasisi hii lakini baadaye taasisi hii ikaachiwa ikajiendesha kwa uhuru zaidi kuliko ambavyo ilivyo sasa hivi. Kwa sababu nina hakika kabisa kwamba kama kutakuwa na watu ambao wanatuhumiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa ambao ni watu walioteuliwa na mamlaka ya Mheshimiwa Rais ni kwamba taasisi hii haiwezi kuwachukulia hatua mpaka ipate kibali hicho cha Mheshimiwa Rais. Sasa mimi nilidhani kwamba taasisi hii ingepewa nafasi ya kufanya kazi zake kwa uhuru zaidi na ikawa taasisi ambayo haiko chini ya Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, hata kama ikiwezekana inaweza ikawajibika pia kwa Bunge maana Bunge si ndiyo linawawakilisha wananchi basi ikawajibika kwa Bunge na ikatuwezesha sisi kujua na kuihoji hiyo taasisi kwamba mbona tunadhani kuna hili na hili mbona hatua za dhati hazichukuliwi. Lakini kwa muundo ulioko sasa hivi mimi nina wasiwasi kwamba hatua za dhati kwa wale ambao wako chunguni, kwenye chungu, ndani ya chungu zinaweza zisichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, la tatu ambalo ningependa kulizungumzia ni suala zima la matumizi ya fedha kwenye chaguzi mbalimbali. Mimi nadhani hapa ndiyo mahali ambapo taasisi wangefanya kazi ya kutosha kwamba zinapojitokeza chaguzi mbalimbali, taasisi ingejikita kwenye maeneo ya uchaguzi kuhakikisha kwamba fedha hazitumiki katika kupata viongozi kwenye chaguzi zetu. (*Makofi*)

Kuanzia kwenye ngazi ya Vitongoji, Vijiji, Mitaa, Kata na kwenye Ubunge na nafasi zinginezo. Kwa sababu tatizo ambalo linaweza kujitokeza kama hali hii ya matumizi ya fedha katika kupata viongozi itaendelea kuwepo uwezekano wa hao viongozi kuwa ni sehemu ya uimarishaji wa rushwa itakuwa ni kubwa sana na hilo kwa kweli litatuletea matatizo huko mbele.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri kwamba katika maeneo ambayo kwa kweli taasisi wangepanfanyia kazi moja ya maeneo ni kwenye maeneo ya chaguzi na nilidhani kama Serikali ingeweza, ingetenga fedha za kutosha kuanzia sasa na huko tunakoelekea kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, chaguzi za Wabunge na uchaguzi wa Rais, kuhakikisha kwamba taasisi inapata nyezo, inapata fedha za kutosha ili waweze kuhakikisha kwamba chaguzi zitakuwa ni za huru na hazifanyiki kwa wagombea kutumia fedha ili waweze kuchaguliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani Maazimio haya ni mazuri lakini ambacho nilikuwa naomba ni kwamba ningependa taasisi basi hata wale ambao wanaonyesha dalili ya kusaidiana nao *either* kwa kutoa taarifa basi na wao wapewe taarifa kwamba nini kinachofanyika baada ya uchuguzi wa taasisi kuwa umefanyika. Maana tunachohitaji kwamba kuna Watanzania ambao wana nia ya kuisaidia taasisi kwa kutoa taarifa lakini kama wanatoa taarifa na taarifa zile zinachelewa kufanyiwa kazi au zinapofanyiwa kazi wale watoaji taarifa hapewi *feedback* ya nini ambacho kimefanyika nadhani pia inawakatisha wananchi wetu tamaa kuweza kushirikiana na hiki chombo kwa hiyo, nilidhani ni vyema basi hawa wanaotoa taarifa kwenye taasisi pia wapewe *feedback* ya kazi ambayo itakuwa imefanywa na taasisi kulinga na hizo taarifa ambazo wanazitoa kwa taasisi.

Mheshimiwa Spika, mimi niseme tu naunga mkono hiyo hoja iliyoko mbele yetu lakini cha msingi zaidi na msisitizo ningependa niuweke ni kwamba tupunguze maneno, tufanye kazi ya dhati kupambana na rushwa. Kwa sababu tungependa kuona hatua zinachukuliwa na wananchi warejeshe imani kwamba taasisi inafanya kazi yake na mimi nadhani ni vyema basi hata taasisi kama kuna matatizo ya msingi kupitia kwenye Kamati zetu za Bunge ikiwepo Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, wakaeleza matatizo ambayo wanakabiliana nayo katika kufanya kazi zao ili angalau sisi kama Bunge pia tusaidie taasisi pale ambapo tunadhani inaweza kuwa na matatizo ya kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono Maazimio yote mawili, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Wamebaki wasemaji wawili tu kwa hiyo, tunakwenda haraka kuliko tulivyokuwa tumepanga lakini hata hivyo nilipanga na kumfahamisha Mheshimiwa Waziri mwenye hoja ya Muswada kwamba yeye ajaandae kuwasilisha Muswada wake kipindi cha mchana. Nilidhani kipindi chote cha asubuhi kitatumika kwenye hoja hii, kwa hiyo, wamebaki wasemaji wawili lakini hata hivyo watakapomalizika na mtoa hoja kujibu hoja zake itabidi Bunge lipumzike mpaka hiyo saa kumi.

Waheshimiwa Wabunge, sasa baada ya maelezo hayo kabla Mheshimiwa Aridi Uledi, hujaanza namwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Makinda, anipokee ili mimi nikazungumze na mgeni niliyemtambulisha asubuhi.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia kiti.*

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Nchi za Afrika kuhusu kuzuia na kupambana na rushwa yaani *African Union Convention of Preventing and Combating Corruption 2003*.

Vile vile Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kuzuia na kupambana na rushwa yaani *The United Nationals Convention Against Corruption 2003*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi ya awali kwa kuipongeza Serikali kwa kuleta Maazimio haya mbele ya Bunge hili ili yaridhiwe. Hivyo nimpongeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora na timu yake kwa mawasilisho mazuri ya Maazimio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa ni adui wa haki na ni kero kubwa mijini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia Serikali ikichukua mikakati mbalimbali katika kuzuia rushwa na lazima niseme hapa kwa mikakati hii imekuwa inaonekana zaidi mijini kuliko vijijini. Kwa hiyo, tatizo hili kuliacha ni kubwa kwenye maeneo ya vijiji maeneo ambayo yana watu wengi kwa hiyo, kuathiri watu hao wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika wakati ambapo wananchi wa vijijini wamejikuta wakikosa haki zao. Wakienda kwenye zahanati wanaodaiwa rushwa, wakienda ofisini wanadaiwa rushwa, wakienda polisi wanadaiwa rushwa wakienda Mahakamani wanaodaiwa rushwa na sasa hata pale wanapotaka kugombea nafasi mbalimbali kwenye chaguzi mbalimbali wanajikuta wakidaiwa rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wengi wanakosa haki zao aidha za kugombea au za kupata huduma kwenye maeneo hayo ambayo nimeyaeleza kwa kushindwa kutoa rushwa.

Kwa hiyo, ni suala ambalo nyeti huko vijijini na mimi ningeiomba Serikali ikabuni mbinu maalum ya kupambana na rushwa kwenye ngazi za vijiji lakini vilevile kwenye ngazi za vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la rushwa huko vijijini limepelekea hata pale ambapo Serikali inapopeleka misaada kwa mfano ya chakula sehemu zingine chakula hicho mwananchi hawezi akakipata mpaka atoe rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huyu ni mtu ambaye ana shida, ana njaa, bado analazimishwa atoe rushwa ili kupata msaada, anastahili kwa hiyo, hapa tunaona ni jinsi gani suala hili linavyowaathiri wananchi ambao kwa kweli hawana kitu, wananchi ambao wanahitaji kila msaada ili kuendesha maisha yao.



Kwa hiyo, ningependa kusesitiza kwa vijijini Serikali ikabuni mkakati maalum kwa sababu maofisa wa kuzuia rushwa tulionao sana sana wanaonekana mijini wapo kwenye Miji Mikuu ya Mikoa, lakini vile vile kwenye Miji Mikuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kule vijijini maafisa hao hawapo. Sana sana labda wanatembelea kwa nyakati fulani fulani. Lakini tunachohitaji ni kwamba Maafisa hao wawepo kule kwa muda wote hivyo kuhitaji Maafisa wa Kuzuia Rushwa kwenye ngazi za vijiji ili wananchi wawaone lakini vile vile wawapelekee shida zao zinazotokana na rushwa.

Kwa hiyo, ningeiomba Serikali basi kubuni utaratibu ambao Maafisa wa Kuzuia Rushwa watakuwepo kwenye ngazi za chini kwa saa zote 24 na sio kutembelea kwa nyakati fulani fulani kitu ambacho hakisaidii sana katika kuzuia rushwa kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kabisa ikiwa suala hili tunataka lionekane kuwa linapigwa vita, tungeanza kwenye ngazi hizi za chini ambako wananchi ambao hawana uwezo wanalazimishwa kutoa hata kile kidogo walichonacho, lakini hivi leo wengine wanakosa zile haki ambazo wanastahili kupata. Sasa ni juu ya Serikali tukawasaidia wananchi hawa ili angalau waone kuwa suala hili la rushwa Serikali imelivalia njuga kweli kweli. Haiwezekani tukakazania mijini na kutokana na uelewa wa watu wa mijini mimi nina hakika kabisa watu wa mijini wanaelewa vizuri zaidi na wanaweza wakapambana na suala hili la rushwa kuliko watu wa vijijini.

Kwa hiyo, hapa ningeiomba vile vile Serikali ikachukua hatua za kutoa elimu vijijini kwa wananchi wote ili wakaelewa suala la rushwa, lakini vile vile wakahamasisha wananchi kushiriki katika mapambano na rushwa. Nina hakika baada ya kufanya hivyo basi suala la rushwa litakuwa limepungua sana nchini na wananchi walio wengi wataondokana na adha ya kukosa haki zao hivyo kujihakikishia wanaishi kwa raha hasa kule vijijini waliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na mchango mdogo sana na mchango wangu ndio huo lakini nasisitiza kuiomba Serikali kuwa wabuni mbinu maalum kwa ajili ya vijijini kwa sababu ndiko waliko wananchi wengi na ndiko ambako wananchi wanapata shida ya kupambana na rushwa, lakini vile vile ya kunyimwa haki zao ambazo ni za msingi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache nikushukuru kwa kunipa nafasi lakini vile vile nimalizie kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini vile vile nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea Mikataba hii inayohusu Vita Dhidi ya Rushwa kutoka katika Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa.

Mimi nina ya jumla ya kuongelea kwanza ambayo niseme tu kwamba la kwanza na mimi niungane moja kwa moja na Msemaji wa Kambi ya Upinzani alipoomba kwamba sasa hivi umefikia wakati kwa kweli wa kuruhusu *Private Investigators*. Hawa *Private Investigators* wanaweza wakafanya kazi binafsi na hawategemei sana *resources* zao, mali za Serikali kwa hiyo, hakuna malalamiko kwamba hatukuwa na gari, karatasi na kadhalika kama tunavyopata wanapojaribu kushughulika na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa vile vile niujiulize tu suala zima la *PCB*. Hivi hawa *PCB* ni wakubwa kiasi gani? Mbona wamekuwa kama siri kubwa sana, watu ambao tunawategemea kutukomboa sisi kutoka kwa wala rushwa wanafichwa kwenye vijumba au maafisi utadhani ni makarani wa kawaida.

Mimi ningedhani katika wakati huu wa uwazi na ukweli na *PCB* wangetakiwa waonekane kama Polisi, kwani kuna tatizo gani? Leo watu wakisema kuna wala rushwa kitu ambacho kila mtu analalamikia wanaambiwa watoe ushahidi. Kwanza hao *PCB* utawaona wapi?

Mheshimiwa Aridi Uledi, amezungumzia kwamba hawa wanaonekana mijini. Mimi nakuhakikishia kwamba hata mijini hawaonekani na hawana alama yoyote hawa. Ukienda Polisi ukitoa taarifa hata kama ni ya uongo inafanyiwa kazi kwanza ndipo inapothibitishwa kwamba ni ya uongo au ni ya kweli na kwa maana hiyo Polisi wanaweza wakaendelea au wasiendeleo kumchukulia hatua yule uliyemtuhumu. Lakini kwa *PCB* wasioonekana sasa tunaambiwa uwalettee ushahidi wewe. Sasa sijui tutautoa wapi? Hawa napenda kusema hawako wazi, hatuwaoni na hii ni moja ya matatizo. Tungependa na wenyewe wawe wazi kama Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nikazie tu suala la Madiwani kuondolewa kwenye *Tender Board*. Kwanza mimi bado naamini na nilisema wakati wa Bajeti kwamba ile ilikuwa ni kinyume cha sheria kwa sababu tulipopitisha Sheria ya *Public Procurement Act, Tender Boards* za Halmashauri hazikuhusishwa na utaratibu ambao sasa umeletwa wa kuwaweka Makarani kusimamia mali. Ni vichekesho kwa sababu wewe mwenye duka hutakiwi hata kujua unanunua nini na unauza kwa bei gani ila yule karani wako ndiyo mithili tunayoiona hapa. Mwenye mali ambaye ni Diwani na ndiyo mwenye duka sasa hatakiwi kujua amenunua gunia la mahindi kwa shilingi ngapi na ataliuza kwa bei gani. Yeye amepangiwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitoe mfano dhahiri kwamba haya mambo yameanza kuonekana. Kwangu kule katika Halmashauri ya Mji Kigoma Ujiji tulikuwa tumetoa kazi za kusafisha mji zilizosimamiwa na Madiwani na mji ulikuwa msafi. Nimerudi safari hii Mji unanuka, watu wanalalamika. Watu waliopewa hiyo *tender* ya kusafisha wengine hata hawajulikani wanaitwa *Texas Investment* wako pale. Mji umechafuka kabisa huu ni ushahidi dhahiri na hata juzi wananchi wameandika kwenye magazeti kuilalamikia Halmashauri yetu kwa sababu wanapewa *tender* na jamaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni dhahiri kwa sababu juzi Mheshimiwa Rais alipokuwa Tabora alipewa taarifa na Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Abbas Kandoro.

Katika taarifa ile Mheshimiwa Kandoro alimfahamisha Rais kwamba kwa Mkoa wa Tabora nadhani na mikoa mingineyo sasa hivi Taasisi zinazoongoza kwa rushwa ni Halmashauri ndiyo ya kwanza ikifuatiwa na Polisi na Mahakama za Mwanzo.

Sasa mimi sijui jambo hili limeanza lini Halmashauri kuwa ndio mstari wa mbele kwa rushwa katika eneo la Mkoa mzima. Lakini amemwambia Rais na nimesoma hiyo. Sasa mimi nasema hili jambo tuliangalie upya na mimi bado nasema ni kuvunja sheria kuwaondoa wenye mali kuwaweka makarani halafu tunaanza kuona vituko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa niliongelee kijumla jumla ni suala zima la Sheria ya Makampuni. Hakuna wizi mkubwa unaofanyika hapa kirushwa na kila kitu kama kupitia Makampuni binafsi. Sina hata uhakika kama yule msimamizi au mwandikishaji wa makampuni ana kitengo cha kuchunguza hata hao anaowaandikisha kama makampuni.

Tumeangalia hapa mara nyingi Kampuni hiyo hiyo imekufa mwezi wa pili, mwezi wa sita inapokea *cheque* na *cheque* ina-clear Benki na *cheque* nyingine zimeandikwa na Serikali. Mtu huyu amepewa leo *tender* ya shilingi bilioni moja atengeneze vitu fulani vya Serikali baada ya miezi mitatu anatangaza *bankrupt*, kesho kutwa anaibuka na Kampuni nyingine anapewa *tender* tena na Wizara nyingine za Serikali na ile ya Ofisi ya Msajili wa Makampuni iko pale na wala haijali na wale watu wanajulikana kwa majina kwa sababu hawaji kuandika majina ya bandia mimi Dr. Kabourou naandika Kampuni *Bunge Limited*, kesho nachukua fedha sijaamilisha kazi niliyopewa inakufa ile Kampuni inakwenda naandika *Mninga Limited* mimi yule yule kwa jina langu na saina yangu. Hii ni rushwa kubwa sana na ni kitu ambacho kinatuharibia uchumi wetu. Mimi ningesema hilo kwa kweli liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kubwa labda tuzungumzie kifalsafa hili suala la urasimu. Urasimu ni kitu kibaya sana na inasababisha mambo mengi. Kwa kweli nawaunga mkono wote wanaosema urasimu sasa usitishwe.

Kwanza Serikali lazima ikubali kwamba tulikaa hapa na kukawa na sherehe tukafanya na *party* tunasherehekea Wizara zinatiliana Mikataba na wadau, tukapewa na vitabu vya rangi nakwambia. Tukavisoma, tukaambiwa wiki mbili tu kila kitu chako kimekwisha, wiki tatu na kadhalika. Sasa hii mimi ninazo kesi mbili. Kijana wangu wa Kasulu amelisha *TTC* kule shilingi milioni kumi na kitu hajapewa fedha zake sasa hivi ananitafuta mimi na si ajabu hata angenipa rushwa. Ananiambia mzee nisaidie mimi nitakupa hela ya mafuta. Nikamwambia aah, sisi wengine tumeshaumwa na nyoka huku maneno hayo hatuyapendi, ila mimi nitalisema. Kijana huyo anaitwa Maliyataabu. Hajalipwa fedha zake na Wizara ya Elimu Utamaduni na hata kama ile shule yenyewe imethibitisha kwamba huyu kweli alitoa na orodha yote ipo na bei alizotoa, hajalipwa urasimu huo sasa hatujui wanatafuta nini hapo. (*Makofi*)

Mimi sipendi kwa kweli kubishana lakini nasema tuangalie masuala haya kama walivyopendekeza ndugu zangu na mimi niongezee tu mawili matatu. Kuna suala la *sovereignty* nchi kuwa *sovereignty* maana yake ina *power*, ina pesa inakusanya kodi, ina

manunuzi makubwa nje. Juzi juzi katika kupitisha Muswada wa Ugaidi, mimi niliwahi kuulizwa na *BBC*. Aliniuliza huyu Mheshimiwa Balala, Waziri wa Kenya huyu. Akasema Dr. Kabourou, tumesikia kwamba Serikali yenu imepewa dola milioni 160 na Serikali ya Amerika ili mpitisha Muswada wa Ugaidi. Nikamwambia kwamba mimi sijui hayo hebu waulize wenyewe. Mimi sipo huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba katika Mikataba hata kwamba ni kati ya nchi na nchi rushwa inatiliwa wasi wasi vile vile. Lakini leo tunaambiwa hapa Tanzania kwamba Mikataba ya Kibiashara ambayo ni kati ya nchi yetu na mtu au Kampuni ambayo kwa maana nyingine ni mtu vile vile yenyewe ni siri ya Serikali, hailetwi hapa. Lakini nani angejua kwamba katika utandawazi, mfumo wa soko huria *capitalism* ni *standard* kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeyote anayenunua kitu kwa *capitalist* anapewa 10% wala haombi na wala sio rushwa, ni kwamba wewe ukishawapa *cheque* ya shilingi milioni 10 basi utapewa shilingi milioni yako moja. Tena utaletewa huombi wala sio rushwa, hatuwezi kusema Mtanzania amekwenda kuomba rushwa kule anapewa kwa sababu ni *standard practise* ya *capitalism*. Sasa tunafanyeje hapo.

Hii mikataba ya siri ya Serikali maana yake ndiyo hiyo kwamba turuhusu mtu apewe asilimia kumi, wanatoa ni kweli. Kwa hiyo, tungependa katika sheria hiyo inayokwenda kuangaliwa na hili suala la asilimia liwe linaingia katika bei kule, asipewe mtu mmoja kwa maana yake Wizara maana yake ni shilingi bilioni 40 au 50. Kama atafanya manunuzi ya shilingi bilioni 30 huyu mtu atapewa shilingi milioni 300. Sasa mtu anasema mtu huyu alijengaje nyumba, amejenga si mmemruhusu. Bepari anajua nini mimi nikinunua ndege ananipa hela yangu. Sasa ni wapi zinakowekwa hatujui sisi. Lakini tunasema Tanzania hatujawa na sifa ya kuficha hela nje isije ikaanza sasa kwa sababu tumeingia kwenye utandawazi, kitu ambacho kiko wazi. Hii ni kitu ambacho uombi unapewa. Tungependa hilo liangaliwe kwa ukaribu sana kwa sababu tunasema kama hiki tunachokiona sasa hivi ni mkataba kati ya Serikali yetu na Serikali nyingine za Umoja wa Afrika, Umoja wa Mataifa zinaletwa hapa Bungeni. Lakini Mkataba kati ya Serikali yetu na Bulyanhulu sijui hapana hiyo ni siri hatuelewi. Labda isiletwe hapa ikajadiliwa. Labda ipelekwe kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi wajadili kule waje kutuletea taarifa kuna ubaya gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kweli nazidi kusema kwamba suala la mikataba ni muhimu sana na ni ukweli tu usiofichika kwamba walio wengi hapa Tanzania kwa kweli ni watu maskini hata kama angekuwa Waziri hata angekuwa nani, wengi wao hawana fedha. Hakuna mwenye dola milioni mia moja hapa na angekuwa nazo ingekuwa vurugu kubwa sana na asingekuwa kwenye nafasi yoyote ya Kiserikali. Kwa hiyo temptation zipo sasa tusiziruhusu zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu la mwisho kabisa imezungumziwa uchaguzi hapa kwamba tuzuie matumizi ya uchaguzi na kadhalika. Mimi nakubali lakini bado narudi pale pale vile vile kwamba katika kesi zote za uchaguzi zinazoamuliwa hapa Tanzania kila siku kuna malalamiko ya rushwa. Kila aliyeshindwa anajua mwenziwe

alitoa rushwa kwa Jaji. Hata mimi niliambiwa nilitoa rushwa. Walisema nilitoa shilingi milioni tano, uongo mkubwa. Lakini hata kama ni uongo ndio *perception* ya watu kwa sababu ya watu na kwa nini? Kwa sababu sisi kama tulivyosema tangu mwanzo Wabunge wanachaguliwa na watu 30,000 au 40,000 unakuja kuhukumiwa na Jaji mmoja amekaa pale hana hata wazee wa Baraza. Sasa tuhuma kama hizi zinaweza kuwa kweli zinaweza zisiwe kweli. Tufanye mabadiliko vile vile kwenye sheria ya Uchaguzi, sio tu kudhibiti pesa itakayotumika wakati wa Uchaguzi, lakini vile vile tudhibiti matokeo ya Uchaguzi. Kwa sababu kwa watu kuendelea kufikiria kwamba Majaji wanakula rushwa katika kesi za Uchaguzi ni dosari vile vile kwa nchi yetu.

Mimi ningefikiri sheria ile vile vile ingewekewa wazee wa Baraza. Kama hata mwizi wa kuku tu anahukumiwa mbele ya wazee wa Baraza saba wanane wajiridhishe kwamba hakuiba huyu Mbunge ana kosa gani. Unakuja kuzuliwa neno lolote pale. Wazee wa Baraza wanaweza kusema hapana hilo analosema kuhusu kijana huyu si kweli na akamwambia Jaji mgeni katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa sasa nafikiri niishie hapo na niishikuru sana Serikali kwa kukubali hii Mikataba kuhusu rushwa na nitoe taarifa kwamba hata sisi Wabunge katika Bunge la Afrika tumepitisha Azimio kwamba Wabunge wote wa Afrika wajiunge na chama ambacho kinapambana na rushwa katika nchi zao. Nadhani hili ni suala zito na tunashukuru kwamba Serikali yetu inaliona hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa dhati kwa kunipatia nafasi kusimamia tena kutolea ufafanuzi mambo mbalimbali ambayo yamechangiwa katika kuunga mkono kuridhiwa kwa Mikataba ambayo punde tu nimeiwasilisha mbele ya Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru Mheshimiwa Kapteni John Chilligati, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kunisaidia katika kufuatilia mjadala wa mazungumzo katika Bunge hili. Huwa ananisaidia mara nyingi na ninamheshimu kwa hilo na nitaendelea kushirikiana naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwataje walioweza kuzungumza wa mdomo kwa kifupi sio wengi. Wa kwanza ni Mheshimiwa George Lubeleje, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, wa pili ni Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou na mmoja kwa maandishi Mheshimiwa Remidius Kissasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliopata fursa ya kuchangia kwa sababu wote wameunga mkono uamuzi wa Serikali wa kuleta Maazimio yote haya mawili ya Umoja wa Afrika Katika Kupambana na Rushwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kuzuia Kupambana na Rushwa.

Nikianza na Mheshimiwa George Lubeleje, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ameeleza Kamati kuunga mkono hoja ya Serikali tunashukuru kwa pongezi alizotupatia kwa ushirikiano tunaupata kutoka kwao na ushauri ambao umetolewa na Kamati tunauzingatia. Wameshauri kwamba ni vyema katika ushirikiano wa Afrika na Umoja wa Mataifa nchi zote za dunia yetu hii katika kukabiliana na tatizo la rushwa, kuangalia namna ya kukabiliana na tatizo la umaskini ambayo unachangia katika tatizo la rushwa na hili ni suala la uchumi na ni jambo jema na mazungumzo yanaendelea katika nyanja za Kimataifa na ya kuboresha uchumi hasa katika nchi zinazoendelea ni jambo la kutiliwa mkazo tunaliunga mkono.

Pia wamezungumzia Taasisi ya Kuzuia Rushwa kutokuwa huru na kwamba wanaweza wakafungua kesi Mkurugenzi wa uendeshaji mashtaka akaifuta kesi hiyo na kwa hiyo si jambo jema ni jambo la kuangaliwa na kurekebisha. Ndani ya Serikali hatua tunazozichukua ni kuimarisha Taasisi ya Kuzuia Rushwa ili iweze kufanya kazi hiyo bila kutegemea msaada wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Taasisi ya Kuzuia Rushwa jinsi ilivyo haina uwezo wa kutosheleza kuzidi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, ndani ya Serikali tuliona kwa awali vyombo hivi viwili vishirikiane ili kuhakikisha haki inatendeka na usimamizi wa sheria unaendana kwa mujibu wa Katiba. Lengo la kumwezesha Mkurugenzi wa Mwendesha Mashtaka kutumia fursa hiyo vibaya na pengine naye kuchukua rushwa ili kusudi aruke Mamlaka ya Taasisi ya Kuzuia Rushwa. Kadri inavyoimarishwa Taasisi ya Kuzuia Rushwa na mjadala wa Kurekebisha sheria ya kuzuia rushwa kadri unavyoendelea tutaangalia namna bora ya kuimarisha Taasisi ya Kuzuia Rushwa na kuipa uhuru ambao ni wa uendeshaji (*Operational Independence*). Lakini hawawezi kuwa na uhuru wa Utawala kwa sababu wako chini ya Ofisi ya Rais kama mnavyofahamu na vyombo kama hivi dunia nzima viko hivyo haviwezi kuwa huru kama Taasisi huru zilivyokuwa za Kiserikali. Mnahakikisha kuwa chombo chini ya Bunge kinakuwa sio chombo cha Serikali na Bunge linaweza likaunda chombo ambacho ni huru cha kufanya kazi hiyo na Bunge haliwezi kuziwa na Serikali.

Kuhusu mbinu ya fedha chafu, tutaliangalia kwa makini kama tulivyoshauriwa. Tumeshauriwa pia suala la Madiwani kuondolewa kwenye *Tender Board* za Halmashauri za Wilaya limejadiliwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa.

Nia ya Serikali ilikuwa ni kuhakikisha Waheshimiwa Madiwani wasishiriki katika *Tender Board* ili kusudi waweze kusimamia *Tender Board* hizo zinazoundwa na Watendaji. Kwa sababu tuliamini ndani ya Serikali kwamba Madiwani hawawezi kushiriki kwenye tenda ikawa na utata bado wakawa ndio wenyewe wanaifanyia tathmini. Inakuwa ni kama mtu anakuwa jaji kwenye kesi yake mwenyewe. Ni kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge ninyi sio wajumbe wa *Central Tender Board*. *Central Tender Board* inaundwa na wataalam. Hata Mawaziri sio wajumbe wa *Central Tender Board* ya Taifa ili kusudi wakivuruga mambo kule yanakuja kwenye Baraza la Mawaziri tunawadhibiti. Sisi tukivuruga Serikali Bunge mnatudhibiti ndio nia njema. Lakini kwa sababu linajadilika na Waheshimiwa Wabunge mmelitolea maelezo na sisi Serikali tuko

wazi kupata ushauri ambao mtaona unafaa kama hoja zitakuwa nzito dhidi ya malengo na madhumuni ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za kigeni nililipata kweli kwenye Kamati kwamba kuna wengine hawatoi stakabadhi mpaka mwananchi aombe. Na hii sio kwenye Masoko ya Kigeni (*Bureau De Change*) tu bali hata kwenye maduka. Mtu kuuza kitu chochote bila kutoa stakabadhi ni kuvunja sheria. Kwa hiyo, tusaidiane Waheshimiwa Wabunge kuelimisha wananchi wadai risiti kwa sababu mara nyingi wafanyabiashara ni wadanganyifu. Kwa hiyo, hilo tumelipata mapema na nimeshawasiliana na Benki Kuu kwa sababu ndio wanawajibika kusimamia vyombo hivi wawe makini zaidi na kuangalia wanaopewa leseni hizo ni watu waadilifu.

Sekta ya madini kwamba inawezekana inaashiria rushwa kutokana na Mikataba yetu tuliyonayo sasa kutotoa mafao ya kutosha kwa Serikali wakitoa mfano wa mrahaba. Niliieleza Kamati na nilieleza Bunge hili Tukufu kwamba Serikali imeunda timu ya wataalamu kuchambua mwenendo mzima wa uchimbaji wa madini na mauzo ya madini tuone je tunapata stahili yetu au tumeliwa katika mijadala yenyewe au kuna ushauri wowote mwingine kwa sababu hata wataalamu wa Kimataifa wanashiriki katika tathmini hiyo. Kwa hiyo, tutaangalia kuhakikisha kama kuna haja ya kufanya marekebisho.

Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, nawashukuru Kambi ya Upinzani kwa kukubali na kuunga mkono hoja za Serikali na ameomba tutoe ufafanuzi kuhusu maneno yaliyotumika ya utajirisho usiokuwa halali. Ni kweli sheria zetu hazitoshelezi na ndivyo nilivyosema katika kuwasilisha hoja na nimeahidi kwamba iwapo Bunge litaridhia Mkataba huu ni mojawapo ya eneo ambalo tutashirikiana na Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine kuliboresha, kutoa ufafanuzi unaofaa, kuondoa mizunguko ambayo inalalamikiwa sasa hivi ni yupi ametajirika isivyo halali na yupo ana mali inayodhaniwa imepatikana kwa namna ambayo si halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya kisiasa kwa Wagombea Upinzani kubambikwa kesi. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ndiyo alikuwa Naibu ananisaidia, tutafuatilia kwa kweli kama kuna mkakati wa kuwekwa watu ndani watolewe baada ya uchaguzi ni kuvunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uwazi na uwajibikaji ndio tunautekeleza, hili halihitaji ufafanuzi ndiyo sera ya Serikali, Bunge. Tunajitahidi kadri ya uwezo wetu katika sekta zote mambo yaendeshwe kwa uwazi na uwajibikaji na kwa uadilifu wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutenda kosa sio kosa ila kurudia kosa, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi nimemsikiliza asubuhi akijibu maswali, amelitolea maelezo. Hii ni lugha ambayo kweli katika jamii inatumika kwa busara ya kusameheana na kusahau yaliyopita kuganga yajayo, lakini kisheria kosa la kwanza unashughulikiwa isipokuwa adhabu inaweza kuwa kidogo zaidi.

Maelezo ya *commission ten percent*, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, amelizungumzia hili. Sisi kwa mujibu wa sheria zetu mtumishi wa Serikali anapokwenda nje ya nchi kujadiliana Mikataba au kufanya manunuzi haruhusiwi kuchukua asilimia

kumi. Kwa hiyo, asilimia 10 haipaswi kuwa sehemu ya gharama ya manunuzi. Endapo anapewa bila kuomba kama Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, alivyosema anapaswa aitolee maelezo anapofika nyumbani. Tunataka wote wawe waadilifu. Ingawaje ni vigumu wengi kusema kama nimepewa asilimia 10 na kama hukumgundua basi na huyo aliyempa hakusema huna namna ya kumshughulikia. Sasa labda kumbana katika utajiri wa ghafla ghafla unaoshangaza na hiyo ndiyo tunaweza tukaipata baada ya kuchambua hiyo sheria itakayohusiana na utajirisho usio halali.

Kuhusu utekelezaji wa sheria na mikataba, ushauri wa Waheshimiwa Wabunge tutaazingatia. Imerudiwa hizi kompyuta za Wizara ya Elimu na Utamaduni jitihada zimefanyika kurekebisha makosa yanayofanyika na kwa sababu limeshafika ndani ya Serikali sina la kuongeza.

Kuhusu wathamini wataalam mabingwa (*Consultant*), nitachukua ushauri tuliopewa kama kweli ni mchambuzi huyo huyo anayeandaa mradi anayesimama anayofanya manunuzi na ina utata kisheria. Desturi za Kimataifa tatalitaza tuondoe mgongano huo na dalili za rushwa au kwenda isivyo stahili.

Kuhusu *Private Investigators* au wapelelezi binafsi hili jambo linavutia sana nimejaribu kushauriana na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi akasema kwa kadri anavyofahamu hakuna sheria inayoruhusu wapelelezi binafsi. Lakini vile vile na mimi mwanasheria sijui sheria inayowazuia wataalamu wa kumpeleleza binafsi kwa sababu tunaruhusu mtu hata kumkamata muarifu. Unaweza mtu ukamkamata mwarifu na kumfikisha kwenye vyombo vya sheria.

Sasa utamkamataje kabla hujampeleleza? Na kwa sababu ni binafsi unapokaribia kumkamata kwa sababu umempeleka *Private Investigator* lakini kama *Private Investigation for purpose of business* kwa ajili ya biashara ni dhana nzuri kwa sababu nchi za nje wapo. Aanzishe Kampuni, apate leseni na hapo tutaweza kuchuja wale ambao wana ubingwa na hata mapolisi wakistaafu wanaweza wakapata ajira kwenye eneo hili. Ni jambo jema litazungumzwa na tutaliangalia katika kurekebisha sheria zetu.

Mipaka ya matumizi ya fedha kwenye Uchaguzi sio bayana. Hilo kwa kweli naweza kusema na mimi huwa naona ugumu huo. Mara nyingi huwa nasema tumia fedha, shauriana na wataalamu, shauriana na wanasheria kama una mashaka usitoe fedha kabisa lakini ukibanwa Mahakama ndio huwa inaamua ni mipaka ipi iliyovukwa na kukushughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeleza ni kwa vipi hii Mikataba inaweza ikatusaidia kwenye kesi kama *IPTL* kwamba inaonyesha kwenye *IPTL* kuna dalili za rushwa na hii Mikataba inaweza ikasaidiaje. Wale ambao wamefuatilia sana mambo ya *IPTL* kwa karibu na mimi ni mmojawao baada ya kuwa Waziri. Suala la *IPTL* kuhusika na rushwa limefikishwa kwenye chombo cha usuluhishi nchini Uingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi imeendeshwa mashahidi wametolewa, Majaji wamekataa kwamba hakuna rushwa na Serikali yetu ndiyo ilikuwa imepeleka hoja ya rushwa. Sasa tunaheshimu vyombo kama hivi, wakishasema sisi kwa upelelezi wetu na



hizi Kampuni za Kimataifa rushwa hakuna ni dili yenu mme-*negotiate*, mmekubaliana mapungufu yapo kwenye bei ikarekebishwa zikapunguzwa tukaamua kutekeleza kwa taabu sana. Lakini dalili za rushwa sisi Serikali hatuamini tena kuendelea kusema kuna rushwa kwenye *IPTL*. (*Makofi*)

Sasa kama ingekuwepo au ikibainika bado hata kesho kutwa hii mikataba inaweza ikatusaidia kuwabana hayo makampuni ya nje ambayo tunashirikiana nayo katika kuendesha miradi hii kupitia *TANESCO*. Fedha za rushwa katika mabenki ya nje, kama zipo tusaidiane itatusaidia hii mikataba kwa urahisi zaidi hasa kipindi hiki.

Pia Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, tunamshukuru ameunga mkono pia na ameweza kutoa ushauri ambao tunaona ni wa msingi kabisa ameeleza kwamba kwa kweli tukiendelea na migogoro katika Afrika utekelezaji wa mikataba hata huu wa Umoja wa Afrika wa kupambana na kuzuia rushwa hauwezi kutekelezwa. Nakubaliana naye kabisa nchi yenye migogoro haiwezi kufuata utawala wa sheria. Umoja wa Mataifa kusaidia Afrika kurejesha usalama na kuondoa migogoro na kupambana na umaskini ni ushauri ambao tunaouchukua kutoka kwa Mheshimiwa Omar Mjaka Ali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa ufujaji wa fedha kwamba ushirikiano ni muhimu sana. Nakubaliana naye ndiyo maana tunaona ni hoja ya msingi kushirikiana na wenzetu ndani ya Afrika na ndani ya Umoja wa Mataifa kwa sababu fedha chafu mara nyingi zinatoka nje. Siyo kwamba zinaanzia Tanzania kwenda kufuliwa nje mara nyingi zinatoka kwenye nchi zilizoendelea kuja nchi inayoendelea kama Tanzania na kuzifua hapa kwa kuwekeza katika miradi midogo midogo na hatimaye fedha kuonekana ilipatikana kwa njia halali. Tukishirikiana tunaweza tukadhibiti hili, bila ushirikiano hatuna hata uwezo wa kujua kama fedha chafu imeingizwa au hapana. Hatua kali kuchukuliwa kwa watakaobainika ni ushauri mzuri, tutaangalia katika marekebisho ya sheria.

Pia ameuliza je, kurejesha fedha zilizoibiwa Moshi, hii mikataba inaweza ikasaidiaje, kwa sababu tukio la jinai Moshi la wizi lilitokea kabla hatujaridhia na shughuli ya kufuatilia kurejesha fedha hii imeanza kwa kutumia Jeshi la Polisi na ushirikiano tulionao na mikataba iliyopo ya kushughulikia wahalifu katika Afrika Mashariki, sasa hivi tunatumia taratibu za kisheria zilizopo na makubaliano tuliyonayo. Lakini naamini mikataba hii ikishapitishwa na sheria zikaundwa kuiba ni mojawapo ya fedha za jinai ambazo zitakuwa zimetoroshewa nje baada ya kutenda kosa la jinai ndani ya nchi. Halafu imeulizwa kwamba fedha kama imefichwa nje inaweza kurudishwa? Jibu ndiyo inaweza kurudishwa ndiyo malengo ya mashirikiano hayo.

Pia Mheshimiwa rafiki yangu Mheshimiwa Eliachim Simpasa, anaunga mkono, ametoa shukrani kwa Serikali kuzingatia ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa *Chief Whip* alikuwa hayumo ndani, lakini kwa niaba ya Serikali napokea shukrani hizo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali sikivu, mambo haya yanaendeshwa kwa kushauriana na wasimamizi wa nchi, mamlaka ambayo ni hii ya Bunge, ambacho ni chombo cha juu kwa mujibu wa Katiba. (*Makofi*)

Amezungumzia matatizo ya walafi wenye tamaa ya kutajirika haraka haraka na nakubaliana naye mtu kama amepewa nafasi ya uongozi ndiye mwenye nafasi ya kula rushwa ambaye hana nafasi ya uongozi hakuna ambaye anavutiwa hata kumpelekea hela, unampeleka ya nini? Sasa kitu ambacho tunaweza tukasema ni kwamba viongozi wanaopewa nafasi kwa Tanzania tunasema wanafuatiliwa na kujitajirisha kinyume tunafuatilia kwa utaratibu wa Kamishina wa Maadili, Mali alizo nazo na ongezeko lako, kama akidanganya jamii inasaidia, akibainika tunamshughulikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya wanafanya vyao na sikusikiliza *BBC* mimi lakini kama kuna Waziri Kenya kwa mwaka mmoja na nusu ameshapata zaidi ya *Kenyan shillings* milioni 17 maana hapo unazidisha mara 10 ya Tanzania. Sasa huyo tunamwachia Mheshimiwa Mwai Kibaki siwezi kuisemea Kenya. Lakini nataka kukuhakishieni Tanzania hatuna Waziri wa namna hiyo. Kama yupo msisite kusema kwa mamlaka iliyomteua ili kusudi ashughulikiwe. Kwa sababu sisemi Tanzania haiwezi kutokea, lakini sasa tusaidiane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, raia wa kawaida kuwa waoga kutoa taarifa hiyo ni sahihi kabisa. Sisi tunachosema ni kwamba tutumie hata mbinu tulizopitisha ndani ya Bunge hili, kwamba raia siyo lazima ajulikane. Hata karatasi tu isiyo na jina yeye atuambie kuna mambo hapa *PCB* watashughulika nayo na ndiyo lengo la kupeleka taasisi ya kuzuia rushwa mpaka ngazi ya Wilaya. Lengo letu ni kuwa na wengi sana kutosheleza hata mahitaji ya kufika kwenye kata huko. Lakini siyo rahisi, kwa sasa hivi Wilaya sita hazijapata maafisa wa taasisi ya kuzuia rushwa kwa sababu hakuna ofisi na nyumba za kuishi. Lakini tutahakikisha wanafika huko na wataongezwa na tuna lengo la kuwapatia magari ngazi ya Wilaya ili waweze kuzunguka zaidi. Tungefurahi sana kama wangekuwa wamejitosheleza wakati wa uchaguzi wa vitongoji, vijiji na mitaa mwezi huu. Lakini sasa wako wawili, mmoja, Wabunge tunaomba muwaelimishe wananchi watusaidie kutoa taarifa kwa vyombo vilivyopo na hawa vijana wachache waliopo ili tuzuie rushwa kwenye uchaguzi wa vitongoji, vijiji na mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini mwaka kesho Ofisi za Wilaya za Taasisi za Kuzuia Rushwa zitakuwa zimeimarishwa ili zijiingize kwenye uchaguzi na kukabiliana na wagombea dhaifu ambao wanatumia fedha ili wachaguliwe.

Halafu Mheshimiwa Eliachim Simpasa, ameshauri utaratibu mzuri wa kupanga vyeo na kuelimisha umma juu ya tatizo la rushwa. Hili nitaomba kwa sababu yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, watusaidie Serikali kwa ufafanuzi namna ya kutekeleza, linavutia sana ili kusudi tuweze kuepukana na matatizo ya viongozi ambao wanapewa nafasi halafu wanavuruga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa elimu tutaendelea kutoa kwa sababu Taasisi ya Kuzuia Rushwa ina kitengo cha taaluma kwa umma na utafiti na Waheshimiwa Wabunge, mnasaidia tunaamini katika mikutano yenu ya hadhara mnalizingumzia hili na kukemea na kuelimisha jamii iweze kushirikiana katika mikakati tuliyoandaa Serikali kuwasaidia kukabiliana na tatizo la rushwa. Tumejitahidi kwa kweli ingawaje huwezi ukasema tatizo hili limekwisha.

Pia kwamba Mahakama zinatia aibu kweli na wenyewe wanakiri na wameweka utaratibu, Mheshimiwa Jaji Mkuu ameweka utaratibu *case management committees* za ngazi ya Wilaya zifanye kazi. Sasa hivi wameanzisha utaratibu, mtu akipewa kesi anapangiwa na muda wa kuimaliza na hazihamishwi hamishwi tena. Tuwasaidie mahakama kwa sababu si wote ni wachafu. Wamo mahakamu ambao wameshakuwa kama wahanga yaani hata ukisema aache rushwa haachi yaani kwa kufa na kupona.

Kwa hiyo, msipotusaidia kwa kweli hawataisha. Yametokea katika majimbo tunayaona ili kusudi Mkuu wa Wilaya, akishindwa kumshughulikia mtuambie sisi kusudi tumsaidie Mkuu wa Wilaya kumshughulikia huyo Hakimku Mahakama ya Mwanzo au Wilaya ambaye ni mkaidi katika mambo ya rushwa. *(Makofi)*

Halafu Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, ametoa ushauri kwamba katika kufanya marekebisho sheria tuondoa ukiritimba. Ushauri wake kwa kweli ni wa msingi. Isipokuwa taratibu ambazo tumeshakubaliana chini ya mkakati wa kupambana na kuzuia rushwa wa Kitaifa na mpango wake haya aliyoyaeleza ya kuondoa urasimu tayari tumeshaazimia. Bahati nzuri ametoa mifano mizuri ambayo tutafuatilia. Haya ni mapungufu siyo ya sheria, ni mapungufu ya utendaji. Kuwatoa Madiwani kwenye *Tender Board* hatukuwa na lengo la kuwatengenezea chakula watendaji. Hilo naomba nifanue nimetoa sababu zetu nia ilikuwa njema mapendekezo yetu nia ilikuwa njema mapendekezo mengine ya kuboresha tunaweza tukapokea.

Mheshimiwa mwenyekiti, urasimu katika Idara ya *Pension* hili tunaanza nalo leo hii kwa sababu kwa mujibu wa sheria ambayo tumeipitisha ndani ya Bunge hili ambayo utekelezaji wake wa Mfuko wa *Pension* umeanza kutekelezwa Julai. Sasa hivi kupata *pension* ni pale unapostaafu unaletewa taarifa miezi sita kabla, siku ya kuondoka unaondoka na *cheque* na kuna uwezo sasa kwa sababu mfuko umeshakuwa na nguvu wa kubadilisha hata *pension* ya Serikali huko huko yaani *capacity* ikaongezeka, wanaita *actuarial procedures*. Kwa hiyo, kama mtu anachezea Idara ya *Pension* pale hili ni suala la utendaji ni vizuri tutalifuatilia. Mtu anafuatilia miezi sita Mbunge anakata tamaa, mwenyewe mwaka mzima bado tutalijua tatizo ni nini kwa sababu inajenga imani ya rushwa kweli. *(Makofi)*

Kuhusu *Exim Bank* nimeshangaa kuisikia tena, hii siyo benki ya Serikali. Lakini kama tuna mkataba nao inachezea, inazungusha ni jambo la kufuatilia, nimeondoka nalo hili ili kusudi tuweze kuondoa tatizo la urasimu kwenye benki hii. Inawezekana pesa kubaki mle wanatengeneza faida wanaweza wakaweka masharti magumu yasiyo na maana ili mshindwe kukopa wenyewe waendeleo kufaidika na riba. Hilo tutalichunguza ili tuwe na hatua za kuchukua. *(Makofi)*

Halafu Mheshimiwa Ibrahim Marwa, huyu mtani wangu amerejesha mjadala wa Bajeti lakini kwa vile tunafahamiana amesema rafiki yangu asingependa leo niseme na kweli nakubaliana naye watani tunaheshimiana, tutayamaliza nje.

Nataka kumhakikishia kwamba Serikali inashiriki kwenye mjadala wa kuzuia rushwa, haizuii rushwa kujadiliwa. Nilisema na iko kwenye kumbukumbu. Kwa sababu

Serikali inawajibika kwa Bunge na wananchi, kunyamaza kimya wakati mjadala unaendelea, vile vile ni utovu wa nidhamu au kutojali. Hiyo ndiyo ilikuwa nia ya Serikali kutoa kauli na mambo aliyotolea taarifa *PCB* wameniletea ki-note kwamba kazi imeshakamilika na wanaohusika wameshajulishwa isipokuwa taarifa ya kunijulisha mimi nimfahamishe Mbunge ndiyo haijanifikia.

Kwa hiyo, naamini itakuwa imeshafika ofisini maana yake hawa wakishughulika, wanashughulika na waliotajwa kwenye tuhuma au wameshashughulishwa na hatua zilishachukuliwa. Sasa mimi wataniandalia na nitakwenda kumueleza Mheshimiwa Mbunge, naona ametoka nje, najua anapolala nitakwenda kumueleza kwa mdomo halafu nitamueleza kwa maandishi pia. (*Makofi*)

Pia, imezungumziwa kwamba tupunguze maneno, tupambane na rushwa. Kwa kweli maneno hatusemi, ndiyo maana *PCB* wanasema hawaonekani, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, amesema wako wapi hawa hata mjini hawaonekani. Wale vijana hawaonekana lakini wanafanya kazi na Waheshimiwa Wabunge wengi mmewasifu, kwa niaba yao napokea shukrani. (*Makofi*)

Mimi nawaomba vijana wale waongeze kufanya kazi. Sasa ile kujificha kutoonekana ni mbinu zao na hii sijui kama naweza kuisemea kiutalaam maana mimi sijawahi kupeleleza. Lakini wananieleza kwamba mpelelezi hapaswi agundulike kwamba anapeleleza. Lakini yule mkubwa wa Wilaya na Mkoa lazima ajulikane kusudi apokee maneno na kupeleka kwenye mashine yake.

Kwa hiyo, tutahakikisha wale vijana wawaone Wabunge, lazima Mbunge awafahamu ili aweze kumwambia mwananchi wa kawaida huyo. Lakini vile vile kuwajua na ofisi zao zikiwa wazi watu hawataenda kule, maana wala rushwa wengi wakishapokea rushwa, anatuma mtu nenda uangalie anayeingia kwa wale *PCB*. Sasa lazima umfiche mahali ambapo akiwa anaingia kama ni kwa Mkuu wa Mkoa huwezi ukaingia na anakwenda ghorofa ya ngapi. Labda ukimfuatafuata anarudi anapoteza lengo na yeye. Lakini kwenye kajengo kale kila mtu anakwenda watu wataogopa zaidi na zaidi kwenda. (*Makofi/Kicheko*)

Pia Mheshimiwa Aridi Uledi, umenieleza mambo ya kusikitisha tutayafuatilia kama kweli kuna vijiji huko mtu ana njaa halafu anadaiwa rushwa ya kupewa mahindi, kwanza hana hela ya kununua halafu atatoaje rushwa, kwa nini asinunue kule? Hiyo tutaifuatilia kule kijijini kwa sababu huo ni mchezo mchafu sana wa Mkuu wa Wilaya kufuatilia kwa karibu. Hii inatisha, hospitalini, polisi, mahakama kwa sababu Mheshimiwa Mbunge, hawezi kusimama hapa kusema uongo anasema kwa niaba ya wananchi na Wilaya ni Masasi, tutaifuatilia tukomesha haraka sana angalau tuanze na Masasi iwe ni mfano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya makampuni hii ni ya Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, ametoa ushauri mzuri siyo ya mwisho *last but one* kuna Mheshimiwa Remidius Kissassi amesema kuondoa Madiwani kwenye *tender* ni kinyume cha sheria. Si kinyume cha sheria kwa sababu tulikuwa tunatoa kanuni ya usimamizi wa kutekeleza

sheria yenyewe ya Kitaifa. Kwa sababu sheria ya Kitaifa ina nguvu kuliko zile za mitaa. Kwa hiyo, hii ni miongozo ya kuboresha. Sasa kama haifanyi kazi vizuri tutairekebisha kama nilivyoomba mlete ushauri. Huyu aliyepata *tender* ya Mji wa Kigoma ni *a specific case* wahusika wamesikia na sisi tutawakumbusha wachunguze inakuaje mtu asiye na uwezo wa kusafisha mji anapewa na *tender* na mji unanuka. Hiyo ni kushindwa kwa *tender*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya makampuni kweli inasikitisha kama mtu anafuta kampuni leo, kesho kwa kushindwa kutekeleza mkataba na Serikali akasajiliwa tena akapewa *tender* kwenye Serikali hiyo kweli ni rushwa ya mazingira, ingawaje si hakimu tena, lakini huu ni ushahidi ambao tunaweza kutufuatilia kwa Msajili wa Kampuni. Naomba ziorodheshwe rushwa za namna hiyo na tunaweza tukasaidiwa hinds kwa sababu Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, amesema ana majina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali kupewa fedha na Marekani kupitisha sheria ya ugaidi. Nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge mimi nimo ndani ya Serikali si kweli. Si Serikali ya CCM, sisi Serikali ya Marekani inatuheshimu. Serikali ya Marekani inaiheshimu Serikali ya CCM kwa sababu tumekataa kukubaliana na masharti ya Marekani kwa kila jambo. Mojawapo niliwatajia hapa ya *Article 1998* ya kuwaruhusu Wamarekani washughulikie wanajeshi wao wakifanya makosa ya jinai nje ya nchi. Sisi tumekataa kushawishiwa na Marekani kuwaunga mkono. Kwa hiyo, tunajisimamia pamoja na kwamba uchumi wetu hauna nguvu namna hiyo. Hata *millenium challenge account* ambayo mwanzoni walikuwa wamelegalega tumekuwa wakali tukasema utawala bora wa Tanzania ni mfano bora kuliko nchi ambazo mnazihusudu, wamekiri. Sasa tunashirikiana nao waweze kutusaidia *under challenge millenium account*. Kwa hiyo, sisi misimamo yetu na Wamarekani ya kutoyumba kwa sababu maelekezo ya Bunge hili yanalenga hivyo hivyo kwamba tusiyumbe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya asilimia 10 nilishaizungumzia. Naomba kama kuna Mtanzania anapata asilimia 10, anaficha nje baada ya kuridhia azimio hila hela hizi zitarudi haraka sana ndiyo malengo haya. Hatuwezi kujua bila kushirikiana na wenzetu kwenye mambo haya.

Halafu kurekebisha Sheria ya Uchaguzi ili Jaji akae na wazee wa Baraza huu ushauri mimi unanivutia sana na mimi naupenda sana. Majaji wakiwa hata watatu au watano ina nafuu zaidi kuondoa hisia za rushwa, akiwa mmoja kama ulivyoifafanua vizuri Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou.

Nimalizie na Mheshimiwa Remidius Kissassi, ameshauri kwamba watoa huduma wote wa afya, walimu, makarani na maafisa wavae *uniforms* na namba vifuani ili wananchi wawatambue iwapo wanapokea rushwa. Kwenye Wizara ya Afya wameanza, manesi na wahudumu kuvaa vitambulisho vyenye majina angalau mimi nimeshuhudia Muhimbili, sijui Mikoani. Ni jambo ambalo tutalifuatilia.

Halafu imeongelewa kwamba *PCB* na polisi wawe wepesi kufuatilia masuala ya rushwa yanapotolewa kwao, tutafanya hilo. Kwa kweli ndiyo wanavyofanya isipokuwa

kupeleleza katika mazingira ambapo wananchi wengi ni waoga kujitolea kutoa ushauri ni jambo ambalo linasikitisha na ndiyo maana imepelekea Serikali tukatoa wito kwa wananchi kutoa ushahidi kwa nia njema siyo kwa Serikali inavua wajibu wake wa kupeleleza. Sisi wanasiasa tukisimama hata hapa mimi nikasema wananchi watoe taarifa au walete ushahidi na haya maneno sisi tunayatumia *interchangeably* taarifa ushahidi ni kwa nia ya kuwataka wananchi watoe ushirikiano, watoe msaada wa maelezo, vinginevyo kulalamika bila kutoa hatua hiyo, Serikali tunakuwa kwenye hali ngumu, siyo kwamba tunadharau au tunapuuzua vilio vya wananchi. Ni katika kuvishughulikia vilio hivyo kikamilifu kwa sababu tunajua bila kwa kweli kupata taarifa sahihi na ushahidi mahakamani hatutasikilizwa na sisi tukishakamata, usiposhinda Mahakamani Jaji anaweza akaamuru Serikali imfidie huyo mwananchi. Kwa hiyo, ni katika kuchukua tahadhari na tunaomba wananchi waelimishwe hivyo, Serikali haina nia mbaya tunaomba wananchi wajikaze watoe ushahidi bila kutoa utambuzi wao, wasitoe majina yao ili tupate pa kuanzia kufanya upelelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana kwa kuunga mkono Maazimio haya mawili la Afrika la Kuzuia na Kupambana na Rushwa la mwaka 2003 na la Umoja wa Mataifa Kuzuia na Kupambana na Rushwa la mwaka 2003 ili kusudi tuweze kushirikiana na wenzetu kupambana na rushwa ambayo ni ngumu ambayo huwezi kuishinda bila kushirikiana na wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa imeungwa mkono. Sasa kwa sababu haya Maazimio malengo yake yanafanana, lakini yanatokana na maeneo tofauti kwa nitaomba niwahoji Azimio moja baada ya lingine na tuyapitishwe kwa pamoja.

**Azimio la Kuridhia Mkataba wa Umoja wa Afrika kuhusu Kupambana na Rushwa**

**Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa dhidi ya Rushwa**

*(Maazimio mawili ya Kupambana na Rushwa yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Maazimio haya mawili yamepitishwa rasmi kwa pamoja na yataendelea na taratibu zinazohusika. Waheshimiwa Wabunge sasa naahirisha kikao mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 06.48 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 10.00 jioni)*

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Naibu Spika, (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Shughuli za Bandari wa Mwaka 2004 (*The Ports Bill, 2004*)

(Kusomwa Mara ya Pili)

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Shughuli za Bandari wa Mwaka 2004, yaani *The Ports Bill, 2004* kama ulivyoorodheshwa kwenye Orodha ya Shughuli za leo, usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza na kuishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Bunge ya Miundombinu chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo, Mbunge wa Tabora Mjini kwa kuuchambua kwa undani na kwa kina Muswada huu. Naomba niahidi kwamba maoni, maelekezo na ushauri wa Kamati utazingatiwa katika utekelezaji wa sheria itakayotokana na Muswada huu. Katika kipindi cha uhai wake, Kamati imeweza kutembelea Bandari za Dar es Salaam, Mtwara, Tanga, Lindi, Mwanza, Itungi na Kasanga. Nawapongeza na kuwashukuru tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ninaouleta kwenye Bunge lako Tukufu utakusudia kuleta mabadiliko katika umiliki, usimamizi, uendelezaji na utoaji huduma katika Bandari za nchi yetu. Inapendekezwa kiundwe chombo kitakachoitwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania, yaani *The Tanzania Ports Authority* ambayo itakuwa mmiliki, yaani *Landlord* wa Bandari na miundombinu yake katika Bandari zilizopo na zile zitakazoanzishwa. Jukumu kubwa la chombo hiki litakuwa ni kumiliki, kusimamia na kuendeleza Bandari za Mwambao na za Maziwa. Aidha, mapendekezo yaliyomo kwenye Muswada huu yanalenga katika kufanya marekebisho ya utaratibu wa shughuli za kibandari ambazo kwa sasa zinafanywa na Mamlaka ya Bandari Tanzania na Kampuni ya Huduma za Meli yaani *The Marine Services Company Limited* ili kuleta ufanisi katika usimamizi wa Bandari zetu.

Umiliki wa Bandari zilizo chini ya Kampuni ya Huduma za Meli utahamishiwa kwenye Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari. Umiliki na usimamizi wa Bandari ya Kasanga katika Ziwa Tanganyika nao utakuwa chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mamlaka ya Bandari ya Mwaka 1977 ilitungwa miaka 27 iliyopita ili kuweka utaratibu wa kusimamia, kuendesha na kuendeleza Bandari za Mwambao. Hivi sasa kuna mabadiliko makubwa yanayotokea duniani katika Sekta hii.

Sehemu nyingi duniani huduma za Bandari zinatolewa na sekta binafsi ikiwa ni pamoja na mahitaji ya uwekezaji katika vifaa na teknolojia ya kisasa. Bandari zetu ni kiungo muhimu kati yetu na sehemu nyingine duniani. Kwa kuzingatia mabadiliko ya Sekta ya Bandari duniani, sheria sasa imeonekana haikidhi mahitaji ya sasa yanayotokana na mabadiliko hasa katika utoaji huduma.

Aidha, uendelezaji na usimamizi wa Bandari za Maziwa umekuwa hauna msukumo wa kutosha na kwa hakika umekuwa hauna uwiano sambamba na ule wa Bandari za Mwambao. Hivyo, kwa madhumuni ya kuleta uwiano katika uendelezaji wa Bandari zote nchini, Muswada huu unapendekeza kuwe na Mamlaka moja itakayosimamia uendelezaji wa Bandari zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ndogo ya Bandari kama ilivyoainishwa katika Sera ya Uchukuzi, ni kiungo muhimu katika kuendeleza uchumi hususan kutumia nafasi nzuri ya kijiografia nchi yetu iliyobahatika kuwa nayo. Bandari zetu zitaimarishwa na kukuza biashara. Aidha, sekta hii ni kichocheo katika kufanikisha mfumo wa utandawazi na kuongeza ustawi wa jamii. Hivi sasa Bandari zetu zinahitaji uwekezaji, uboreshaji wa mifumo, usimamizi thabiti utakaowezesha kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye.

Kutokana na hali hiyo, Serikali baada ya kushirikisha wadau, imeandaa Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Bandari wa mwaka 2004 (*The Ports Bill, 2004*) ambao una lengo la kutunga sheria mpya yenye kukidhi mahitaji ya sekta pamoja na kutoa fursa kwa sekta binafsi ambapo kwingineko duniani uzoefu umeonyesha kuwa ina uwezo mkubwa wa ujasiriamali, ubunifu na ufanisi katika utoaji wa huduma za kibandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za kutunga sheria hii mpya ni pamoja na:-

- (1) Kutekeleza sera ya Serikali ya kujiondoa katika uendeshaji wa shughuli za kibiashara na kubakia na jukumu la kubuni sera na kusimamia utekelezaji wake na kuiachia Sekta Binafsi jukumu la kutoa huduma.
- (2) Pili, kuwezesha uwekezaji ili kuweza kupata mitaji na teknolojia ya kisasa.
- (3) Kuunda chombo kitakachosimamia pamoja na mambo mengine utoaji huduma na uwekezaji katika Sekta ya Bandari chenye uwezo wa kumiliki, kusimamia na kuendeleza Bandari za Mwambao na zile za Maziwa Makuu.
- (4) Kuwezesha kuwa na uwiano wa uendelezaji wa Bandari na utunzaji wa mazingira.
- (5) Kuboresha masuala ya kiusalama na kiulinzi katika Bandari zetu.
- (6) Kusisitiza umuhimu wa kuitumia bahati tuliyonayo ya jiografia nzuri ya Tanzania katika kuendeleza Taifa na kuhudumia nchi jirani zisizo na Bandari.



Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Serikali kuamua kujitua katika shughuli za biashara, kumekuwa na marekebisho makubwa katika Taasisi zake yenye lengo la kufanikisha utekelezaji wa uamuzi huu. Wajibu wa Serikali unabakia kuwa ni udhibiti kupitia vyombo huru vya udhibiti kama vile *SUMATRA*, Usimamizi na Uhimizaji wa Ujira na Ufanisi wa Huduma zitolewazo au biashara.

Sambamba na marekebisho haya, Serikali itaendelea kubaki na umiliki wa miundombinu. Hivyo basi, mwelekeo huu unahusu pia sekta ndogo ya Bandari.

Aidha, utoaji huduma za Bandari utakuwa mikononi mwa sekta binafsi. Serikali kupitia Mamlaka mpya itaendelea kubaki na umiliki wa miundombinu kupitia Mamlaka hii. Itakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa mazingira ya Bandari yanakuwa safi, salama na yanaruhusu kufanya shughuli za Bandari kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida za msingi zitokanazo na Muswada huu ni pamoja na zifuatazo:-

- (1) Kutakuwa na muundo mpya wa kusimamia utoaji wa huduma na uendelezaji wa Bandari katika mfumo wa 'umiliki wa Bandari' yaani *Landlord*.
- (2) Kuchochea uwekezaji.
- (3) Kuleta mbinu mpya za utendaji kazi na teknolojia mpya ya kisasa na hivyo kuboresha utoaji huduma katika Bandari zetu.
- (4) Kulinda mazingira ya Bandari na kuimarisha ulinzi na usalama wa Bandari.
- (5) Kuchochea ukuaji wa uwiano na uwezo wa shughuli za Bandari zote za Mwambao na za Maziwa Makuu na hivyo kuziweka Bandari zetu katika hali nzuri ya kiushindani na hatimaye kuongeza pato la Taifa kwa ujumla.
- (6) Kuendeleza Bandari za Maziwa Makuu ili ziwe kiungo kati ya Tanzania na nchi za Maziwa Makuu na hivyo kuitumia jioografia yetu kwa faida ya nchi yetu na faida ya majirani zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ufafanuzi huu, naomba kwa muhtasari tu kupitia sehemu hadi sehemu ya Muswada huu wenye sehemu 15 kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza inahusu masuala ya utangulizi, jina la sheria ambayo inapendekezwa kutungwa, eneo la matumizi ya sheria na tafsiri ya maneno ambayo yatatumika kwenye sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya pili inapendekeza kuundwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bandari Tanzania, muundo, majukumu na masuala mengine yanayohusu Mamlaka hiyo. Madhumuni ya kuanzishwa kwa Mamlaka hii ni pamoja na kuweka mfumo wa usimamizi unaofaa katika shughuli za Bandari na kuhakikisha kuwa huduma za Bandari

zinatolewa kwa ufanisi. Mamlaka imepewa uwezo wa kukasimu kazi za kutoa huduma kwa mtoa huduma, yaani *Operator*.

Katika mabadiliko haya, inaundwa Bodi ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia shughuli za Mamlaka za kila siku. Sehemu hii inaazimia kuiwezesha Tanzania kutumia nafasi, bahati na faida iliyonayo kutokana na jiografia kama nchi yenye Ukanda wa Bahari na sehemu kubwa ya Maziwa Makuu barani Afrika.

Sehemu ya tatu inahusu wajibu na majukumu ya Mamlaka. Wajibu huo ni pamoja na jukumu la kutekeleza sera na mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu katika kuendeleza shughuli za Bandari; kuweka na kusimamia Mikataba mbalimbali ya uendeshaji wa shughuli za Bandari. Mamlaka hii pia itakuwa na jukumu la kudhibiti mambo ya kiutawala yanayohusu ardhi na maji ndani ya mipaka ya Bandari.

Aidha, Mamlaka itakuwa na jukumu la kuendesha na kutunza minara ya kuongozea meli iliyo katika maji ya Tanzania yaani *The Tanzania Territorial Waters*.

Sehemu ya nne inahusu mambo ya huduma za Bandari ambazo mtoa huduma atahusika nazo. Huduma za Bandari zitatolewa kuzingatia masharti ya ukodishaji.

Sehemu ya tano inaundwa Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu. Mamlaka itakuwa na Mkurugenzi Mkuu ambaye atakuwa kiongozi katika utawala wa Mamlaka. Vile vile, kutakuwa na Meneja wa Bandari ya Dar es Salaam, Mkuu wa Bandari ya Dar es Salaam na *Harbour Master* kwa Bandari za Tanga, Mtwara na kwa kila Bandari za Maziwa.

Sehemu ya sita inahusu utaratibu utakaotumika kudhibiti usalama katika Bandari za Maziwa na utaratibu wa kuweka viwango vya ushuru mbalimbali.

Sehemu ya saba inahusu uwezo wa Waziri mwenye dhamana ya Bandari katika kutengeneza Kanuni za Uendeshaji na Uongozi wa Bandari, usalama wa meli na uchafuzi wa mazingira. Sehemu hii pia inahusu utaratibu wa kushusha na kupakia abiria na mizigo katika Bandari zetu. Sehemu hii inatambua majukumu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*).

Sehemu ya nane inahusu uwezo na uwajibikaji wa Meneja wa Bandari na Wasaidizi wake.

Sehemu ya tisa inahusu utaratibu utakaotumika kuondoa meli mbovu na chombo chochote kitakachozama kwenye maeneo ya Bandari na kusababisha hatari au kipingamizi kwa watumiaji wengine wa Bandari.

Sehemu hii pia inatoa uwezo kwa Mamlaka kumtaka mtu yeyote anayemiliki chombo kama meli au jahazi au vitu vingine vya aina hiyo kuzuia, kuondoa au kuviharibu vyombo hivyo pale itakapobidi kufanya hivyo kwa ajili ya usalama wa Bandari, watu au vyombo vilivyopo Bandarini na maeneo yake.

Sehemu ya kumi inahusu uwezo wa Mamlaka kutoa maelekezo kuhusu kuingia na kutoka kwa meli katika Bandari, yaani *pilotage* na utaratibu wa kutoa misamaha kwa baadhi ya meli kwa mujibu wa sheria.

Sehemu ya kumi na moja inahusu uwezo wa Mamlaka katika kuongeza kina cha maji, uchimbaji, upanuzi wa Bandari na masuala ya utafiti wa kisayansi katika maji yaliyoko kwenye eneo la Bandari.

Sehemu ya kumi na mbili inahusu vyanzo Vikuu vya mapato vya Mamlaka ambavyo ni pamoja na ada ya ukodishaji, ada ya utunzaji na utoaji mizigo na ada ya huduma za wenye meli. Aidha, sehemu hii inaelezea pia kwamba Mamlaka inaweza kupata ruzuku kutoka Serikali kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu ya Bandari. Sehemu hii vile vile inaelezea dhamana ya Mamlaka katika ulipaji wa mikopo na jinsi ambavyo itakuwa inatunza taarifa za fedha.

Sehemu ya kumi na tatu inahusu uhamishaji wa raslimali na madeni na wafanyakazi. Sheria itakapoanza kutumika, maeneo yote ya Bandari na maeneo mengine yanayomilikiwa, mali yote isiyohamishika, raslimali, uwezo, haki, dhamana na dhima za Mamlaka ya Bandari ya sasa zitahamishiwa kuwa mikononi mwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari.

Aidha, eneo lote la Bandari linalomilikiwa na Kampuni ya Huduma za Meli ikiwa ni pamoja na raslimali zote za kibandari, zitahamishiwa Mamlaka mpya ya Usimamizi wa Bandari.

Vile vile, Muswada unaweka bayana umiliki na usimamizi wa Bandari ya Kasanga katika Ziwa Tanganyika kuwa chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari. (*Makofi*)

Inapendekezwa kwamba kwa kuanzia, ajira ya wafanyakazi wote wa Mamlaka ya Bandari ya sasa iendelezwe chini ya Mamlaka mpya. Baadhi ya wafanyakazi wataendelea na ajira chini ya Mamlaka, wale walio katika vitengo vitakavyokodishwa watalipwa mafao yao na Mamlaka kabla ya ajira kuhamishwa.

Aidha, wafanyakazi wa Kampuni ya Huduma za Meli wanaoshughulika na kazi za kibandari watahamishiwa kwenye Mamlaka mpya. Wafanyakazi wa Kampuni wa Huduma za Meli wenye majukumu yasiyokuwa ya kibandari wataendelea kutoa huduma za meli hadi hapo Kampuni itakapobinafsishwa. Aidha, wafanyakazi wa Kampuni ya Huduma za Meli ambao hawatahamishiwa kwenye Mamlaka mpya ya Bandari na ambao hawataajiriwa na mwekezaji, watalipwa mafao yao na Serikali.

Aidha, kutakuwepo na kipindi cha mpito ili kuiwezesha Kampuni ya Huduma za Meli kuendelea kutumia miundombinu ya Bandari za Maziwa bila malipo hadi hapo Kampuni itakapobinafsishwa.

Sehemu ya kumi na nne inahusu madeni ya Mamlaka, namna ya kushughulikia upotevu na uharibifu wa mali.

Sehemu ya kumi na tano inapendekeza kufuta sheria ya Tanzania *Harbours Authority Act* ya mwaka 1977 na kuruhusu kuendelea kutumika kwa sheria ndogo ndogo. Aidha, mambo ya kiutawala yataendelea kutekelezwa mpaka hapo yatakapofutwa au kuamuliwa vinginevyo kupitia kanuni (*regulations*) zitakazotayarishwa na Waziri mhusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutungwa kwa sheria hii inayopendekezwa kutasababisha yafuatayo:-

- (1) Kufutwa kwa sheria ya Mamlaka ya Bandari ya Mwaka 1977;
- (2) Kuundwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari, yaani *The Tanzania Ports Authority*;
- (3) Kuhamishwa kwa raslimali za kibandari zilizokuwa zinamilikiwa na Kampuni ya Huduma za Meli na kupelekwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari;
- (4) Kuweka Bandari ya Kasanga katika Ziwa Tanganyika chini ya umiliki na usimamizi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari;
- (5) Kuhamisha wafanyakazi wenye shughuli za kibandari wa Kampuni ya Huduma za Meli kwenda kwenye Mamlaka mpya na kuendeleza ajira za wafanyakazi wa Mamlaka ya Bandari chini ya sheria mpya;
- (6) Kutoa fursa kwa sekta binafsi katika utoaji wa huduma za Bandari;
- (7) Kuendana na mabadiliko yanayotokea kote duniani katika biashara ya Bandari;
- (8) Kusimamia kikamilifu ulinzi na usalama wa bandari zetu;
- (9) Kuweka mazingira bora ya usimamizi wa usalama na hifadhi ya mazingira;
- (10) Kuongeza ufanisi na tija na hivyo kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii yetu;
- (11) Kuwa na ajira endelevu ya wafanyakazi na wale ambao hawataajiriwa na Mamlaka kulipwa mafao yao kikamilifu; na
- (12) Kuchochea matumizi ya bahati nzuri ya jiografia nzuri ya Tanzania kwa manufaa ya sasa na vizazi vinavyokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza maudhui ya Muswada huu naomba kuuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu ili uweze kujadiliwa, kukubaliwa na hatimaye kuwa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. DR. AMAN W. A. KABOUROU - (k.n.y. MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ya mwaka 2004, yaani *The Tanzania Ports Authority Bill, 2004*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, ninashukuru kupata fursa hii ya kutoa maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Bandari Tanzania wa mwaka 2004, yaani *Tanzania Ports Authority Bill, 2004*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Miundombinu imeundwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 89. Kwa mujibu wa Kanuni ya 103(b)(1) inasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:- Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa maoni yetu, napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

Wa kwanza ni Mheshimiwa Prof. Mgombelo, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Zamda Bozzan, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Robert Buzuka, Mheshimiwa Bakari S. Faki, Mheshimiwa Abdallah Feruzi, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mheshimiwa Ally Karavina, Mheshimiwa Mohamed Khatib, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Danhi Makanga, Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mheshimiwa Zubeir Maulid, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Karim Othman, Mheshimiwa Sijamini Shaame na Mheshimiwa Maria Watondoha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kufuta Sheria ya Mamlaka ya Bandari ya Mwaka 1977 na *Marine Services Company Cap. 212* ya Mwaka 1997 na kuanzisha Mamlaka mpya ya Usimamizi wa Bandari za Tanzania, kuhamisha raslimali zilizokuwa zinamilikiwa na Kampuni ya Huduma za Meli Tanzania na kwenda katika Mamlaka mpya ya *TPA* na kutoa fursa kwa sekta binafsi katika utoaji

wa huduma za Bandari. Kukidhi matakwa ya mabadiliko ya kibiashara yanayotokea duniani kiteknolojia na kiuchumi katika Sekta ya Bandari na kuongeza ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya ushirikishwaji wa wadau, kwa mujibu wa Kanuni ya 69 kifungu kidogo cha pili cha Kanuni za Bunge Toleo la 2003, Kamati ilisikiliza maoni ya wadau mbalimbali wa Muswada huu, yaani *Public Hearing* tarehe 26 na 27 Oktoba, 2004. Wadau waliunga mkono Muswada kwa kutoa maoni na mapendekezo yao ambayo Kamati imeyazingatia katika marekebisho mbalimbali ya Muswada huu pale ilipoonekana inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati katika Kikao chake cha tarehe 27 Oktoba, 2004 ilipata maelezo ya Muswada wa *Tanzania Ports Authority (TPA) 2004* yaliyotolewa na Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mbunge na Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu madhumuni na sababu za kuwasilisha Muswada wa sheria hii. Baada ya kupata maelezo hayo, Kamati ilijadili kwa undani Muswada huo na kupitia kifungu kwa kifungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutafakari kwa kina na kujadili kwa undani maoni ya wadau na maelezo ya kina yaliyotolewa na Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu hoja mbalimbali zilizotolewa na Wajumbe, Kamati imeridhika na inaunga mkono hatua ya Serikali ya kuleta Muswada huu wa *Tanzania Ports Authority, 2004. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada wa Sheria hii ambao unakidhi mabadiliko yanayoendana na wakati. Muswada unazingatia Sera ya Serikali ya kujiondoa katika kufanya shughuli za biashara na badala yake kuacha zifanywe na sekta binafsi ili kuongeza ufanisi na tija. Hii inatoa fursa kwa Serikali kubaki kama mmiliki wa Bandari na miundombinu yake kwa Bandari zilizopo na zitakazoanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii kwa nia ya kuboresha Muswada huu na kuimarisha utekelezaji wake, Kamati yangu inatoa maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa vile Serikali ilichelewa sana kuanzisha Mamlaka za *SUMATRA, EWRA, TCRA* na kadhalika, Kamati inashauri kuwa maandalizi ya haraka na ya kutosha yafanywe kabla ya kuanzisha *TPA* yaani *Tanzania Ports Authority* ili pasiwe na ucheleweshaji wa utekelezaji wa sheria ya *TPA* kama ilivyotokea kwa sheria nyingine zilizotajwa hapo juu.

Pili, Mheshimiwa Naibu Spika, ili *TPA* iweze kupata mwanzo mzuri na endelevu, Kamati inashauri Serikali iipatie Mamlaka hii fedha za kutosha hususan pale inapopata misaada ya fedha husika bure kutoka Wafadhili wa ndani na nje ya nchi.

Tatu, Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mpito kutoka *THA* kuelekea *TPA*, Kampuni ya Huduma za Meli Tanzania (*Marine Services Company Limited*)

isitozwe kodi katika maegesho ya vyombo vyao vya majini kwa vile hawana uwezo wa kulipia kutokana na kukoma kwa vyanzo vyao vya mapato.

Kuhusu suala la kuzisaidia Bandari ndogo, Kamati inashauri kuwa Muswada uanishe nafasi ya Bandari hizo ambazo zimekuwa zikitumika kwa muda mrefu ili kuepuka adhabu kwa Vituo hivyo. Aidha, Wizara ianzishe Mfuko Maalum wa Maendeleo kwa ajili ya kuzinufaisha Bandari hizo ili ziweze kujiendesha zenyewe na kuendelea kutoa huduma kwa wananchi kama ambavyo wamekuwa wakiitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza kuwa, uwepo mpango madhubuti wa kuzisaidia na kuziendeleza Bandari ambazo zitakosa wawekezaji kwa kuzingatia kuwa baadhi ya maeneo nchini usafirishaji wa mizigo na abiria unategemea sana kuwepo kwa Bandari hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa, katika zoezi la ubinafsishaji wa *THA* na *MSC Limited*, suala la wafanyakazi liangaliwe kwa kina pamoja na maslahi yao na sheria iainishe wazi wazi, mafao yao ili kuondoa utata.

Kamati inasisitiza kuwa suala la mafao ya wafanyakazi wa *THA* lizungumzwe kwenye Mkataba wa Hiari na wafanyakazi waelimishwe kuhusu zoezi hilo ili waweze kuchagua kuendelea au kutoendelea na *TPA*. Kwa wale watakaochagua kutoendelea na *TPA*, basi walipwe mafao yao mara moja. (*Makofi*)

Kamati inashauri kuwa kuwepo utaratibu mzuri katika kulinda maslahi ya wafanyakazi wanaorithiwa na Mamlaka mpya ili wasipoteze mafao yao ya miaka mingi itakapotokea huko walipokwenda wameachishwa kazi.

Serikali iwalipe wafanyakazi hao mafao yao mapema ili yale yaliyojitokeza kwa Mamlaka zilizokuwa chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yasijirudie. Malipo yatolewe mara moja na kwa wakati ili kuepuka kushuka kwa thamani ya Shilingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha zoezi la ubinafsishaji kufanyika kwa amani, utulivu na kuondoa manung'uniko, Kamati inaishauri Serikali kuwashirikisha wafanyakazi husika kupitia Vyama vyao katika hatua zote za maandalizi ya mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kutamka tena kwamba Kamati inaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kifungu cha 43(5)(b)(c) na kile cha 81(1) Toleo la 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha pili cha Muswada kinachohusu mipaka ya kutumika kwa Sheria ya Bandari inatamka kwamba sheria itazihusu Bandari zilizo katika Ukanda wa Bahari, mito na Maziwa katika Tanzania Bara. Lakini katika jedwali la pili limeorodhesha Bandari zitakazohusika na sheria hii na kuziacha nyingine.

Kwa hiyo, Kambi ya Upinzani inashauri kwamba ili Muswada uwe wazi zaidi, basi kiongezwe kipengele kinachoeleza kwamba sheria itazihusu Bandari zote kubwa na zile ndogo ndogo ambazo *TPA* itaona zinastahili kuwa *Ports*, badala ya kutaja baadhi ya Bandari na nyingine zikaachwa. Hii italeta mizozo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria inampa Waziri mamlaka ya kutangaza bandari nyingine yoyote kuwa ni bandari itakayohusika na sheria hii. Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha 3(e) inawanyima wananchi wa maeneo husika haki yao ya msingi ya kudai bandari zao kuendelezwa kama neno *Port* lilivyofafanuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya upinzani inaishauri Serikali kwamba kusiwepo na ridhaa ya Waziri kutamka ipi ni bandari na ipi siyo, bali sheria iwe moja kwa moja inawaruhusu wananchi wa maeneo husika waweze kudai wanachooni ni haki yao kwa mujibu wa Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya upinzani imeshaona jinsi wananchi wa maeneo mbalimbali wanavyokosa haki kwa kuwa Sheria haiwapi wao haki hiyo ila Waziri mwenye dhamana anapewa haki hizo na kuzitoa huwa ni kwa mbinde. Hivyo ni bora kila kitu kuwa wazi, kama ikishindikana basi Mahakama itoe tafsiri na kuwapa wananchi haki wanayoidai kwa mujibu wa Sheria. Lakini baada ya Waziri kutoa ridhaa yake hata Mahakama haitaweza kutoa haki kwani Sheria tayari imempa Waziri haki ya wananchi kitu ambacho ni hatari katika demokrasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria haionyeshi wazi kuwa bandari zitakazokosa mwekezaji ni nani ataziendesha na kuziendeleza. Lakini kwa mujibu wa maelezo ya Serikali zitakuwa chini ya *TPA*. Kambi ya upinzani inataka maelezo kuhusu hilo, kwa sababu historia ya uwekezaji kama inavyoeleweka ni pale penye faida ndipo wawekezaji wanapokimbilia. Nadhani mifano tunajua. Ina maana bandari zenye hasara *TPA* itatakiwa kuziendesha. Maana yake Serikali itaendelea kuzitolea ruzuku bandari hizo. Kwani *TPA* haitakuwa na maeneo yanayozalisha faida. Vitengo vyote vitakuwa vimebinafsishwa au kukodishwa kwa wawekezaji na hivyo mzigo utawarudia walipa kodi. Kwa hali hii ilivyo mamlaka inakuwa kama mpangishaji. Na mpangaji hawezi kulipa zaidi kwa mpangishaji.

Kambi ya upinzani inashauri tunapowekezaji na kukodisha tusirudie makosa yaliyofanyika katika *NASACO* wakati inakufa na watu wakaweka mbele manufaa binafsi badala ya manufaa ya Taifa. Kwa sasa mambo yote ni wazi na hadharani, manufaa ya Taifa na wananchi ndiyo kitu cha kwanza, badala ya manufaa ya binafsi.



Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 5(a) mpaka 5(e) kama ilivyoainishwa kwenye Muswada huu kuhusu azma au makusudio na wajibu wa mamlaka mpya ya bandari bado haipo wazi. Ni kwa vipi jamii inayoizunguka bandari itafaidika zaidi ya maeneo yanayomilikiwa na bandari pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya upinzani inaunga mkono moja kwa moja maoni ya wadau wa kutoka *THA* ya kuongeza vifungu vifuatavyo:-

Kifungu 5(f) kinachosema kwamba: "*Promotion of logistics inter modilism and transport network*" na 5(g), "*Promotion of a port community stake holders that will attract investors in the port industry.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ushindani mkubwa wa kibiashara, bandari na kuwa na ubunifu wa kutengeneza miundombinu ya sehemu zinazopatikana shehena kubwa za bidhaa zinazosafirishwa kwenda nje ya nchi. Kwa njia hii miji mingi yenye bandari inainuka kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya upinzani inashauri kuwepo na kipengele kinachoruhusu pindi uongozi wa Mamlaka ya Bandari utakapoona sehemu yenye bidhaa itakazoweza kuingiza mapato ifanye hivyo bila ya kuwepo na ukiritimba na Manispaa Za Wilaya husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tumeshauri Wizara ya Ushirika na Masoko ijaribu kufanya kazi ya ziada kuona bidhaa zinapata soko nje ya nchi siyo Wizara hiyo tu, bali hata Wizara ya Viwanda na Biashara inaweza kusaidia kupatikana kwa ufanisi wa Mamlaka ya Bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 13 ibara 76 kinachohusu *transfer of employees*. Muswada huu haukuzingatia sheria ya Uajiri, (*Employment Ordinance Cap.366*) Muswada huu unawahamisha wafanyakazi wa *THA* na *MSC* kama vile ni bidhaa, *assets and liabilities*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya upinzani inaona jambo hili kuwa ni la kiuonevu. Kwani mfanyakazi anahiari ya kuajiriwa na mamlaka mpya ya *TPA* au kukataa baada ya kulipwa mafao yake yote kutoka kwa mwajiri wake wa awali. Masharti ya mkataba wa mwajiri mpya ambaye ni *TPA* ni juu ya mfanyakazi kukubali au kukataa na siyo lazima marupurupu yawe juu kulingana na mwajiri wa awali. Hiyo itategemea uwezo wa mwajiri mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada ufanyiwe marekebisho, kuzuia wafanyakazi kurithiwa na Mamlaka ya *TPA* kutoka *THA* na *MSC* bila ridhaa zao na kulipwa mafao yao ya utumishi wa mwajiri wao wa mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi juu ya hayo niliyoyaeleza hapo juu. Baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia machache katika Muswada huu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, mambo yote yaliyotolewa na Mwenyekiti wetu mbele yako Mheshimiwa Naibu Spika, nayaunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wa Wizara hii kwa kutayarisha Muswada huu kwa wakati muafaka. Bila kupoteza muda naunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli sina jipya la kusema zaidi ya yale niliyochangia katika vikao vyetu mbalimbali vya Kamati. Lakini lengo kubwa ni kwamba nataka kukazia hapa na pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia katika kifungu 51(1)(b), Kifungu 58(1) na Kifungu 79 na 80 vinavyohusu wafanyakazi. La kwanza, kifungu 51(1)(b) Muswada unatoa madaraka kwa *SUMATRA* kupanga *rates* na *charges* zitakazotumika na *TPA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona hali hiyo siyo nzuri hasa kwa wakati wa leo, wakati biashara zote, huduma zote zitatolewa na watu binafsi. Hali hiyo ilifaa wakati uchumi ulipomilikiwa na umma. Lakini leo uchumi wetu na huduma mbalimbali zitatolewa na watu binafsi. Kwa hivi kiwe chombo angawaje *SUMATRA* abakie kuwa *regulator* lakini isingekuwa vema ikapewa tena kazi ya kupanga *rates* na *charges*. Kazi hiyo ingefaa ipangwe na *TPA* yenyewe. La pili, juu ya kifungu Na. 58(1) inaelezea majukumu ya *TPA*. Majukumu yake yako mengi, lakini nitaelezea jukumu lile moja la kuendeleza bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli ya kuendeleza bandari, nataka nitoe tahadhari hapa. Kuna bandari nyingi hazifanyi kazi kwa faida, ni bandari chache tu zinafanya kwa faida, bandari ya Tanga, Mtwara, Lindi, Mafia na bandari za Ziwa Nyasa. Kwa hivi katika bandari hizi mwekezaji hatapatikana upesi. Nitoe mfano, bandari ya Ziwa Nyasa. Bandari ya Ziwa Nyasa zinahudumia meli mbili, meli hizo zote ni za muda mrefu, zimechakaa na mara nyingi hugaribika.

Kwa hivi hali ya bandari hizi kwa ujumla hazifanyi kazi kwa faida. Lakini huduma wanazotoa kwa wananchi ni muhimu sana. Kwa hiyo, ieleweke wazi, Serikali ingewekeza kwa *TPA* ili *TPA* ipate uwezo wa kuzihudumia bandari hizo. (*Makofi*)

Kwa mfano, meli zimechakaa, hakuna chelezi ya kutengeneza hizo meli. Meli zikiharibika zinapelekwa Malawi, na mara zote kupata nafasi inakuwa kazi. Kwa hiyo, mara zote meli zinafanya kazi wakati zinahitaji matengenezo. Kwa hivi ni vema Serikali ikawekeza kwenye chelezi ili meli hizo mbili zilizochakaa ziweze kupata mahali pa kutengeneza kwa urahisi isije baadaye zikafanya kazi wakati hazina hadhi mzuri ya kufanya kazi na zikaleta madhara makubwa ya kupoteza mali na maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine juu ya hizo bandari. Bandari ya ziwa hili zote hazina hadhi na kazi kubwa ni kuendeleza hizo bandari. Kwa hivi tungeomba sana *TPA*

iwezeshe, ipewe vifaa iweze kutekeleza majukumu yake vizuri. Lingine linalohusu hali hiyo ni kwamba maeneo yote ya bandari ya Ziwa Nyasa hayajapimwa kwa hivi kunahitajika fedha za kuweza kutumika ili maeneo hayo yaweze kupimwa ili *TPA* iweze kumiliki maeneo yanayoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi mojawapo ya *TPA* ni kuendeleza hizo bandari kuwa kuondoa vikwazo vyovyote vinavyozuia meli kutumia bandari hizo. Kwa hivi, naishauri Serikali iwezeshe *TPA* ili *TPA* iweze kufanya kazi hiyo ya kuondoa vikwazo vinavyozuia meli hizo kutumia bandari kama bandari ya Ndumbi, bandari hii imefanya kazi kwa muda mrefu sana lakini kwa miaka mitano, kumi ya hivi karibuni bandari hiyo haifanyi kazi ni kutokana na hali ya Ziwa Nyasa maji yanajaa kila mwaka ni tofauti kabisa na maziwa mengine. Maziwa mengine maji yanapungua kila mwaka. Lakini Ziwa Nyasa maji yanajaa mwaka hadi mwaka. Mabonde yote ya Ziwa Nyasa yamemezwa na maji. Bonde la Lituhi, bonde la Mbaha, Bonde la Ngumbo na mabonde mengine. Mabonde mengine yanamezwa na maji kila siku. Kwa hiyo, hii bandari ya Ndumbi, mawe yaliyokuwa nje, leo sehemu ile iko majini, yale mawe yanazuia meli kutumia hiyo bandari. Kwa hiyo, ni vema Serikali iwezeshe *TPA* ili iweze kuondoa hivyo vikwazo na bandari hiyo ikatumiwa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kifungu 79 na 80. Kifungu hiki kinahusu wafanyakazi. Nakubaliana na mapendekezo ya Serikali kuwa wafanyakazi wote watakaohamishwa kutoka *THA* na *MSC Limited* kwenda *TPA* hakuna matatizo. Kwa sababu wanatoka Taasisi ya Serikali wanakwenda Taasisi ya Serikali kwa hivi ni vema sina tatizo kwa hilo. Lakini ningependa nichangie jambo moja hapa. Lengo la Sheria hii ni kuiondoa Serikali katika shughuli ya huduma ya bandari ili Vitengo mbalimbali viweze kubinafsishwa. Je, kwa wale wafanyakazi watakaohamishiwa kwa opereta au kwa mwekezaji yoyote nje ya Serikali kwa nini hawa wafanyakazi wasipewe nafasi ya kuchagua alipwe kwanza maslahi yake ya huko nyuma.

Kwa sababu itakuwa siyo vizuri mfanyakazi ametoka *MSC Limited* ama *THA* akahamia kwa mwekezaji binafsi na maslahi yake yote baadaye itaweza kuleta matatizo. Kwa hivi ni vema mfanyakazi kama huyo hata kama huyo mwekezaji atakubali kumwajiri, lakini ingefaa mfanyakazi huyo akapewa nafasi mwenyewe ya kuchagua, kama anataka kulipwa maslahi yake yote ya nyuma aliyofanya kazi *THA* ama *MSC Limited* halafu akaanza upya, mkataba na huyo mwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo machache narudia tena kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru na mimi kwa kunipa nafasi nichangie Muswada uliopo mbele yetu. Naomba nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, ningependa nichangie kwa ufupi sana katika maeneo makubwa mawili. Moja ni kuhusu stahili, mafao na haki za watumishi hawa ambao wapo sasa hivi *THA* ambao wanahamia katika Mamlaka

mpya. Hii ni sababu ya hofu kutokana na matatizo yanayowapata waliokuwa wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao mpaka leo bado wanadai haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri atueleze hasa ukweli, wale wazee wa *THA* kweli wana haki pale au hawana haki? Na kama haki yao ipo kwa nini hawapati. Asilimia zaidi ya 40 watu wale sasa wameshakufa tayari. Lakini bado wanaendelea kudai, wanajaa pale CCM Makao Mkuu siku zote lakini hakuna wanachokiambulia. Sasa waambiwe ukweli kama wanayo haki, haki yao wapewe, kama hawana waambiwe msiondelee kusumbukasumbuka hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kuhusu kile kifungu ambacho kinasema *TPA* ina kazi ya kuendeleza bandari zilizopo. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, namwomba kwa heshima zote kwamba Mamlaka hii mpya basi iturejeshee bandari yetu ya Lindi kama ilivyokuwa pale awali. Bandari ile imeachwa ife na *THA*. Wameikuta ikiwa bandari inafanya kazi. Wanabadilika ikiwa bandari imekufa. Naomba waturudie, siyo waipanue iwe kubwa zaidi, waturudishie iwe na uwezo kama ule wa awali. Nimeongea na Mheshimiwa Naibu Waziri naye alikubali, nusu nusu ya kukubali kwamba nadhani ule uamzi wa kufukia ule uwazi chini ya bandari ndiyo umesababisha bandari kujaa mchanga mara kwa mara. Nilikua naomba Mheshimiwa Waziri mjitahidi bandari ile irudi kama zamani, angalau kama zamani tu, isizidi uwezo ule, tuweze kuendelea kuitumia.

Yapo maswali madogo madogo hivi ambayo hayana nguvu, wanasema Lindi mizigo siyo mingi. Lakini mara nyingi nimesikiliza maswali yanayoulizwa. Hata leo asubuhi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi wakati akijibu maswali kuhusu maombi ya watu mbalimbali wawekewe simu za mkononi Mlalo, lakini hajawahi kuulizia idadi ya *hand set* zilizopo huko, anajibu tu kwamba simu mwezi fulani. Lindi tuwekeeni bandari, mizigo itakuja. Msituambie kwamba mizigo hakuna. Hakuna watu wowote wachukua mizigo kwenda pwani, kule ili bandari ijengwe, wekeni miundombinu, halafu muone kama mizigo itakuja au haikuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo tu. Naunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia mjadala katika Muswada huu. Naomba niseme kimsingi naunga mkono dhana ya kuondoa Serikali katika shughuli za uendeshaji bandari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napata wasi wasi kwa jinsi ambavyo tunatekeleza hili jambo. Ibara ya 4(iii) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaelezea kwamba shughuli za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zitatekelezwa na Mamlaka ambazo zimewekwa na kwa ajili ya shughuli hizo. Ibara hiyo imetamka ni mambo gani katika Tanzania ambayo yanashughulikiwa kama mambo ya Muungano. Ibara ya 4(iii) ya Katiba inasema hayo mambo yapo kwenye Nyongeza ya Kwanza katika Katiba.

Ukiangalia kwenye Nyongeza ya Kwanza, kipengele cha 11 bandari ni jambo la Muungano. Ina maana kwamba liko chini ya mamlaka ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na bandari zote Tanzania kwa mujibu wa ibara ya 4 ya Katiba zinatakiwa ziwe chini ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kinachonipa wasiwasi ni kwamba katika Muswada huu kifungu cha 2(1) kinasema Muswada Sheria hii itahusu bandari tu zilizo Tanzania Bara. *This Act shall apply to sea ports and inland water ways in Mainland Tanzania.* Maana Sheria hii haihusu bandari za Zanzibar na Pemba. Wasi wasi wangu je, katika kutunga Sheria hii hatuvunji ibara ya 4 ya Katiba? Tunayo mamlaka ya kutunga Sheria inayohusu jambo la Muungano na kutangaza litahusu sehemu moja tu ya Muungano? Na kwa nini bandari za Zanzibar na Pemba zisiwe chini ya hii sheria tukawa na *Port's Authority* moja itakayotawala jambo lolote kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nahofia katika kujaribu kuleta Muungano tunaweza tukawa tunajisukuma mbali zaidi na Muungano. Tunafumbia macho mambo machache lakini baadaye yatakuwa makubwa. Kwa sababu tutakuwa na mamlaka mbili za bandari katika Tanzania wakati Katiba Sheria Mama ya nchi hii imeelekeza kwamba mambo ya bandari yashughulikiwe na Serikali moja tu. Na chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, ninaomba wakati Mheshimiwa Waziri atakaposimama ajaribu kuoanisha kifungu cha 2(1) cha huu Muswada na ibara ya 4 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya wasi wasi huo nitasita sana kuunga mkono kifungu cha 2(1) cha huu Muswada. Jambo lingine nilililo na nia ya kulieleza ni kuhusu mamlaka ambayo tunaipa hii mamlaka. Katika Kifungu cha 4 cha huu Muswada. Hii Mamlaka inaundwa kama *individual legal personality* yenye madaraka ya kudai na kudaiwa, yenye madaraka ya kuwa na mali yake yenyewe. Kwa maana kwamba ni nje ya Serikali. Lakini kinachonitisha ni kwamba huyu mtu binafsi ambaye anaundwa anapewa *privileges* ambazo ni tofauti na *privileges* za watu wengine binafsi.

Kwa mfano, kifungu cha 27(1) kinaipa mamlaka *operator* yule mwekezaji, madaraka ya kuuza mali ya mtu kama atakuwa anadaiwa na halipi. Lakini mtu anaweza akasema madai yako siyo sahihi. Sasa ukimpa yule *operator* madaraka ya kusema nakudai, tuseme dola 5,000 wewe unasema hapana. Kwa mujibu wa taratibu ninazojua ni dola 2,000. Yeye akasema basi nina mamlaka ya chini ya kifungu cha 27 nakamata mali yako nauliza. Nafikiri tutakuwa tumekwenda mbali mno. Tutakuwa tumemtunguia sheria ambayo yeye atakuwa ni mdai na yeye atakuwa ni mahakama na yeye atakuwa ni mtekelezaji. Mimi nafikiri wakati ambapo tutakuwa na matatizo juu ya malipo, hayo matatizo yakabidhiwe Mahakama. Siyo yule *operator* awe na mamlaka tu ya kuamua. La sivyo tuwape kila mtu ambaye anafanya biashara haki ya kukamata mali ya mwenzake. Kwa nini huyu opereta awe na mamlaka ya kuuza mali ya mtu wakati kuna ubishano juu ya malipo.

Kifungu kingine ambacho nina wasi wasi nacho ni kifungu cha 40. Kifungu cha 40 kinaipa mamlaka hii *Authority* kukamata meli wakati mwenye meli anadaiwa *port charges*. Sisemi kwamba wenye meli wasilipe, lakini kuna wakati ambapo kutatoka

mabishano juu ya kiwango cha malipo. Kuna wakati ambapo mwenye meli atasema hapana. Mimi usinidai kukaa kwenye bandari kwa wiki moja kwa sababu nchi yako ilikuwa na mgomo. Bandari ilikuwa na mgomo kwa hiyo, sikuweza kupakua. Au usinidai kwa sababu hakukuwa na umeme kwenye bandari kwa hiyo krini hazikuwa zinafanya kazi. Sikuweza kupakua. Haya mambo ya mabishano hivyo, ni mambo ambayo yanatakiwa kuwe na chombo kingine ambacho kinaweza kikaamua ni kiasi gani ambacho mtu anastahili kulipwa lakini kwa kuwa na kifungu cha 40 ni kwamba Mamlaka inaweza ikaamua kwa vyovyote vile bila kuhakikisha, bila ku-*prove* kwa mtu yoyote kwamba inadai hiyo meli na itakamata meli ya mtu.

Imeshatokea Mheshimiwa Naibu Spika, miaka michache iliyopita *Linea Messina* imekamatiwa mali yake na Mamlaka ya Bandari na baada ya ile mali kuuzwa ika kugundulika kwamba *Linea Messina* haikuwa inadaiwa na *THA*. Hayo mambo yanatokea ni ubinadamu. Nilikuwa nafikiria pia kwa kuwa Serikali imejitoa hakuna sababu ya kuilinda hii mamlaka kupita kiasi.

Hii Mamlaka iende ikafanye madai yake halali na kwa sababu hawa *operators* wa Meli ni watu wanaokuja na kuondoka ni Kampuni za Kimataifa ambazo zinajulikana uwezekano wa kushindwa kulipa deni wakati chombo kinachostahili kikatiba kuamua nani ana haki ya kulipwa na nani hana haki ya kulipwa kitakapoamua. Mimi nafikiria Vifungu vya 27 na 40 Mheshimiwa Waziri avifikirie sana. Nilikuwa nimempa rafiki yangu Mwanasheria Mkuu wa Serikali taarifa kwamba ningetoa *Schedule of Amendment* lakini nimefikiria badala ya kuwa controversial afadhali niende kwa kushauri nishauri, kwamba hili jambo tunalofanya hapa ni jambo ambalo ninaweza likakatisha tamaa watu ambao watataka kuleta mizigo yao hapa na watu wataanza kutumia Bandari za Tanzania. Kwa sababu kama kuna *Authority* ambayo inaweza ikakamata meli tu kwa sababu imesema lipa. Hata kama hutakiwi kulipa basi mimi sitaleta meli yangu Tanzania. Mheshimiwa Naibu Spika, kama hayo yatazingatiwa ninaunga mkono hii hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie kwenye Muswada huu wa Sheria ya Usimamizi wa Shughuli za Bandari wa mwaka 2004 Port Speed 2004. Mheshimiwa Naibu Spika naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu na kwa kweli ukiangalia Madhumuni ya Muswada huu madhumuni ya kuunda chombo hiki unaweza ukasema kwamba Muswada huu umechelewa kuletwa Bungeni ungekuja mapema zaidi ya hapo. Lakini vile vile nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa bahati mbaya sikuwepo wakati anawasilisha lakini mimi nina uhakika aliwasilisha vizuri kwa ufasaha sana na bila ya kukawia nataka kusema kwamba ninaunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie maeneo mawili:-

(1) Liko katika Ibara ya (5) ya Muswada kama ilivyorekebisha. Katika Ibara hii Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la msingi *Fundamental Objective* wanasema wenyewe, lengo la msingi la Mamlaka inayoundwa kwa Sheria hii katika kutekeleza majukumu ni

kuongeza na kuimarisha faida zinazotokana na nafasi ya Kijiografia ya nchi yetu kama nchi inayozungukwa na nchi ambazo zinategemea bandari zetu. Tanzania imezungukwa na nchi ambazo uchumi wao unategemea bandari zetu kwenye Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Zinategemea bandari zetu za Bahari ya Hindi Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na nyinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi hii ya nchi yetu kijiografia bado hatujaitumia ipasavyo, bado hatujaitumia kikamilifu, hatujajielekeza kikamilifu kuzitumia fursa ambazo tunazo kwa kutegemewa na nchi jirani kwa kusafirisha bidhaa zao kupitia katika bandari zetu. Fursa hizi hatujazitumia kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya (5) kipengele kidogo (a) mpaka (e) ndivyo hasa vinavyofafanua na kuonyesha jinsi gani Mamlaka mpya hii itakapoundwa itaimarisha, itatumia fursa ambazo tumekuwa tukizikosa kwa muda mrefu. Iwapo Mamlaka hii mpya itayoanzishwa kwa Muswada huu itazingatia na kutekeleza kwa kikamilifu vipengele hivi nilivyovisema vya Ibara ya (5) (a) mpaka (e) Sekta ya Bandari mimi nina hakika itachangia kwa kiasi kikubwa katika kukua kwa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari ni milango muhimu katika uchumi wa Taifa lolote. Milango ya Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Congo, Uganda, ni bandari za Tanzania, ndio milango yake. Zile nchi hazina milango mingine baharini isipokuwa ni Bandari za Tanzania. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutumia Sekta ya Bandari isipoteze fursa hizi kubwa ambazo nchi nyingine zinategemea kutoka kwetu kama milango yao.

Lakini ninataka niongezea jambo la pili hapa, kwamba Sekta hii ya bandari itaweza ikaipa na kuziongezea Tanzania fursa ya Kijiografia kama reli na barabara zitaelekezwa kwenye Bandari za Maziwa hayo makubwa.

Reli na barabara zitaelekezwa tena siyo barabara za udongo barabara za lami barabara za uhakika kwenye Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Bila ya kuwa na reli iliyoimarika ili iweze kubeba mizigo kutoka Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Congo na Uganda na Zambia na bila ya kuwa na barabara za lami kutoka kwenye bandari hizo ninavyosema hizo maana yake ni zile bandari zilizoko kwenye Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa na kuelekea kwenye bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara, fursa za nafasi ya nchi yetu kijografia bado tutasikosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitize hili kwamba sasa nchi kama *Mozambique*, Kenya, *South Africa*, ingependa kutunyang'anya fursa hizi na kwa kweli ingependa mizigo ya Burundi, Rwanda ipite Kenya na hii ya Congo, Zambia ipite Afrika ya Kusini. Lazima tubadili mtazamo wetu kuhusu mtandao wa barabara na kuhusu uimarishaji wa reli ya kati ndipo tunapoweza kufaidika na sisi kama Tanzania kuwa kijografia tunategemewa na nchi nyingine kwa bandari zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili liko katika Ibara ya (80). Ibara ya (80) iliyorekebisha inazungumzia wafanyakazi kuhamia mamlaka mpya. Muswada huu

umeweka utaratibu mzuri wa wafanyakazi kuhamia mamlaka mpya. Lakini ningependa nishauri mambo mawili:-

Kwamba Wafanyakazi waelimishwe vizuri juu ya utaratibu huu utaoanishwa katika Muswada huu au utakaoainishwa katika Sheria hii itakapokuwa Sheria na jinsi gani mikataba yao ya kazi inavyoana au inavyohusishwa na Sheria hii au Muswada huu mpya. Ibara ya (80) kifungu cha (2) katika marekebisha, inazungumzia juu ya Wafanyakazi ambao hawatahamia mamlaka mpya na kwamba watalipwa maslahi yao kwa mujibu wa Sheria na Taratibu za Ajira na Masharti ya Kazi.

Mimi ningeshauri kwamba hawa Wafanyakazi wamelitumikia Shirika la Bandari kwa miaka mingi. Wengine wametoka huko *East Africa, Harbours* huko wamekuwa na Shirika hili kwa miaka mingi na sasa wamekosa nafasi ya kuingia katika Shirika jipya au katika Mamlaka mpya. Mimi nilikuwa naomba Serikali iwafikirie kuwapa mkono wa kheri. Mkono wa kheri ni mkono mzuri tu ni wa kheri kwamba umekaa na sisi kwa miaka mingi pamoja haki zako za msingi basi tunakutakia kila la kheri.

Mimi nina uhakika idadi ya wafanyakazi wa namna hiyo hawatakuwa wengi kwa sababu kwa utaratibu wa Muswada huu Wafanyakazi karibu wote watahamia katika mamlaka mpya kwa hiyo watakaobaki ni wachache sana ambao mimi nina uhakika Serikali inaweza ikafikiria namna ya kuwapa mkono wa kheri ili waweze kwenda kuanza maisha yao vizuri zaidi.

Ningependa kushauri kwamba malipo yao yaandaliwe mapema ili yawaondolee usumbufu wa kuyafuatilia mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ushauri na mchango huo mimi nasema tena Muswada huu ni mzuri ninauunga mkono mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika Muswada huu wa Sheria ya Usimamizi ya Bandari (*TGA*). Baada ya kupitia huu Muswada, nakumsikiliza Mheshimiwa Waziri akiuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, nimeridhika na mawasilisho ya Muswada wenyewe na Maudhi na Maeneo na Malengo ya huo Muswada na kwa sababu hiyo naunga mkono Muswada huu mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuunga mkono napenda nimpongeze sana Waziri kwa maeneo mbalimbali hasa Malengo Matatu aliyoyaonyesha kwamba Shabaha ya Muswada huu itakuwa:-

- (i) Kuimarisha bandari kama kiungo katika kuendeleza uchumi na kukuza biashara.
- (ii) Bandari itakuwa kichocheo kufanikisha Mfumo wa Utandawazi.
- (iii) Itachochea Uwekezaji.



Mheshimiwa Naibu Spika, ili malengo hayo matatu yaweze kufanikiwa chombo kitakachoundwa hii Mamlaka ya bandari, kitabidi kichukue hatua za makusudi kurekebisha dosari ambazo Mheshimiwa Waziri amezitaja zinazohusu bandari zilizoko katika Maziwa yetu Makuu. Mimi nitajielekeza katika mchango wangu wa kwanza katika Ziwa Tanganyika. Kitu kimoja kinachovutia Uwekezaji ni usalama wa hao wanaoendesha biashara katika eneo husika. Usalama unaopashwa kuwepo kati ya bandari moja na bandari nyingine.

Uchukuzi kwa njia ya Maji unaweza kulinganishwa kwa namna fulani na Uchukuzi wa Anga. Uchukuzi wa Anga Miundombinu yake iko katika Viwanja vya Ndege kati ya kiwanja kimoja na kiwanja kingine ndivyo ilivyo katika uchukuzi kwa njia ya maji kati ya bandari moja na bandari jingine. Usalama wa anga ni muhimu na ndio maana kunakuwa na vyombo vya usalama kama Rada na hata abiria unapopanda ndege unaambiwa zima simu yako ya mkononi ili usivuruge mawasiliano na hivyo kusababisha hatari kwa ndege. Meli ni hivyo hivyo na uwekezaji katika uchukuzi kwa njia ya maji watavutiwa kama kati ya bandari moja na nyingine kuna usalama na usalama ambao unakosekana kwenye Ziwa Tanganyika ni kwamba halijafanyiwa uchunguzi au *survey* ambayo ingewezesha kuwepo na nyenzo zitakazomwezesha nahodha kuweza kuendesha meli kwa usalama. Kama ilivyo katika anga ziko nyenzo kubwa tatu ambazo nahodha wa Meli anazihitaji. Nyenzo hizo ni Dira, Dira *and Compus*, Rada na *Chart* za kuongoza meli. Wanasema kwa kingereza *Navigational Charts*.

Hizi ni muhimu zaidi kwa sababu zinamwonyesha huyo nahodha maeneo mbalimbali ya Ziwa au ya Bahari, mahali ambapo kuna kina kifupi, mahali ambapo kuna vitu ambavyo viko chini ya maji ambavyo rada haiwezi kuvionyesha au dira haiwezi kuzionyesha kwa sababu dira itaonyesha tu mwelekeo. Mashariki ni pande za dunia ambapo rada itamwonyesha vile vilivyo juu ya maji lakini vilivyo chini ya maji kama visiwa au kama miamba ambao ni hatari kwa meli haviwezi kuonyeshwa na hizo nyenzo mbili.

Lakini zile *Navigational Charts* zinaweza kufanya hilo. Sasa Ziwa Tanganyika halijafanyiwa ukaguzi unaowezesha kuwa na *Navigational Chart*. Sasa nilipata faraja nilipokuwa nafahamishwa kwamba kuna maelekeo ya hilo kufanyiwa kazi. Sasa kabla halijafanyiwa kazi, kwa hiyo bandari ya Kigoma au Ziwa Tanganyika ili kuwavutia Wawekezaji itakuwa ni ngumu kama hilo halijawekwa sawa. Kwa hiyo, hilo ndio wito wangu kwa chombo hiki kitakachoundwa kisimamie hilo.

Tatizo la pili ambalo litapashwa liangaliwe ni ndani ya Bandari ya Kigoma, ni kwamba bandari inaendelea kufukiwa na mchanga unaoporomoka kutoka katika Halmashauri ya Mji wa Kigoma kiasi kwamba uegeshaji wa meli zilizopakia unakuwa mgumu. Kiasi kwamba inatangulia meli ambayo kupakia inakuja meli nyingine iliyopakia ili ipate kina cha kutosha. Sasa nimefarijika na kifungu kinachoonyesha kwamba mamlaka hii itasimamia usafishaji (*draining*) uchimbaji ili kina kiweze kuwa ni cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la tatu ambalo nadhani ni muhimu mamlaka hii ijielekeze ni kujenga Magate. Ni bahati mbaya Mheshimiwa Naibu Spika kwamba katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika ambayo ni sehemu ya Jimbo langu la Kigoma Kusini vituo vipatavyo kumi hakuna hata kimoja chenye Gate. Hii inaleta usumbufu mkubwa na hatari hata kwa meli ile inayofanyakazi kwa sababu inasimama kwa kina kirefu na Upakiaji wa Mizigo na Upakuaji unakuwa ni mgumu sana na wa hatari sana. *(Makofi)*

Nakumbuka tulishawahi kuzungumza na Mheshimiwa Waziri kwamba angalau kuwepo kituo kimoja cha katikati kituo cha Buhingu kijengewe *gate* kwa sababu maeneo yale yana bidhaa nyingi za daga, za kilimo, za misitu na pia ni kituo ambapo Watalii wanaotembelea Mbuga ya Taifa ya Mahale wanashukia pale.

Sasa wengi wanapooa jinsi upandaji na ushukaji unavyokuwa ni wa kutisha Watalii hawawezi kurudi katika mazingira ya namna hiyo. Kwa hiyo, kuna sababu ya kufikiria kituo kama hicho kupewa *gate* kwa sababu za kiuchumi na usalama katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu wa Spika, eneo jingine ambalo ni vema nilichangie ni eneo iliyo katika Kifungu cha Muswada huu Kifungu Na.(53) hiki kifungu kinasema naomba nisome kwa Kiingereza kama kilivyo: *“The Harbour Master may direct the Owner, Master or Agent of any vessel intending to enter or leave a port to furnish, before to entering or leaving the port such information as the Harbour Master may require relating to the vessel, its cargo and the estimated time of entering or leaving the port”*.

Hapa nadhani kwa sababu tunazungumzia taarifa ya meli inayoingia ndani ya bandari ni taarifa ambayo ni za lazima zipatikane kwa sababu ni pamoja na ukubwa wa meli ili iweze kupewa *pilotage*. *Pilot* wa kuingiza ndani na kuitoa na inapokuwa imekuwa namna hiyo maana ni gharama meli itakaposimama pale bandari ile basin inaposimama inalipa.

Sasa siyo suala la bei hapa, mimi ningeona hapa ni shallow huyo *Harbou Master shall require or direct the owner* atoe hizo taarifa kwa sababu zitatumika katika kufanya makadirio ya gharama gani ambazo meli hiyo itapashwa ilipe.

Ndio maana nikiunganisha na mchango wa Mheshimiwa Dr. Lamwai sina hofu kabisa ya kuikamata meli kwa sababu meli inakamatwa baada ya mawasiliano marefu sana na ambayo yanakuwa yamezingatia mikataba iliyofikiwa kati ya Bandari na Wakala wake inayohusu gharama za kulipwa.

Kwa hiyo, ni baada ya mawasiliano inapofikia kwamba halipi na mkataba kwa mfano *chart par* imeeleza kwamba meli isikae bandarini kwa muda fulani na pesa hizi zinapashwa ziwe zimetumwa kabla ya meli kufika ndizo Sheria zinavyoelekeza hizi *Maritime Law* katika masuala yanayohusu bahari Uchukuzi kwa njia ya Bahari. Sasa nadhani kushika meli inakuwa ni hatua ya mwisho lakini mawasiliano yanakuwa yamekwisha fanyika ya kutosheleza kulingana na mikataba ambayo *Operator* na huyu Mtu wa Bandari wanakuwa wameshaipitia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie eneo la tatu kwa kuonyesha furaha yangu ambayo iko katika Muswada huo ya kuonyesha kwamba Muswada huo kwenye Schedule imeonyesha kwamba umeutambua Bandari ya Ujiji kama ni Bandari Ndogo.

Hii ni bandari ya Kihistoria wote tunajua na kutokana na umuhimu wake tangu wakati wa utumwa bandari hii ndio ilikuwa inapitisha Watumwa na kadhalika na imeendelea kuwa inatoa hudumu lakini bila kutambuliwa kuwa ni Bandari Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu maandalizi haya yalivyofanyika chini ya Muswada huu kwamba inapoimarishwa bandari ile na biashara itakapongezeka kati ya Bandari ya Kigoma na nchi za jirani basi Bandari ile ya Ujiji ambayo haiko mbali sana kutoka Kigoma itapunguza msongamano katika Bandari ya Kigoma. Kwa hiyo napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kuliona hili na kulifanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru pia nifurahie *delegation* au ujumbe mzito wa maafisa kutoka Wizara ya Mawasiliano waliotembelea Ukanda wa Ziwa Tanganyika na tukawa kwenye meli pamoja. Hawa walijionea hali halisi na naamini kwa kufanya ziara kule imetoa fursa ya wao kuelewa mazingira ya Ziwa Tanganyika na hivyo wataimarisha hili Shirika au hii Mamlaka inayoundwa kuweza kusimamia kwa karibu sana maendeleo ya bandari katika Ziwa Tanganyika.

Hivyo watakuwa katika nafasi kubwa ya kutuunga mkono kwa ufanisi mkubwa zaidi na nchi za Maziwa Makuu ambazo Kigoma ni mlango mzuri wa kuunganisha na Bandari ya Dar es Salaam. Hivyo kuvutia biashara kutoka nchi hizo zinazozunguka Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa na ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa *The Ports empty*. Umekuja kwa wakati muafaka na ningependa niungane na Wabunge wenzangu kuunga mkono kabisa na ninaona kazi yetu ni kusema pale ambapo tunaona tunaweza tukatoa mapendekezo kwa mambo ambayo yanaweza yakaboreshwa. Tunaweza tukaangalia baadhi ya mamlaka ambazo zimeanzishwa kwa miaka michache iliyopita zimebadilisha sana sura ya Tanzania kiutendaji na mimi nafikiri *efficiency* itaongezeka sana katika bandari yetu baada ya hii Sheria kupitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie maeneo mawili tu. La pili kama nitakuwa na nafasi.

- (1) *Clause No. 5* na kipengele kidogo cha (b) kinachozungumzia usalama wa *ports* kwa ujumla.
- (2) Ushindani wa kibiashara kwa hizi bandari zetu na zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna nchi kubwa ukiangalia kuanzia ukiimaliza Kenya unianza Tanga mpaka Dar es Salaam, Lindi kwa rafiki yangu Membe, Mtwara ukielekea upande mwingine unaenda Mafia. Ukitoka Mafia kuna Zanzibar na Zanzibar na Pemba ni maeneo makubwa sana ya *water ways* na kama usalama wa nchi ina maana yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika ninaomba nimuunge mkono kabisa Mheshimiwa Masumbuko Lamwai kwa kusema kwamba Sheria hii ikipita kama Sheria ya Tanzania Bara peke yake bado kuna maswali mengi sana hayajajibiwa na mimi ninasema hivyo *specific* kwa suala la usalama. Najaribu kufikiria tatizo tulilo nalo la Ziwa Tanganyika la usalama na kwa sababu bandari ni kama ndege ni kama Viwanja vya Ndege ambavyo watu wanaingia na kutoka mizigo inaingia na kutoka na kwa sababu tuna nchi kubwa sana ambayo hakuna mtu yeyote anayeweza kum-*monitor* mtu akitoka na Mtumbwi Bagamoyo kwenda Zanzibar.

Hakuna mtu yeyote atayekusimamisha. Kwa hiyo, suala hili la nani atakayepewa kazi ya kusimamia *operations* za bandari kwa upande wa *business implication* ina maslahi ya moja kwa moja na suala zima la ulinzi na usalama na hili suala siyo Tanzania peke yake. Ukiangalia Bandari ya *Durban South Africa*, kipengele ambacho kina-*control* na kinamkagua nani anaingia na nani anatoka ukitengeneza Mamlaka ambayo inampa yule mwenye mamlaka asilimia mia moja ya nguvu na huwezi ukamfanyia *vetting* wala huwezi ukam-*control* kutakuwa na tatizo sana la sisi kuja ku-*control* vitu vinavyoingia na kutoka vinavyohusiana na suala nzima la usalama na tunafahamu kwamba bandari zinatumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuingiza Madawa ya Kulevya wala huwezi mkam-*control* kutakuwa na tatizo sana la sisi kuja ku-*control* vitu vinavyoingia na kutoka vinavyohusiana na masuala mazima ya usalama na tunafahamu kwamba bandari zinatumiwa Mheshimiwa Naibu Spika, kuingiza madawa ya kulevya zinaingiza ama zinatoa hiki tunachokiita *human tracking* ambalo ni tatizo kubwa sana na linazidi kuongezeka. Bandari zinatumiwa kwa kuingiza silaha nyepesi nyepesi na silaha kubwa kubwa na tunajua kwamba bandari aidha ya Dar es Salaam au ya Mombasa au ya *Durban South Africa* ndiyo ambazo zimetumika kwa njia moja au nyingine kuwapatia silaha hawa watu wanaopigana huko Congo na sehemu zingine hamna mahali pengine wamezipata zaidi ya ya bandari ambazo zipo. Huu mwambao na ujasusi wa kimataifa kwa ujumla uta-*target* bandari ambazo zinausalama hafifu na sasa hivi nina uhakika Mheshimiwa Naibu Spika, tuna uwezo wa kutumia *radar* inayotumika kwenye uwanja wa ndege kufanya *surveillance* kwenye kilomita na kilomita za bandari na *water ways* za Tanzania.

Lakini nina wasi wasi jambo la kwanza kwamba wewe unawezaje kuulinda Tanzania kilomita zaidi ya 2500 kuanzia Tanga mpaka Mtwara na ukahakikisha kwamba

hakuna mbaya anaweza akakuingilia. Kwa sababu mtu aliyeshika, jambo la kwanza *in the future business it will depend* na usalama na watu watakapo- *feel* kwamba ukienda bandari ya Dar es Salaam ni salama, Bandari ya Tanga ni salama watapeleka meli zao.

Suala lingine ni *efficiency* ni kiasi gani mizigo ya watu itapakuliwa na watu kuondokana na ukiritimba mwingine ambao ningependa kuelezea kwa dakika moja inayofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani suala la hii sheria liunganishe na Zanzibar. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaanza kuogopa ogopa mpaka lini kwa suala kama hili kutokuliweka mamlaka hii itawale Zanzibar, itawale Pemba, itawale na Tanzania Bara kama tunavyoifahamu na mimi nina amini Mheshimiwa Naibu Spika, hawa walioitunga hii sheria wamefikiria *now we told you expect*.

Mimi suala langu ni moja tu kwamba tutahakikishaje nchi hii ina usalama wa kutosha kama tukitofautisha mamlaka ambayo inaingiza na kutoa vitu muhimu kama hii mamlaka ya bandari na sehemu zingine wamefanya ubinafsishaji wa bandari na makampuni yanayoendesha bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini huwezi ukabinafsishaji vitengo hivi muhimu pasipo kuwa-*vet* wale unao wapa hiyo kazi. Kuna watu wengi hapa wanakuja Tanzania wametelemka pale *Dar es Salaam* wameingia kwa sababu sisi si watanzania na wanajiita *investor* na wana kampuni imeandikwa *Limited XYZ Limited*. Kwanza wanapewa viti vya mbele. Halafu pili wanasikilizwa zaidi, halafu tatu hatujawa na *system* jinsi ya kuwafanyia *vetting* hawa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kuwa *vet* hawa watu bila kutumia *intelligence*, huwezi kabisa mtu akikuambia mtu ametoka *South Africa* mwingine akuambie ametoka Marekani au ametoka China. Sisi tutamjuaje na *system* ya kuwa *vet* hawa watu lazima iwe *developed* na ni *system* ambayo itatusaidia sana kumjua huyu ni nani. Sasa sheria ambayo tunawatungia ya kuzipa hizi kampuni mamalaka makubwa sana kwa nia nzuri tu ya kuwavutia waje baada ya Mwaka mmoja, miwili nchi hii watakao kuwa wanatembea vifua mbele ni wageni na dalili tunaziona na tuna nchi nyingi sana Mheshimiwa Naibu Spika, ambazo wame-*privatize* lakini wamefanya hivyo kwa njia ambayo hai-*jeopardize* sisi wenye nchi na inawafanya waendeleo kuheshimu sheria za nchi ambayo wanafanya kazi.

Kwa hiyo, ningependa niseme tu kwamba suala zima la usalama wa bandari ambao utasimamiwa na hii *port safety* ni lazima uhusiane na usalama mzima wa nchi kuhakikisha kwamba nchi yetu iko salama kwa *water ways*. (*Makofi*)

Suala la pili ni lazima ama fedha zitolewe ama iandikwe jinsi gani Serikali itakuwa inatoa fedha za usalama hakuna mgeni yeyote aliyekuja hapa kufanya biashara utamtegemea yeye aweke fedha ya kuhakikisha kwamba anafanya *investigation* anafanya usalama anahakikisha kwamba kila kinachoingia na kutoka ametumia fedha za kutosha

kuhakikisha kwamba ni kwa ajili ya maslahi ya nchi yake. Kwa sababu mfanyabiashara anataka kwanza fedha wanaita *maximization of profit*.

Kwa hiyo, sijajua itakuwaje lakini ninapendekeza kwa Mheshimiwa Waziri anayehusika kuwe na *provision* ambayo itataja kwamba Serikali itakuwa inahusika moja kwa moja na gharama za kiusalama wa nchi na la pili ningependa Waziri anayehusika pia atujibu hili na anijibu ni juu ya *strategic investors* watakapo ingia kwenye suala la bandari najua wapo lakini nataka tujue au hili bunge lielezwe wana wa-*vet* namna gani na ile *vetting system* ikoje na inaweza ikawa *proved* vipi kusudi tu usije ukafika mahali una mtu mmoja ameshika bandari zako una huyo huyo mjomba wake ameshika benki zako huyo huyo, mwingine ameshika barabara zako utafika mahali wajukuu watajuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari itafanikiwa kibiashara kama kutakuwa na ushindani wa dharti na sasa hivi *competition* sisi wateja wetu ni hao hao hawabadiliki, wateja wa Tanzania watakuwa ni Tanzania yenyewe, Watakuwa ni Congo, watakuwa ni ndugu zetu wa Zambia, Malawi kidogo lakini Rwanda, Burundi, Uganda na labda sehemu za kusini kabisa Kaskazini kabisa mwa Sudan. Hao ndio wateja wakudumu wa bandari za Tanzania. lakini *competitors* wale watu wanaotaka kuchukua biashara za Tanzania mkubwa zaidi ni Mombasa na *Durban South Africa* na tunafahamu jinsi ambavyo mwekezaji mmoja anaweza akaja akachukua shirika lako la ndege na kuliua nimetoa mfano Mheshimiwa Naibu Spika, anaweza akaja mwekezaji aka-*bid* fedha nyingi na wale wanaokaa kupitisha wakisema huyo ametoa fedha nyingi lakini *strategically* ame-*bid* ili baada ya miaka mitano aliuwe ilo shirika anyanyue la kwake na mimi ningependa *for the sack of this country* wale ambao wamepeleka dhamana ya kubinafsisha tunafanya hii kazi leo lakini kesho ni watoto wetu ni wajukuu zetu *for the sack of this country*. Hili suala liangaliwe mara mbili mara tatu. (Makofi)

Kama mimi ningekuja nikainunua kampuni ya *coca-cola* kwa sababu mimi ninataka lazima niwe nauza pepsi kuliko *coca-cola* nitainunua halafu nitahakikisha tu kwamba mauzo yanapungua na baadaye nafunga au namuuzia mtu mwingine halafu kama kawaida mnakunywa pepsi na hilo limetokea katika nchi nyingi. Waganda wameshindwa kabisa kufufua *Uganda Air Lines* na kuna mifano mingi sana ya nchi ambazo waliingia kwa nia nzuri na katika *bidding process* huwa tunaangalia ni nani aliyetoa pesa nyingi na tunajua kabisa kwamba *the highest bidder* wakati mwingine *a crazy highest bidder* anakuwa na *motives* ambazo *sometimes* ni *questionable* na naomba sana sana tuliangalie kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa kumalizia na lile ambalo ulilisema hapo nyuma wakati wa kikao cha Bunge la Bajeti hatutaweza kufikia ulinzi kamili wa nchi kwa kuwategemea watu wa nje na kwa kuwategemea wawekezaji na kwa ulinzi wa bahari na maji *complications* na ugumu uliopo katika kulinda maeneo ya mbali ya maji ni mgumu kuliko kulinda mipaka kwa sababu mnaweza mkapeleka wanajeshi wakakaa.

Sasa ni lazima nchi hii ifikie kuweka *mean-navy* siku chache zilizopita *Ivory Coast* unajua wanaendelea na tatizo la mapigano ya wao kwa wao. Nchi ambayo ni wachokozi kabisa ambao kwa heshima sitawaja wamekwenda wakaungana na wapinzani

wanawapelekea silaha na wale wapinzani wanapiga watu na wanaua majeshi ya Serikali na Serikali yao wakapeleka majeshi wakatwanga wakawapiga na hao wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichotokea ndani ya muda mfupi wote tunafahamu ziliondoka ndege mbili nafikiri za kijeshi zikaenda kusambaratisha kabisa jeshi la anga la nchi hiyo. Kulikuwa na hizi *helicopter gun ships* tunazifahamu, *Mig Fighters* zile za wa-Russia wakizifuata waka *zi-target* zote zikaisha ni kwa sababu tu kwamba *strategically* hawa jamaa hawajakaa sawa wamefika wanavi-*helicopter guns* vitano.

Lakini sisi tunavyovingapi *surveillance* ambayo tunaweza tukaifanya kwenye mwambao wa pwani kama ujasusi ukifanyika katika Jiji la Dar es Salaam na Mtwara tunaweza tuka-*dispatch helicopter* ama ndege kwa kiasi gani na hizo zinasaidiana ni hizi *mean navy* za baharini ambazo nchi nyingi sana kwa zaidi ya dola milioni 100 wameweza kuwa nazo na watu watakuambia ni *expensive*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningepomba sana sana tulifikirie kwa ajili ya manufaa na kwa ajili ya maslahi nchi yetu kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumza. (*Makofi*)

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili nami nichangie mchango Muswada huu mimi nataka nianze tu kwa kusema kwamba Watanzania wengi wanategemea bandari ama kwa kusafiri ama kwa kusafirisha lakini Watanzania wanategemea bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka nielekeze michango yangu katika maeneo mawili makubwa. Eneo la kwanza nataka nizungumzie masuala ya meli mbovu na boti mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina bandari nyingi kama walivyosema wenzangu. Lakini mimi nataka nizungumzie bandari ya Dar es Salaam. Bandari ya Dar es Salaam sasa hivi imekuwa ni jaa, ni jaa la kukusanya mameli mabovu na boti mbovu ambazo Serikali haijatafuta maeneo maalum ya kuziweka.

Sasa kwa maana hiyo meli nyingi zinazotoka nje zinashindwa kupita bandarini kutokana na msongamano wa meli mbovu na boti mbovu. Sasa mimi mawazo yangu na mchango wangu naomba hizi meli na boti zitafutiwe maeneo mengine ziwekwe ili meli kubwa zipate kuingia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine ambalo nataka kulichangia ni suala la mkusanyiko wa magari bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi huagiza magari yao lakini kwa bahati mbaya yanapofika bandarini wanashindwa kuyachukua magari yao kutokana na ushuru mkubwa. Sasa magari yale baada ya kuyatafutia mahali pa kuyapeleka magari yale yote yanakusanyika bandarini sasa ndugu Mheshimiwa Naibu Spika, nachotaka kukiongea

hapa kwamba kama hili ni jukumu la bandari basi. Kama ni jukumu lao waendeleo kuziweka kama sio jukumu ni jukumu la Wizara ya Viwanda na Biashara basi watafutiwe maeneo maalum ya magari haya yatafutiwe mahala yawekwe. Vinginevyo itakuwa ni vurugu tupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naomba masuala haya ya magari yatafutiwe mahala yawekwe na magari haya yanakuwa mengi kwa sababu ushuru tu ni mkubwa unaweza wewe ukanunua gari Dubai kwa shilingi 2,000,000/= lakini njoo uipeleke Tanzania ushuru wake ni zaidi hata ya kunulia kwa hivyo ndiyo maana magari mengine yanaendelea kubaki pale bandarini. *(Makofi)*

Sasa mimi nasema kwamba Serikali lazima ifikiriea namna gani ya kuyaweka haya magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho naomba nichangie masuala ya kontena, suala la makontena nalo pia limekuwa kero kwa sababu makontena mengi baada ya kuleta hayajatafutiwa mahala gani yawekwe makontena hayo. Kwa hivyo naomba vile vile Serikali ifikirie namna ya kuwatafutia makontena pa kuyaweka badala ya kukusanya pale bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilisema kwamba angekuwa wa mwisho nilitarajia angetumia muda wa dakika kama kumi hivi naona zimebaki dakika kumi tano. Lakini kwa sababu niliaandaa kuwa yule awe wa mwisho basi nadhani tuishie hapo.

Sasa kesho wamebaki wachangiaji wanne. Nadhani muda utapatikana hao wachangie, halafu Mheshimiwa Waziri aweze kujibu. Waliobakia ni Mheshimiwa Benedict K. Losuruta, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Wilfred M. Lwakatare na Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah. Baada ya maelezo hayo sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.45 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jamanne tarehe  
9 Novemba, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*



